

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nane – Tarehe 15 Aprili, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Ushindani kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Fair Competition Commission (FCC) for the Financial Year 2008/2009*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji Leseni kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Mwaka wa Fedha 2007/2008 (*The Annual Reports and Audited Accounts of Business Registrations and Licensing Agency (BRELA) for the Financial Years 2006/2007 and 2007/2008*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 100

Mpango wa Kutwaa Ardhi kwa Ajili ya Kupanga na Kupanua Mji

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.N.Y. MHE. PHILIPA G. MTURANO)
aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kutwaa ardhi za Wananchi wa Kata ya Somangila, Mitaa ya Kizani na Mwera kupima viwanja kwa lengo la kupanua mji; na kwa mujibu wa Sheria ya Vijiji ya Mwaka 1999 na Kanuni zake zinazitaka mamlaka zinazotwaa ardhi za Vijiji kulipa fidia kamili ya haki na ilipwe kwa wakati:-

(a) Je, ni Wakazi wangapi wa Mitaa ya Kizani na Mwera wamelipwa fidia ya mali zao, usumbufu, malazi, upotevu wa faida na usafiri?

(b) Je, mpaka hivi sasa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imekamilisha zoezi la ulipaji fidia kwa mujibu wa Sheria husika?

(c) Ni kiasi gani cha fedha kimeshatumika katika zoezi hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, hadi sasa hakuna Mkazi wa Mtaa wa Kizani na Mwera aliyelipwa fidia. Serikali inaendelea kutekeleza utaratibu wa kulipa fidia kwa Mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 ili Wakazi wa Mitaa ya Kizani na Mwera walipwe fidia ya mali, usumbufu, malazi, upotevu wa fidia na usafiri. Jumla ya Wakazi 1,050 wamethaminiwa mali zao (mazao, ardhi na nyumba 249).

Mheshimiwa Spika, hati za fidia kwa ajili ya mali za Wananchi wa Mitaa ya Kizani na Mwera zimekamilika. Zoezi la kulipa fidia kwa Wananchi wa mitaa hiyo litaanza rasmi tarehe 18 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, imekamilisha taratibu zote na ipo tayari kuanza kuwalipa fidia Wakazi wa Mtaa wa Kizani na Mwera kufuatia kukamilika kwa mchakato wa kupata fedha ya mkopo kutoka Benki ya Raslimali ya Tanzania (*TIB*).

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka huu wa Fedha (2010/2011), Serikali inatarajia kutumia kiasi cha shilingi bilioni 8.0, mkopo kutoka Benki ya Raslimali ya Taifa kati ya hizo shilingi bilioni 7.5 zitatumika kwa ajili ya kulipa fidia kwa Wananchi wa maeneo husika.

MHE. PHILIPA M. MTURANO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa ni jana tu nimepata taarifa kwamba, Serikali imeanza kufanya utaratibu wa kuwalipa kwa kuwapelekea Wananchi fomu za kujaza, lakini vilevile kwa kuwa wamesema kwamba, wanalipa kwa *square meter* moja shilingi 750 halafu Serikali itawauzia kwa shilingi 6,000:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki?

(b) Watu hawa ni wale ambao walihamishwa enzi zile za Mwalimu Nyerere kupelekwa Gezaule na Kimbiji; sasa wanapoondolewa pale wanapelekwa wapi? (*Makofi*)

SPIKA: Haya ndiyo maswali, yanaulizwa vizuri, *direct and clear*; ninakupongeza sana. (*Makofi*)

NNAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Philipa Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kulipa fedha kidogo katika Halmashauri linao utaratibu wa kisheria kwamba, kwanza, inathaminiwa sehemu ya ardhi inayochukuliwa na thamani ni ile ile ambayo imeandaliwa kiserikali; haina matatizo na wala haina shida katika hilo. Kama kumetokea tatizo la kulipwa fedha kidogo, hilo litakuwa ni kosa lililotendwa na Watendaji wetu pale. Kwa hiyo, ninaweza kuahidi kwamba, nitalifuatilia hilo ili kuweza kutoa majibu yaliyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali inapotaka kuchukua ardhi eneo ambalo inataka litumike au kwa kupanua maeneo ya miji au kuliendeleza kwa shughuli nyingine ya uwekezaji au vinginevyo; hatua ya kwanza ni kwamba, inakutana na Wananchi waliokaa kwenye eneo hilo kuzungumza nao ili kuweza kukubaliana na hatua utakapotangaza hatua zote za kiserikali, baadaye Serikali inatoa tangazo la kuonesha nia ya kuchukua eneo hilo. Kwa hiyo, eneo hilo linapotaka kuchukuliwa lazima kuwe na mawasiliano kati ya Serikali na Wananchi walioko pale na ni lazima waridhie na wakisharidhia, taratibu za kawaida za uthamini wa eneo hilo zinafanyika na baada ya uthamini, taratibu za malipo zinakamilishwa.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa nyakati tofauti, Viongozi wa Serikali wamekuwa wanatoa taarifa zinazogongana kuhusiana na bomoabomoa ambayo ilikuwa inaendelea katika maeneo kadhaa ya nchi yetu, ambapo ardhi imekuwa ni chanzo cha ugomvi mkubwa kati ya raia na Serikali:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa Bunge na kwa Wananchi kwamba kinachoongoza Serikali katika Sera ya Ardhi ni kauli za Viongozi au ni Sheria? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ninaomba ujibu swali hilo.

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Mbowe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaongozwa na Sheria. Katika masuala ya Ardhi, kuna Sheria Na. 4 ya Mwaka 1999, Sheria Na. 5 ya Mwaka 1999, Sheria Na. 7 na Sheria Na. 8 ya Matumizi ya Ardhi za Mwaka 2007 ambazo zinafuatwa. Katika suala la barabara, kuna Sheria Na. 13 ya Mwaka 2007 ambayo inaendana pia na mabadiliko ya Sheria Na. 66, Cap. 167 ya Mwaka 1967. Kwa hiyo, Sheria ndiyo inayoongoza na ningependa kujibu kwamba, Serikali ya CCM inaongozwa na Sheria na ndiyo maana

hata tunapoapa huwa tunamalizia kwa kusema tutalinda Sheria na kumwomba Mungu atusaidie. (*Makofi*)

Na. 101

Vituo vya Afya Nchini

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Serikali ina nia njema sana ya kupeleka Zahanati na Vituo vya Afya katika Kata na Vijiji, lakini zile zilizopo hazifanyi vizuri kutokana na kasoro mbalimbali:-

(a) Kwa nini Serikali isipandishe hadhi baadhi ya Zahanati zilizojengwa na Taasisi za Kidini kama Lukuledi, Nangoo na nyingine katika Mkoa wa Mtwara ili ziwe Vituo vya Afya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Kituo cha Afya Wananchi wa Chiungutwa kutokana na kuwepo watu wengi?

(c) Je, Serikali itawathibitishia Wananchi wa Mnavira kwamba itapeleka Wataalam na vifaa watakapomaliza ujenzi wa Kituo cha Afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Agness Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, inaelekeza Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali kujenga Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata katika sehemu ambazo hakuna vituo hivyo. Zahanati ya Nangoo iko karibu na Hospitali Teule ya Ndanda, umbali wa kilomita tatu. Aidha, Zahanati ya Lukuledi ipo katika Kata ya Chiwale, ambapo kuna Kituo cha Afya cha Chiwale. Kutokana na sababu hizo, haitakuwa busara kwa Serikali kupandisha hadhi Zahanati hizo kwa kuwa Vituo hivyo vipo karibu na Vituo vya Afya na Hospitali nyingine katika Kata hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuipandisha hadhi Zahanati ya Chiungutwa kuwa Kituo cha Afya katika Mpango wa Maendeleo wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa Mwaka 2012/2013.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka vifaa tiba na Watumishi katika Kituo cha Afya Mnavira kitakapokamilika. Aidha, vifaa vingine vimenunuliwa kupitia Mfuko wa Pamoja na Ukarabati (*Joint Rehabilitation Fund*), ambavyo ni pamoja na vitanda vya kujifungulia wajawazito na samani. Katika mwaka wa 2010/2011, Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 40.0 kupitia Fedha za Ruzuku ya

Maendeleo (*Capital Development Grant - CDG*) ili kuendelea kujenga Kituo cha Afya cha Mnavira.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kumwuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Hospitali ya Ndannda ni Teule na inatumika kama Hospitali ya Rufaa kwa Wakazi wa Mkoa wa Mtwara, Lindi na hata Msumbiji na hivyo kusababisha msongamano mkubwa na huduma duni; na kwa kuwa fedha zinazopelekwa katika Halmashauri kwa ajili ya Mpango wa MMAM ni kidogo sana:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza fedha katika mpango huo ili kuziwezesha Halmashauri za Wilaya kuharakisha ujenzi wa Vituo vya Afya kama Sera ya Afya inavyoelekeza? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agness Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kuongeza Vituo vya Afya ni mipango ya Halmashauri yenyewe kwa kuweka kipaumbele kwamba ni vituo vingapi vinahitajika ndani ya wilaya na mtapenda kuanza na ujenzi wa vituo vingapi. Kwa hiyo, Baraza la Madiwani litaweka utaratibu wake. Serikali inapeleka fedha zikiwemo na hizi za Mpango wa MMAM na pia ipo *Capitation Development Grant*; zote hizo ni zile fedha zinazosaidia kuboresha na kusaidia jitihada za Wananchi walioamua kujenga Vituo vya Afya kadiri ambavyo Baraza la Madiwani limeweka kipaumbele katika ujenzi wa Kituo cha Afya ili kupanua na kuongeza Vituo vya Afya.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa ninapenda kumwuliza swali kwamba, kutokana na hali ilivyo katika Wilaya ya Masasi kwa kuwa na Hospitali moja tu Wilaya na kwa jiografia ya Jimbo la Lulindi inahitajika kupatikana hospitali nyingine:-

Je, Serikali itakuwa tayari baada ya mchakato wa Halmashauri ili kukipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Lupaso ili kiwe Hospitali badala ya kuendelea kuwa Kituo cha Afya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kupanua vituo zaidi ili kuongeza na kuboresha huduma ya afya ipo, lakini kwanza Halmashauri yenyewe ioneshe nia kupitia Baraza la Madiwani na yeye mwenyewe akiwa miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani, waanze mchakato na wakitupa taarifa ya kuanza kwa mchakato huo, Serikali inaweza kupeleka *support* kupitia Mpango wa MMAM, lakini pia ile *Capital Development Grant* ili kusaidiana na Wananchi wale kuweza kupandisha hadhi baadhi ya Vituo vya Afya vilivyopo.

Na. 102

Umuhimu wa Barabara Kimawasiliano

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Barabara ni muhimu kwa shughuli za maendeleo:-

Je, Serikali itapandisha lini hadhi barabara inayoziunganisha Wilaya za Chato, Geita na Mbugwe kutokea njia panda ya Lumasa, Kaduda, Ipalamasa, Magenge, Nyikonga, Lalembelea, Kashelo, Bugalagala, Mbogwe, Nyasato, Lugunga hadi Masumbwe kuwa barabara ya Mkoa na kujengwa kwa kiwango cha lami?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Mbugwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007, zinaeleza kwamba, hatua zifuatazo zitatekelezwa kabla barabara haijapandishwa hazi kutoka daraja moja kwenda daraja lingine. Kwanza kabisa, Wilaya ikijiridhisha kuwa barabara inakidhi vigezo vya kisheria vya kupandisha daraja, itapeleka ombi kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa. Bodi ikijiridhisha, itamwandikia Waziri mwenye dhamana kuomba aipandishe hadhi barabara husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Vijiji vya Magange, Nyikonga, Lulembela hadi Kashelo, alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, viko ndani ya Barabara iliyoahidiwa na Mheshimiwa Rais, kujengwa kwa kiwango cha lami. Kutoka Katoro – Kaseme – Magange – Nyikonga (km. 27) kwa upande wa Wilaya ya Geita na Lulembela – Kashelo – Butinzya – Bwenda hadi Ushirombo (km. 27) kwa upande wa Wilaya ya Bukombe na sehemu ya Luluasa – Kaduda hadi Ipalamasa ni Barabara ya Mkoa chini ya *TANROADS* Mkoa wa Kagera.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa Waziri amesema kwamba Wizara yake iko tayari kuridhia ujenzi na kupandisha daraja barabara hii ambayo nimemwuliza ya kutoka Ipalamaswa kwenda Masumbwe; na kwa kuwa Halmashauri tayari imeshafanya utaratibu wa kuipima na kuona kama barabara hii inazo sifa za kuwa Barabara ya TANROADS; je, Waziri atakuwa tayari kuidhinisha barabara hii kuweza kuwa ya Mkoa endapo *TANROADS* watakuwaji kuipandisha daraja? (*Makofi*)

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):
Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Augustino Masele, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, ninampongeza Mheshimiwa Masele, kwa juhudi zake nyingi anazozifanya katika kuhakikisha kwamba, barabara za jimbo lake zinapitika. Ninataka kumhakikishia kwamba, barabara aliyoitaja ambayo inatoka Lumasa –Kagunga – Nyikonga – Masumbwe itakapoletwa katika Wizara yetu kama itakidhi vigezo, tutaipandisha na kuwa Barabara ya Mkoa.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa swali namba 102 linafanana kabisa na changamoto zilizopo kwenye Jimbo la Nkasi Kusini hasa kwa Barabara ya Kitosi – Wampembe na Barabara ya Nkana – Kala; na kwa kuwa Bodi ya Barabara ya Mkoa tayari imekwishaandika barua Wizarani ili kuzipandisha daraja kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri kuzihudumia; je, Waziri anawaahidi nini Wananchi ambao tayari wameshaleta maombi kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa?

SPIKA: Swali ni jipya, kama unataka Waziri akuahidi, lete swali la msingi atakuahidi, lakini hivi hivi tu mbona inakuwa rahisi. Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wewe ni mtaalamu lakini usia hidi hapa, unaweza kueleza tu lakini kuahidi hapana.

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):
Mheshimiwa Spika, barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, ambazo anaomba zipandishwe hadhi, nimeeleza kwamba, barabara zitakuwa zinapandishwa hadhi kama zitakidhi matakwa ya Sheria Na. 13 ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba, katika barabara kwa mfano zilizopandishwa hadhi mwaka jana, ambazo zilikuwa zaidi ya kilomita 2,400 zilipandishwa hadhi lakini utekelezaji wake hazikuweza kutengenezwa vizuri kwa sababu fedha zinazotumika katika kutengeneza barabara hizi pia zinatokana na Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Barabara unahudumia pia barabara ambazo ziko ndani ya Halmashauri za Wilaya. Ningependa kutoa wito kwa Halmashauri za Wilaya, zile fedha zinazotolewa kwa ajili ya *Road Fund*, zitumike katika kazi za kutengeneza barabara, zisitumike fedha hizo kwa ajili ya kulipa posho, kwa sababu sheria inazungumza fedha za *Road Fund* ni lazima zitumike kwa ajili ya matumizi ya barabara peke yake.

Kwa hiyo, wito wangu ni huo kwa Halmashauri zote, zizingatie thamani ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya *Road Fund* ambapo katika bajeti ya mwaka huu ni shilingi bilioni 289. Nina uhakika zikitumika vizuri katika Barabara za Halmashauri, hapatakuwa na sababu ya kuomba kila mara barabara hizo kupandishwa daraja kutoka Halmashauri kwenda Barabara za Mkoa kwa sababu fedha zinazotumika ni hizo hizo za Mfuko wa Barabara.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashukuru sana kwa kuniona. Ningeomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Same Mashariki, Kata kumi zote ziko milimani na barabara zake ni nzito sana; na kwa kuwa huko huko milimani ndiko ambako tumejenga Kiwanda cha Tangawizi ambacho karibu kitaanza uzalishaji; je, Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa kuzipandisha daraja barabara ambazo ziko kwenye viwanda ili magari yaweze kufika kwa urahisi na kuchukua tangawizi ambayo itakuwa nyingi sana na tutaweza kupeleka hata nchi za nje?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kilango Malecela, kwa juhudi kubwa alizozifanya hadi akapata Kiwanda cha Tangawizi kule milimani kwa Wapare. Nina uhakika sasa Malecela atakuwa anakwenda vizuri kule atakapokuwa anatembelea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, Sheria ya Barabara (*Road Act. No 13* ya Mwaka 2007) ina viwango ambavyo vimewekwa na katika viwango vile, watakapojadili kwenye Halmashauri za Wilaya na kukubaliana kwamba zile barabara zinatakiwa kupandishwa hadhi, barabara zile zilizopendekezwa zinapelekwa kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa na Bodi ya Barabara ya Mkoa wanatuandikia sisi Wizarani na Wizarani huwa tuna *Committee* Maalum ya Wataalamu wa kuzi-*upgrade*. Kama barabara hizi zitakidhi hadhi ya kuzipandisha ziweze kuwa za Mkoa, Wizarani yangu haitakuwa na matatizo kuzipandisha hadhi.

Na. 103

JWTZ Kufanya Kazi za Jeshi la Polisi

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Je, ni wakati na mazingira gani Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) linawajibika kufanya kazi za ndani badala ya Jeshi la Polisi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna wakati au mazingira yatakayolifanya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kufanya kazi za ndani badala ya Jeshi la Polisi, bali

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaweza kusaidia pale Jeshi la Polisi linapoemewa na kuombwa kufanya hivyo. Msaada wa JWTZ kwa shughuli za ndani si katika masuala ya usalama wa ndani tu, bali Jeshi linaweza kuombwa kusaidia katika shughuli nyingine, inapobidi; kama vile shughuli za uokoaji, ujenzi hususan nyakati za dharura na majanga mbalimbli.

Mheshimiwa Spika, Majeshi ya Ulinzi yanatumika pale panapotokea uvunjifu wa amani au dalili za uvunjifu wa amani na inapodhihirika na Mamlaka za Kiraia kuwa Polisi wameelewema. Majeshi ya Ulinzi yanapotoa msaada huo, hayachukui nafasi ya Mamlaka za Kiraia (*do not replace the civil power*), isipokuwa yanasaidia kudumisha sheria na amani (*enforcement of law and order*).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya Mwaka 2002 (*Cap. 192*), Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), linaruhusiwa kutoa msaada wa Mamlaka za Kiraia (*Civil Authorities*), pale ambapo kuna machafuko (*Riot*) au ghasia (*Disturbance*) au uasi (*insurgence*), pindi linapoombwa na Mamlaka ya Kiraia kufanya hivyo. Aidha, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaweza kufanya jukumu la ulinzi wa vituo muhimu nchini endapo uwezo wa Polisi ni mdogo. Utaratibu unaotumiwa na JWTZ katika kutoa misaada kama hiyo, umebainishwa kwenye Kanuni ya 15 ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Juzuu ya Kwanza (Utawala) (*The Defence Forces Regulations, Volume I (Administrative)*), inayozungumzia majukumu ya Majeshi ya Ulinzi katika kusaidia Mamlaka za Kiraia.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa uniruhusu nijibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi wa Novemba, 2010, pale Bandari ya Mkoani Pemba, walikuwepo Wanajeshi wetu wengi sana, walikuwa wakiwaongoza Wananchi kuingia kwenye meli, lakini nilishuhudia baadhi ya Wanajeshi wakiwapiga wasafiri wale na kuwapaka matope. Nilikwenda Unguja pale nikaona kuna Jeshi, nikapata wasiwasi, nikaenda Dar es Salaam nikakuta kumetulia kabisa:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba vitendo kama hivi vinaidhalilisha Zanzibar?

(ii) Je, haoni kitendo cha Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania kuwapiga Raia wa Tanzania ni kukiuka Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu na kuivunja hadhi nchi yetu ya Tanzania?

SPIKA: Swali ni moja tu, ninaomba ujibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, linaweza kuombwa kutoa msaada pale ambapo Mamlaka za Kiraia zinaona ni muhimu kufanya hivyo. Hakuna Mwanajeshi anayeruhusiwa kwa wakati wowote ule, kufanya au kutoa adhabu

kwa raia katika eneo hilo. Ninachosema ni kwamba, yapo baadhi ya matukio yanayotokea ya baadhi ya Wanajeshi kukiuka maadili na kufanya vitendo viovu inapothibitika kwamba, mambo hayo yamefanyika, taarifa zikitolewa kwa Makao Makuu ya Jeshi, hatua za kinidhamu mara zote zimekuwa zikichukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, si kwamba Serikali au Jeshi linawatuma Wanajeshi kufanya vitendo viovu, lengo na madhumuni ya Jeshi letu ni kutoa msaada kwa Mamlaka za Kiraia katika nyanja mbalimbali na sote ni mashahidi Wanajeshi wamekuwa mstari wa mbele kusaidia raia katika majanga, maafa na kadhalika.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba, endapo Mheshimiwa Mbunge ana ushahidi wa matatizo kama hayo, anatakiwa atoe taarifa kwa Mamlaka husika na ninamhakikishia kwamba, hatua za kinidhamu zitachukuliwa.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa nini kila unapoingia Uchaguzi Mkuu; Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatumiwa Visiwani lakini halitumiwi Bara? Wakati huo huo niulize; je, Jeshi la Polisi huwa limeshindwa kusimamia chaguzi hizo? Na kwa nini Bara hawafanyi hivyo Jeshi la Wananchi wa Tanzania kusimamia uchaguzi? (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, linaweza kuombwa na Mamlaka za Kiraia kutoa msaada. Mara nyingine Jeshi la Wananchi linaombwa kutoa msaada wakati wa Uchaguzi na misaada hii inakuwa ni ya aina mbalimbali ikiwemo kulinda vituo vikuu, mfano, bandari, *airport* na kadhalika.

Suala hili linafanyika kwa pande zote mbili, kutegemeana na uwezo wa Polisi katika maeneo husika. Imedhihirika kwamba, mara nyingi na hususan kabla ya mwafaka, kule Zanzibar kulikuwa kuna matukio mengi sana katika maeneo mengi kiasi cha kwamba Polisi walikuwa wanazidiwa nguvu na ndiyo sababu Mamlaka za Kiraia zikawa zinaomba Jeshi la Wananchi liongeze nguvu katika maeneo kadhaa na hii si kwa Zanzibar peke yake, yapo baadhi ya maeneo kwa Tanzania Bara, ambayo yaliomba msaada huo na mara zote Jeshi limekuwa likitoa.

Na. 104

Ugonjwa wa Kuanguka na Kupiga Kelele

MHE. KIDAWA HAMID SALEH aliuliza:-

Katika baadhi ya shule wanafunzi wa kike wamekuwa wakianguka na kupiga kelele:-

- (a) Je, huu ni ugonjwa gani na husababishwa na nini?

(b) Ni kwa nini ugonjwa huo huwapata zaidi watoto wa kike?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Tatizo la wanafunzi kuanguka na kupiga kelele kama kundi (*Mass Hysteria*) ni tukio la kisaikolojia, ambalo huwaathiri zaidi watoto wa umri wa shule hasa wa kike, kutokana na mazingira yanayowaletea mshtuko, mfidhaiko au wasiwasi/woga uliokithiri. Waathirika hupatawa na dalili mbalimbali zikiwemo kizunguzungu, kuzirai, kuumwa kichwa, tatizo la kupumua, kutetemeka, kifafa bandia, kuwashwa, kuweweseka, kuumwa tumbo, kutapika, kichefuchefu na kucheka mfululizo au kulia; dalili ambazo huenea haraka pale mwanafunzi anapowaona wenzake walioathirika. Hali hii inaweza kuathiri uwezo wa wanafunzi kwenye masomo yao.

(b) *Mass hysteria* huwapata zaidi wanafunzi wa kike kutokana na kuongezeka kwa msongo wa mawazo yatokanayo na masuala yanayowakabili watoto wa kike shuleni bila suluhisho. Ili kuondoa tatizo hili, hapana budi walimu na wazazi kushirikiana na Wataalam wa Afya na Elimu katika kufuatilia malezi na makuzi ya vijana, hususan kukua kimwili, kiasili, kisaikolojia na kijamii.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa tatizo hili linatokea zaidi katika kipindi cha mitihani. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni kwa nini inatokea katika kipindi cha mitihani?

(ii) Kuna imani potofu zinazojengeka kwa wazazi na wazee wa vijiji kuwa ugonjwa huu ni wa kimazingara au mazingaombwe na wakati mwingine wanachinja mbuzi kutoa kafara na mambo mengine. Je, Mheshimiwa Waziri atawaeleza nini Wananchi au atatoa elimu gani kuhusu tatizo hili? Ahsante.

SPIKA: Ahsante, tatizo ukishamwuliza Waziri ambaye ni Daktari hapa, *lecture* mtakayoipata leo itakuwa ya mwaka. Ninaomba useme kwa kifupi tafadhali. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, wanafunzi wengi huwa wanapata matatizo wakati wa mitihani. Wakati wa mitihani ndiyo wakati wanafunzi wanapata msongo wa akili mkubwa sana na unakuta kwamba, wakati mwingine wanafunzi hawa wanakuwa hawana mtu wa kuwashauri, hawana mtu wa kuwasikiliza na hawana uhakika kama kweli wataweza kufanya mtihani wakafaulu, wanaogopa wazazi wao watafanya nini nyumbani wakifeli na wanaogopa pia maisha yetu ya baadaye yanakuwaje kwa sababu ndicho kipindi kinachoamua kwamba, maisha ya

mwanafunzi yanakuwaje baada ya ule mtihani. Kwa hiyo, ule msongo ndiyo unafanya wanafunzi wanakuwa katika *extra stress*, tunasema msongo wa kupita kiasi unajitokeza. Aidha, kwa kupata kifafa bandia au kwa kucheka au kwa kulia sana. Hiyo ni dalili kwamba, wanafunzi wana msongo mwingi.

Mheshimiwa Spika, ninajibu swali la pili sasa; mara nyingi inapotokea hivyo, kwa sababu ni jambo ambalo limejitokeza hivi sasa, zamani tulikuwa na shule chache, tulikuwa na walimu wa kutosha, wanafunzi walikuwa wanafundishwa vizuri na walikuwa wanapata mahitaji yote yanayohitajika; ndugu zangu ninaomba niseme kwamba, wanafunzi sasa wanapata haya matatizo, wazazi hawakuzoea kuyaona, jamii haikuzoea kuona haya matatizo, yalikuwa yanatokea mara chache sana, shule zimekuwa nyingi, kwa hiyo yanaongezeka, kwa sababu hakuna maelekezo ndiyo sababu Wananchi wanaambatanisha na imani za kichawi. Hapa kwetu Tanzania na Afrika, ugonjwa wowote ule ambao hauna maelekezo na maelezo na ni mpya, mara nyingi tunatafuta sababu tunasema kuna mkono wa mtu na kutokana na hilo ndiyo maana Wananchi wanasema kwamba shule imerogwa.

Ninaomba nitoe ushauri kwamba, wanafunzi wanapocheka au kulia na kuanguka ni maradhi ambayo yanaweza yakatibiwa na Daktari yeyote siyo uchawi, wala hakuna jirani anayeroga shule. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba, wazazi wajaribu kuwatimizia watoto wao mahitaji yao. Walimu shuleni nao wawajibike kutoa huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi, kila shule iwe na mlezi wa wanafunzi hasa wanafunzi wa kike wa kuwasikiliza na huyo mtu awe tayari kuwasikiliza wanafunzi. Mara nyingi wanafunzi wanaweza wakamtaja ni nani ambaye wanamwamini, kwa hiyo, hakuna ushirikina ila ni matatizo ya ugonjwa wa akili ambao siyo mkubwa.

SPIKA: Ili semina hii tusiiharibu, tunaacha maswali ya nyongeza mengine.

Na. 105

Malipo ya Askari Mgambo Katika Jimbo la Mwibara

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA aliuliza:-

Kumekuwapo na malalamiko mengi kutoka kwa Wananchi wa Jimbo la Mwibara kuwa wamekuwa wakitozwa fedha kwenye Vituo vya Polisi kama malipo ya posho ya Askari Mgambo kwa ajili ya kukamata watuhumiwa wao; Vituo vya Polisi vya Kibara na Kisorya vina Askari wa Mgambo ambao wamekuwa wakitumia na Askari Polisi kufanya kazi ya ukamataji wa watuhumiwa ilihali hawawezi kufanya kazi hiyo bure:-

- (a) Je, nani anawalipa Askari Mgambo hao?
- (b) Kama wanalipwa na Serikali; je, utaratibu wa kuwalipa umeanza lini; na ni kiasi gani cha fedha wamelipwa kama posho tangu mwaka 2005 kwa nchi nzima?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Jeshi la Polisi limekuwa likiwatumia Askari Mgambo kusaikia katika kazi za Polisi hasa katika maeneo ambayo kuna uchache wa Askari Polisi au yaliyopo mbali na huduma za Polisi. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Mgambo (*The People Militia Act, Cap 111 (R.E. 2002)*). Kifungu cha 4(1) kinasema kwamba, Askari wa Mgambo anapofanya kazi za Polisi anakuwa na mamlaka ya kukamata na kupekua, pamoja na masharti mengine anayopewa Askari Polisi mwenye cheo cha *Constable*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kazi ya mgambo ni ya kujitolea, kwa hiyo, haina malipo rasmi. Jeshi la Polisi halina fungu la kuwalipa Askari Mgambo na hakuna kituo chochote kinachotoza fedha toka kwa Wananchi kwa ajili ya posho za Askari Mgambo. Iwapo wapo askari wanaofanya hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, anipatie majina ya wahusika ili niwachukulie hatua zinazostahiki.

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Askari wa Mgambo wanawatumia vituoni kutokana na uhaba wa askari; na kwa kuwa amekiri kwamba Askari wa Mgambo hawa wanapokuwa wanafanya kazi hizi ni kwa mujibu wa tafsiri ya Afisa wa Polisi katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na ile ya Mgambo; na kwa kuwa wanakuwa wamejivua gamba la mgambo na kuvaa gamba la upolisi; kwa nini isiwe wakati muafaka mgambo walipe kwa sababu wanakuwa wameshakuwa ni polisi kwa mjibu wa tafsiri?

(ii) Kwa kuwa pia Naibu Waziri amekiri kwamba kuna uhaba wa askari na kwenye vituo vya Kibara, Kisoja na Blamba askari mgambo hawa wapo na wamekuwa wakikamata; na kwa kuwa wao ni binadamu toka asubuhi mpaka jioni wanashinda vituoni na wanakamata watu ambao wengine wanakuwa na nguvu za kuwadhuru; je, Naibu Waziri haoni kwamba kuna kila dalili na mazingira kwamba Wananchi wa Mwibara ni kweli wanasumbuliwa na kutozwa fedha na kwamba tunahitaji askari wa kutosha vituoni?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, suala la kusema kwamba, askari mgambo kwa kuwa wanasaidia katika maeneo husika katika nchi yetu ya Tanzania, kwa tafsiri ya haraka haraka inawatoa katika umgambo wao kwa maana ya kusema kwamba, kwa lugha aliyoitumia kwamba, wanajivua gamba wanakuwa kama polisi siyo sahihi na siyo kweli. Polisi atabaki ni polisi kwa taratibu na sheria tulizonazo katika nchi yetu na mgambo watakuwa ni mgambo kwa maana ya kusema kwamba, wanasaidia katika maeneo yenye upungufu wa askari.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, ipo sheria ambayo tunayo katika nchi yetu, inahusu *auxiliary police* ambayo iko chini ya Halmashauri na Halmashauri zina haki kabisa kwa mujibu wa sheria, kuweza kuwa na askari ambao wako chini yao na kuweza kutazama maeneo yao; lakini Halmashauri zimekuwa hazifanyi hivyo na huko nisingependa kwenda, isipokuwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunawatumia hawa kwa sababu ya upungufu wa askari, lakini ni katika maeneo ambayo yanaeleweka kwa mujibu wa sheria kama ilivyotungwa na Bunge hili. Sasa kuhusu eneo la Mwibara askari mgambo wanatoza Wananchi fedha; hili nimelijibu katika jibu langu la msingi na nimesema kwamba, iwapo vitendo kama hivi vinatokea kinyume na sheria ni kwamba, tupate taarifa na tupate majina ya wale wanaohusika na hutua stahiki kwa sababu ni kinyume cha sheria.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ni kweli baadhi ya wanamgambo wanawanyanasa Wananchi kwa njia ya kuwadai fedha kama ujira kwa kazi wanayofanya kwa msingi kwamba wao wanajitolea. Je, ni kigezo gani kinatumiwa na Wizara katika kuteua baadhi ya mgambo kuwasaidia askari polisi katika kazi zao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kweli yamekuwepo malalamiko ambayo tumeyasikia kuhusu vitendo vya askari mgambo, lakini askari mgambo kwa sheria tuliyonayo, wako chini ya Uongozi wa Serikali za Vijiji na Serikali za Kata wala siyo Serikali Kuu kama Jeshi la Polisi. Sisi wanatusaidia kwa askari jamii ambao tulikuwa nao na ulinzi shirikishi ambao tunaupa nguvu, lakini malalamiko haya yamekuwepo na tumekuwa tunayafanyia kazi. Mheshimiwa Selasini anaweza akawa shuhuda katika hili, tunakiri kwamba, matendo yamekuwepo lakini kumekuwepo na upungufu na tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba, haki za Watanzania zinabaki palepale na zinaheshimiwa na mgambo watafanya kazi kwa mujibu wa Sheria, lakini si kwa mujibu wa faida zao binafsi.

Ninatoa wito kwamba, katika Tanzania yetu hii, pale ambapo itaonekana kwamba, askari mgambo wanakwenda kinyume na sheria na wanawafanyia Wananchi wetu mambo ambayo ni kinyume na taratibu na sheria, tupewe taarifa na hatua za haraka zitachukuliwa.

Na. 106

Power Tillers Zisizo na Viwango

MHE. MKIWA A. KIMWANGA alijibu:-

Ingawa wakulima wengi wameitikia wito wa Kilimo Kwanza katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo nchini; lakini limejitokeza tatizo la baadhi ya Wafanyabiashara wamewauzia Wakulima *power tillers* ambazo hazikidhi viwango:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwadhibiti Wafanyabiashara hao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 19 ya 1981, ilianzisha Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (*CAMARTEC*) na kukipa dhamana ya kusimamia ubora wa zana za kilimo kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*). Kazi za *CAMARTEC* ni pamoja na kufanya majaribio na kupima ubora wa zana za kilimo zinazoingizwa na kutengenezwa nchini, kabla hazijaruhusiwa kuuzwa kwa wakulima. Wizara yangu inawashauri wakulima ambao wanahisi au wameuziwa trekta ndogo (*Power Tillers*) au zana nyingine za kilimo zisizokidhi viwango, kutoa taarifa kwenye Ofisi za Kilimo za Wilaya na kuwasiliana na Mkurugenzi Mkuu, *CAMARTEC*, S.L.P. 674 Arusha, Simu Na. 027 12549214 au barua pepe *camartec@yahoo.com* ili hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi ya wauzaji kama ilivyofanyika katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwishatayarisha viwango vya kiufundi (*Technical Specifications*) na kuvisambaza katika Halmashauri zote nchini ili kuzisaidia kununua zana zinazofaa kwa wakulima katika maeneo yao. Aidha, kanuni moja ya kupata zabuni ya kusambaza *Power Tillers* ni kuwa na uhakika wa upatikanaji wa vipuri na huduma baada ya mauzo (*After Sale Services*). Wizara pia imetayarisha mwongozo wa matumizi na matunzo ya *Power Tillers* na matrekta na kuusambaza kwenye Halmashauri zote ili kuwawezesha wakulima kutumia matrekta hayo kwa ufanisi na kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wanapenda kilimo, Wizara yangu itaandaa nakala za kutosha za miongozo niliyotaja ya viwango vya kiufundi na matumizi bora ya *Power Tillers* na matrekta madogo na makubwa na kuwapatia ili iwasaidie wao wenyewe na kutoa ushauri kwa watu wengine katika kuchagua aina ya trekta kufuatana na mahitaji yao.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

(i) Kwa kuwa zana za kilimo ni muhimu sana hapa nchini; Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti bei hasa upande wa *power tillers* ambazo huuzwa kwa bei ghali sana na wakulima wadogo kushindwa kukidhi bei hizo?

(ii) Kwa kuwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi amesema upimwaji wa ubora wa zana za kilimo hufanywa na *CAMARTEC* na *TBS* na inatakiwa kabla hazijaingia katika soko ziwe zimeshafanyiwa majaribio; ikiwa Wananchi watajitokeza ambao wameuziwa zana zisizokidhi haja na Serikali ikahakiki; Serikali itakubaliana nami wapimaji wa ubora wa *CAMARTEC* na *TBS* wachukuliwe hatua kwa kuwasababishia Wananchi hasara hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kuhusu kidhibiti bei, sasa hivi ni soko huria; tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba, zana zote zinazoletwa nchini zinadhibitiwa ubora. Sasa wanaoziingiza wana haki ya kupanga bei na wewe unakwenda kununua ukiridhika kwamba, bei hiyo ni sahihi utanunua, lakini kwa kuwa ni wengi unaweza kwenda kuchagua nani anakuuzia chombo na kwa bei gani. Kuhusu hawa ambao wanaleta zana ambazo hazikidhi, mimi nimesema kwamba, kama umeona hazikidhi, wasiliana na vyombo hivi ambavyo vinadhibiti ubora. Kama wale watu wameingiza zana hizi na hazikupitia kule, basi ikithibitika kwamba wale walihusika kuzipitisha zana hizi, tuna haki kabisa ya kuwafuatilia kwa nini waliziruhusu ziingie nchini.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa inawezekana Mamlaka zilizopewa ruhusa kuruhusu zana mbalimbali za kilimo ziweze kuingia nchini pengine zikaruhusu zana feki; na kwa kuwa hivi karibu katika Wilaya ya Kasulu zipo taarifa kwamba kuna *power tillers* ambazo wanauziwa wakulima ambazo ni sawasawa na zile ambazo zimekuwa zikiripotiwa kuwa hazina uwezo wa kuwasaidia wakulima kulingana na ardhi iliyopo Wilayani Kasulu:-

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa kauli gani juu ya *power tillers* ambazo zimeingizwa majuzi na ambazo zinaonekana kwamba ni sawasawa na *power tillers* zilizokuwepo siku za nyuma ambazo hazikuweza kukidhi viwango vya kilimo ndani ya Wilaya ya Kasulu na kuwachukulia hatua watu wote ambao wameruhusu *power tillers* hizo kuweza kuendelea kuingizwa hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, si rahisi kupiga pasi roho za Wafanyabiashara, haiwezekani. Kwa hiyo, kama watu wameingiza zana feki, ninataka nimhakikishie kwamba, tutakachokifanya ni kukagua. Tutawaagiza vyombo vinavyohusika vifanye ukaguzi wa ubora halafu wale wote watakaothibitika kuingiza zana hizi ambazo ni feki, tutawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Na. 107

Hitaji la kuwa lazima leseni itolewe na Bodi

MHE. SUSAN L. KIWANGA aliuliza:-

Sheria zinazotoa hitaji la kuwa na leseni inayotolewa na Bodi kama ilivyo kwa Sheria ya Sukari ya 2001 linawaathiri sana Wafanyabiashara na Wakulima; kwani linawasababisha washindwe kufanya makubaliano na viwanda vya sukari ili kusaga miwa, na wao kulipia gharama hizo halafu kuwa wamiliki halali wa sukari yao, utaratibu kama huo unatumiwa na Uganda kwa Kiwanda cha Sukari cha Kagera:-

(a) Je, kwa nini Serikali isibadilishe sheria hizo kandamizi ili Wakulima waweze kuzalisha sukari yao?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa kero waliyonayo Wakulima wa miwa kwa kushindwa kupanga bei ya mazao yao?

(c) Je, kwa mtindo huo wa mnunuzi kujipangia bei; Kauli ya Kilimo Kwanza inamnufaisha mkulima au mfanyabiashara?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Sukari ya Mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2009, inatambua usawa baina ya wazalishaji wa sukari (wenye viwanda), Wakulima wa Miwa, walaji na waingizaji wa sukari nchini. Aidha, usawa kati ya wazalishaji wa sukari na wakulima wa miwa umeainishwa katika sheria hiyo kwa kuweko bayana uwepo wa mkataba maalum wa uuzaji wa miwa kutoka kwa mkulima kwenda kwa mwenye kiwanda.

Pamoja na mambo mengine yanayohitajika katika mkataba huo, upangaji wa bei ya uuzaji wa miwa unahusisha pande zote mbili (vyama vya wakulima na mwenye kiwanda). Mikataba huaandaliwa kila mwaka kabla ya msimu wa uzalishaji sukari kuanza au kipindi kinachokubalika na wadau katika eneo husika. Wakulima wanashauriwa kushiriki kikamilifu kabla ya kufikia makubaliano. Aidha, Sheria ya Sukari haimzui mkulima wa miwa au Wakulima kwa umoja wao, kuanzisha viwanda vyao ya sukari pale wanapokuwa wamefuata taratibu zilizowekwa chini ya sheria hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Sukari ya Mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa 2009), kifungu cha 4(1) na Kanuni namba 35 (1) inabainisha kuwa, Wakulima wa Miwa hujumuishwa kwenye mchakato mzima wa upangaji wa bei kupitia kwenye mikataba wanayoiweka kwa pamoja na wazalishaji wa sukari kabla ya msimu wa uzalishaji sukari kuanza.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia Wakulima wa Miwa, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu ya kilimo cha mkataba ili waweze kuelewa mianya inayoweza kuwanufaisha au kuwaletea hasara. Aidha, Wizara itasaidia kuwakutanisha wakulima wenye viwanda vya sukari kwa lengo la kupata mwafaka wa bei.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza pamoja na majibu ya Waziri na katika jibu lake ameonesha kwamba; kumbe wakulima wana nafasi ya kuweza kuanzisha viwanda ili kuzalisha sukari.

(i) Kwa kuwa katika maeneo mengi Wakulima Wadogo wananyanyasika sana na wenye viwanda kwa miwa yao kuungua moto na wenye viwanda hao kuikataa

miwa hiyo ingawa inafaa kuzalisha sukari. Je, Serikali sasa iko tayari kuwasaidia Wakulima hao kushirikiana na *SIDO* kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili kuwaondolea hasara wakulima hao kusaga sukari yao na kuiuza?

(ii) Je, Serikali itasaidia kudhibiti bei ya sukari?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa na ninaungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ipo tayari kushirikiana na Wananchi wale na kushirikiana na *SIDO* ili kuangalia namna ya kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika miwa ya Wakulima hawa.

Na. 108

Kodi Kwa Wafanyabiashara Toka Zanzibar

MHE. MBAROUK SALIM ALI aliuliza:-

Mamlaka ya Mapato Tanzania ni Taasisi ya Muungano na hutumia Sheria moja:-

Je, ni kwa nini Wafanyabiashara wanaonunua bidhaa Tanzania Zanzibar wanatozwa kodi ya ziada wanapoleta bidhaa zao Tanzania Bara?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Jimbo la Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato katika kutekeleza jukumu lake la kukusanya na kuzuia uvujaji wa mapato ya Serikali, imepewa nguvu ya kisheria na inawajibika kufuatilia kodi wakati wowote na mahali popote pale. Hali kadhalika, pale inapothibitika kuwa kodi haikukusanywa kikamilifu kwa sababu yoyote ile, Mamlaka huchukua hatua za kisheria kukusanya tofauti kati ya kodi sahihi na ile iliyokusanywa awali. Hii siyo kutozwa kodi ya ziada.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufafanua kuwa, utaratibu huu si kwa mizigo inayoingia kupitia Tanzania Zanzibar na kuvushwa kuja Tanzania Bara pekee, bali ni kwa mizigo yote inayoingia kupitia kituo chochote cha forodha nchini. Kinachosababisha tofauti hii ya ukusanyaji mara nyingi ni kwa waingizaji wa mizigo wenyewe, kutotoa taarifa sahihi na kufanikiwa kuwapiga chenga Maafisa wa Forodha kwenye hatua za awali za uingizaji mzigo, ndiyo maana Mamlaka ikaweka katika muundo wake vitengo vya *Free Anti-Smuggling Team (FAST)*, *Post Clearance Audit* na Idara ya Upelelezi wa Kodi kama ngome ya pili ya ulinzi (*Second Line of Defence*). Aidha, Mamlaka imeanzisha utaratibu wa ukadiriaji unaofanywa kwa kutumia mtandao badala ya kadhia zinazoletwa na mletaji mzigo.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi zake za kupunguza kujirudiarudia kwa hali hii, Mamlaka ya Mapato imeanzisha mfumo wa kompyuta ambapo kadhia za uingizaji mizigo kupitia vituo vyote nchini, inashughulikiwa kupitia kituo kimoja (*Dar es Salaam Customs Service Centre*). Mfumo huu ulianza karibuni mwaka mmoja uliopita, kwa upande wa Bara umeleta uwiano mkubwa wa uthamini wa bidhaa. Mamlaka imo katika mchakato wa kuiunganisha Forodha Zanzibar katika mfumo huu wa lengo la kukomesha kabisa uthaminishaji wa bidhaa zaidi ya mara moja itakapofika mwisho wa mwezi wa Aprili, 2011.

MHE. SALIM MBAROUK ALI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningelipenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Katika jibu la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, pale inapothibitika kuwa kodi haikukusanywa kikamilifu, mamlaka inayohusika inachukua hatua za kisheria kuhakikisha kwamba inakusanya tofauti ya kodi hii. Je, hii ni kuthibitisha au Naibu Waziri anaweza akathibitisha mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba Kituo cha Ukusanyaji Mapato cha Zanzibar hakikusanyi mapato kikamilifu? Na kama hakikusanyi mapato kikamilifu, je, ni kwa sababu gani mizigo au bidhaa ambazo zinabakia pale Zanzibar hazitozwi au hazifuatiliwi zikatozwa tena kodi ya ziada, lakini mizigo ambayo inakuja Tanzania Bara inakuwa ndiyo mizigo ambayo inatozwa kodi mara mbili?

(ii) Ahadi na Vikao vya *TRA* imekuwa ni nyimbo ambayo tumeshaizoea na tuna wasiwasi kwamba bado tunaendelea kupewa ahadi kuhusiana na tatizo hili. Hii ni kero ya muda mrefu na Wafanyabiashara pamoja na Wazanzibari wananyanyasika sana na tatizo hili. Je, Naibu Waziri anaweza katoa kauli ya Serikali, ikiwemo tarehe na siku mahususi ambayo tatizo hili litamalizika? (*Makofi*)

SPIKA: Haya, tuendele. Hiyo tarehe na siku mahususi huwezi kupata kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, kero hii ambayo inaikabili Zanzibar, Serikali imedhamiria kuwa inaweza ikafikia mwisho au itakuwa imefikia mwisho baada ya kuweka utaratibu ambao ni bora zaidi wa kutathmini bidhaa zinazopitia Zanzibar na zile zinazopitia Tanzania Bara. Nimesema kabisa kwamba, ifikapo mwezi wa Aprili, mwaka huu, kero hiyo itakuwa imekwisha.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, muda hautoshi; angalieni saa hata swali la kumi sijafika.

MHE. AINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kabla sijauliza swali langu, ninaomba nipate mwongozo wako katika swali langu hhili. Kwa nini maswali mawili ambayo yamefanana...

SPIKA: Ahaa, uliza swali Mheshimiwa ama usahihishe swali. Tukiingia kwenye mwongozo tunakula muda wa maswali. Uliza swali, kama unataka kuliondoa, liondoe.

MHE. AINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ninaomba swali langu namba 109 lijibiwe.

Na. 109

Utaratibu wa Kulipia Ushuru wa Bandari

MHE. AINA MOHAMED MWIDAU aliuliza:-

Mzigo wowote unapoingia Tanzania Zanzibar kwa ndege au kwa meli hulipiwa ushuru *TRA* na unapovushwa kwenda Tanzania Bara hutakiwa tena kulipiwa ushuru:-

- (a) Je, kwa nini ushuru ulipwe mara mbili?
- (b) Je, Serikali itachukua hatua gani dhidi ya tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyoona yeye mwenyewe mwuliza swali, kwa kweli hata mimi imenikanganya kidogo, kwa sababu swali ambalo nimelijibu hapa mwanzoni linafanana na swali hili. Swali lililotangulia linaulizia kuhusu kutozwa kodi ya ziada; na swali hili linauliza kutozwa ushuru mara mbili. Kwa hiyo, jibu ni lile lile ambalo nimelitoa pale mwanzo.

Jibu la Msingi kwa hili ni kama jibu ambalo nimelitoa pale mwanzo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba nilipitie kwa haraka haraka kwa sababu maswali haya mawili yanafanana na yameulizwa na watu wawili tofauti na wote wanatoka Zanzibar.

SPIKA: Jibu swali la mtu, ameuliza!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushuru wa forodha unalipwa mara moja tu aidha, Zanzibar au Tanzania Bara na siyo mara mbili.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufafanua tena kuwa, utaratibu huu si kwa mizigo iliyoingia kupitia Tanzania Zanzibar na kuvushwa kuingia Tanzania Bara, bali ni kwa mizigo yote inayoingia kupitia Kituo chochote cha Forodha nchini. Kinachosababisha tofauti hii ya ukusanyaji mara nyingi ni kwa waingizaji wa mizigo wenyewe kutotoa taarifa sahihi na kufanikiwa kuwapiga chenga Maafisa wa Forodha kwenye hatua za awali za uingizaji mzigo. Hii hutokea si kwa sababu ya uzembe wa maafisa, bali kutokana na mazingira ya utendaji kazi katika hatua hizo za awali, kwani siku zote kumekuwa na msukumo mkubwa kutoka kwa wadau wote wa kuharakisha utoaji mizigo mara tu inapowasili, hali ambayo mara nyingine hupelekea kutokukagua kadhia kwa asilimia mia moja. Kwa kulitambua hilo, ndiyo maana Mamlaka ikaweka katika muundo wake, Vitengo vya *Free Anti-Smuggling Team, Post Clearance Audit* na Idara ya Upelelezi wa Kodi kama ngome ya pili ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRA* katika juhudi zake za kupunguza kujirudia rudia kwa hali hii, Mamlaka ya Mapato imeanzisha mfumo wa kompyuta ambapo kadhia za uingizaji mizigo kupitia vituo vyote nchini, zinashughulikiwa kupitia kituo kimoja cha Dar es Salaam ambacho kinaitwa *Dar es Salaam Customs Service Centre*.

MHE. AINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo sjaridhika nayo kwa kiasi fulani, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala hili la utozwaji wa ushuru mara mbili linawachanganya sana Watanzania walio wengi, wanalipa japokuwa hawaelewi kwa nini wanalipa mara mbili. Je, Serikali haioni kuwa huu sasa ni wakati muafaka wa kutoa elimu ya kutosha kwa Watanzania wote ili waweze kuelewa nini haki zao za msingi na vile vile waweze kujitetea pale ambapo wanatakiwa kulipa ushuru mara mbili?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninakubaliana naye kwamba, elimu bado haijatosha hasa kwa wenzetu ambao wanaona kwamba, hizi bidhaa zinatozwa ushuru mara mbili. Nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba, bidhaa kusema kweli hazitozwi mara mbili. Kwa hiyo, elimu hapa inahitajika. Ninakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutafanya hivyo kwa kutoa elimu, watu waweze kuelewa kwa undani matatizo haya ya kodi mara mbili.

Na. 110

Uhaba wa Maji – Nanyumbu

MHE. JUMA A. NJWAYO (K.N.Y. MHE. DUNSTAN D. MKAPA) aliuliza:-

Kata za Maratani na Mnanje Wilayani Nanyumbu zina uhaba mkubwa wa maji safi na salama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka na wa kudumu wa kutatua kero hiyo ya maji katika Kata hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Maratani ina Vijiji vinne vya Maratani, Lipupu, Malema na Mchangani. Kwa Vijiji vitatu vya Maratani, Malema na Mchangani, kila kimoja kina kisima kirefu kimoja chenye pampu ya mkono. Visima vyote vinafanya kazi na watu wanapata huduma ya maji. Hata hivyo, visima hivyo havitoshelezi mahitaji kutokana na wingi wa watu. Kijiji cha Lipupu hakina huduma rasmi ya maji. Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, inashauriwa kutenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji katika Vijiji vya Kata ya Maratani.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mnanje ina Vijiji vinne vya Mnanje, Holola, Mikuva na Ngupe. Kijiji cha Mnanje kina kisima kirefu kimoja na kifupi kimoja. Vijiji vingine vina kisima kimoja kwa kila kijiji. Visima vyote vina pampu ya mkono na vinafanya kazi na kutoa huduma ya maji. Kwa kuwa visima hivyo havitoshelezi mahitaji, Kijiji cha Holola ni moja kati ya Vijiji kumi vilivyopewa kipaumbele na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu katika utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imemwajiri Mtaalam Mshauri, *Don Consult Ltd*, tarehe 20 Mei, 2009 ambaye amekamilisha utafiti wa vyanzo vya maji. Pia tarehe 25 Februari, 2010 Halmashauri hiyo ilimwajiri Mkandarasi, *Mwasi Drilling Co. Ltd*, kwa ajili ya kazi ya uchimbaji wa visima na kazi hiyo imekamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha kazi ya uchimbaji wa visima, Mtaalamu Mshauri anaendelea na usanifu wa Miradi na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa Miradi hiyo katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha huduma ya maji katika Vijiji vya Kata za Maratani na Mnanje, Serikali inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, kuzipa kipaumbele Kata hizo na kuweka vijiji vyake katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itakayoanza kutekelezwa mwezi Julai, 2012.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi anaeleza wazi kwamba, tatizo la maji kwenye maeneo tajwa ni kwa sababu maji yanayopatikana hayatoshelezi mahitaji; na ni ukweli ulio wazi kwamba karibu maeneo mengi nchini suala hili la maji limekuwa ni kero; hivi Serikali imejipangaje kumaliza tatizo hili katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne?

(ii) Kwa kuwa matatizo ya maji kwa Kata zilizotajwa za Wilaya ya Nanyumbu yanafanana kabisa na matatizo ya maji yaliyoko katika Wilaya ya Tandahimba na Wilaya ya Newala chini ya Mradi wa Makonde; na kwa sababu ni dhahiri

kwamba Serikali au Wizara ya Maji imekuwa ikichangia kwa namna moja au nyingine kwa sababu imekuwa haiwalipi wakandarasi waliokuwa wamepewa dhima ya kurekebisha matatizo kwenye Mradi kama ule wa Makonde; kwa mfano, *EFAM* ambayo ime-*supply* vifaa karibu miaka miwili sasa hajalipwa: Serikali haioni kwamba kutowalipa kunachangia kutomaliza matatizo kwenye Miradi hii ya Maji na hivyo Serikali yetu kuonekana kama haifanyi kazi sawa sawa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli huduma ya maji katika Mkoa wa Mtwara haitoshelezi. Sasa tumejipanga vizuri kuweza kufikisha azma hiyo, kwa sababu tumewaahidi Wananchi kwamba ifikapo 2015, asilimia 65 watapata huduma ya maji. Tumejipanga kutekeleza huu Mradi ambao tunao. Vilevile kuna misaada mingine, kwa mfano, Serikali ya Japani imeahidi kutoa Dola 100,000 kwa ajili ya kuendeleza Miradi katika Halmashauri hii ya Nanyumbu pamoja na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kwamba, Mradi wa Makonde, umecheleweshwa kwa sababu ya kumlipa mkandarasi, labda suala la kumlipa mkandarasi nilifuatilie ili niweze kuona limefikia wapi kwa sababu ni azma ya Serikali kwamba, kama mkandarasi amefanya kazi inayoridhisha ni lazima tumlipe.

Na. 111

Mradi wa Maji Katika Vijiji Kumi kwa Kila Wilaya

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Mradi wa Maji kwa Vijiji Kumi kila Wilaya Nchini unaogharamiwa na Benki ya Dunia ni wa gharama kubwa sana kwani unagharimu kati ya shilingi 200,000,000 hadi 400,000,000 kwa kisima licha ya kwamba Wananchi watatakiwa kuchangia:-

Je, Serikali haioni kuwa gharama ya asilimia kumi ambayo Mwananchi atatakiwa kuchangia ni kubwa sana hivyo kuna hatari ya Miradi kukwama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upimaji wa maji chini ya ardhi Wilayani Mbozi, umeonesha kuwa uchimbaji wa visima utakuwa wa kina kati ya mita 70 hadi 150 chini ya ardhi. Uchimbaji wa kisima kimoja chenye kina cha mita 70 hadi mita 150 unagharimu wastani wa shilingi milioni 15 hadi 28.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Machi, 2011, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ilisaini Mkataba kati yake na Kampuni ya Uchimbaji wa Visima ya *Ardhi Water Dwells*, ikishirikiana na *Pump International*, kwa ajili ya kuchimba visima kwenye vijiji kumi

vya Halmashauri. Kazi ya uchimbaji imekwishaanza kwenye Kijiji cha Ihanda. Jumla ya visima kumi vitachimbwa katika Vijiji vyote kumi. Baada ya kukamilisha uchimbaji wa visima, kazi ya usanifu na uandaaji wa zabuni za Miradi itafanyika ikifuatiwa na ujenzi wa miundombinu ya maji. Mradi huo unatekelezwa katika Vijiji vya Ihanda, Lungwa, Maninga, Kulungu na Utambulila, ambavyo vipo Jimbo la Mbozi Mashariki na katika Vijiji vya Ntambalala, Iyendwe, Nyuzi, Chilulumo na Itumbula ambavyo viko Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Wananchi kwenye vijiji kumi vilivyochaguliwa na Halmashauri, wanatakiwa kuchangia asilimia 2.5 ya gharama ya Mradi. Maelekezo ya Serikali ni kuwa, katika Miradi yote ya Maji ya Bomba, Wananchi huchangia asilimia 2.5 ya gharama ya Mradi, kiwango ambacho Wananchi wanaweza kumudu kuchangia. Hivyo, hakuna hatari ya ujenzi wa Mradi kukwama. Kulingana na Sera ya Maji, uchangiaji huo unahamasisha Wananchi kuona kuwa Miradi hiyo ni yao na kuwajibika kuitunza na kuifanya kuwa endelevu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ambayo yanaonesha pia Wananchi hawatakuwa na mzigo mkubwa wa kuchangia kwenye Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Wilaya ya Mbozi ina Vijiji 201; kwa msingi huo ni Wilaya kubwa na kwa maana hiyo vijiji kumi ambavyo tumepewa ni vichache sana. Sasa, Serikali haioni kwamba kuna sababu ya kuifikiria Wilaya kubwa kama Mbozi wakatupa vijiji vingi zaidi ili Wananchi wengi zaidi waweze kufikiwa lakini pia *speed* ya Miradi yenyewe ikaongezeka maana utekelezaji wake unasuasua?

(ii) Serikali ilikubali kugharimia Mradi mkubwa wa Maji wa Lukululu ambao uko katika Kata ya Mlangali na Mradi huo utakapokuwa umekamilika, utavisaidia vijiji ambavyo vipo kwenye Kata ya Mlangali, Kata ya Myovizi pamoja na kutoa ziada ya maji katika Kata ya Mlowo. Serikali inatuambia nini maana imechukua muda mrefu na Wananchi wa maeneo hayo hawaelewi kinachoendelea? Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kweli Mbozi ni kubwa, ina vijiji hivyo alivyosema 201 na ndiyo maana Serikali imeigawa Wilaya hiyo kuwa Wilaya mbili; kuna Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Momba. Sasa, kwa maana kwamba Wilaya ya Momba nayo itakuwa na programu ya vijiji kumi na Wilaya ya Mbozi itakuwa na Programu hiyo; pamoja na hilo, tuna washirika wengine wa maendeleo ambao wanaendelea kufadhili katika Maendeleo ya Sekta ya Maji. Tuna hiyo *Local Government Capital Development Fund*, tuna Madhehebu mbalimbali ya Dini na tuna Wadau wengine ambao wamejitokeza katika kufadhili maendeleo ya Sekta ya Maji. Pia kwa mwaka ujao, Serikali imeahidi kuongeza Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, nina imani kabisa kwa kufanya hivyo, Vijiji vingi vitapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu Mradi wa Lukululu; ni kweli kwamba, tulichelewesha kiasi, lakini sasa hivi usanifu umekamilika na kazi hizo zitaanza katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

MHE. MOHAMED G. DEWJI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa matatizo ya maji ya Jimbo la Mbozi Mashariki yanafanana na Jimbo la Singida Mjini; kuna tatizo kubwa sana la maji Singida Mjini na kuna Mradi mkubwa ambao umefadhiliwa na Benki ya *BADEA* na *OPEC* wa zaidi ya shilingi bilioni 20 kubadilisha miundombinu yote ya maji safi ndani ya Jimbo la Singida Mjini; nitapenda kumwuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri, je, huu Mradi utakamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna Mradi mkubwa wa Maji katika kukarabati miundombinu ya maji na kuweza kupata chanzo cha uhakika wa maji katika Mji wa Singida. Mradi huo unaendelea vizuri na siwezi kuwa na jibu kwamba lini utakwisha, lakini upo kwenye *track* unaendelea vizuri, nikipata *data* lini unakamilika nitamjulisha Mbunge.

SPIKA: Waziri wa Maji, nilikuangalia nikaona umekaa.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama Mbozi Vijijini na Singida Mjini vinalingana, lakini ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tumekubaliana na Mheshimiwa Dewji kwamba, kabla ya Bunge lijalo, nifike kule nitembelee Mradi huo mkubwa tukiwa pamoja ili tutoe msukumo kuhusu ukamilishaji wa Mradi mkubwa wa Singida Mjini.

Na. 112

Tatizo la Uhaba wa Walimu Nchini

MHE. AMOS G. MAKALLA aliuliza:-

Walimu ni tegemeo kubwa katika kufundisha wanafunzi kuanzia shule za awali mpaka vyuoni lakini kuna uhaba wa walimu hao kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu yakiwemo yale ya Kata za Kibati, Pembe, Maskati na Vijiji vya Ubiri, Kisimagulu, Mndela, Mziha, Lukuyu na Msengela katika Jimbo la Mvomero:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kutatua tatizo hilo kwenye maeneo yaliyotajwa?
- (b) Kama Serikali italitua tatizo hilo, je, imejiandaaje kwa ujenzi wa nyumba za walimu?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge wa Jimbo la Mvomero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa, walimu wa kutosha wanapatikana ili kukidhi mahitaji katika shule za msingi, sekondari na elimu ya juu nchini. Kwa shule za msingi na sekondari, pindi walimu wanapomaliza mafunzo yao, Serikali huwagawa katika ngazi ya Halmashauri na Halmashauri nazo huwagawa katika shule kulingana na mahitaji. Ili kukabiliana na uhaba wa walimu, Serikali itaendelea kuweka mkazo kufundisha walimu zaidi kila mwaka na Wizara itaendelea kuwapanga walimu wahitimu kwenye Halmashauri ili kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, ilipewa mgao wa walimu wa Shahada 30 na wa Stashahada 32. Kwa upande wa shule za msingi, Halmashauri ya Mvomero haikupata mgawo wa walimu kutokana na uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kuwa 1:43, ambao ni uwiano mzuri ukilinganishwa na ule wa Kitaifa wa 1:51. Halmashauri ya Mvomero ina jumla ya shule za msingi 142, wanafunzi 60,111 na walimu 1,407. Aidha, tunaishauri Halmashauri iangalie upya mgawanyo wa walimu katika shule zake.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada za kujenga nyumba za walimu kulingana na uwezo wa kifedha. Kwa upande wa shule za msingi, kwa mwaka 2009/2010, Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, imetumia jumla ya shilingi 68,088,000 kwa ajili ya kujenga nyumba mpya mbili za walimu na kumalizia ujenzi wa nyumba 19 za walimu. Aidha, Serikali kupitia MEM II na MMES II, itaendelea na juhudi zake kuhakikisha ujenzi wa nyumba za walimu unakamilika. Juhudi hizi ni pamoja na mchango wa nguvu za Wananchi wa Halmashauri husika.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Majibu ya Waziri yanasema kwamba, wana walimu 30 wa Shahada na Stashahada 32, lakini tatizo la walimu kwa sekondari bado lipo. Ameeleza pia kwamba, mwaka 2011 hawakugawa walimu kwa sababu uwiano wa moja kwa arobaini na tatu ni mzuri na Kitaifa ni moja kwa hamsini na moja.

Anazo taarifa kwamba, pamoja na uwiano huo zipo shule kama Kisimagulu uwiano ni wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi mia moja na shule ya Ubiri mwalimu mmoja kwa wanafunzi mia nne:-

(a) Je Waziri anazo taarifa hizo?

(b) Amesema kwamba Serikali ilitenga milioni sitini na nane kujenga nyumba mbili za Walimu; anaweza kunitajia nyumba hizo zimejengwa katika Kijiji gani, Kata gani na pia anazo taarifa kwamba walimu wengi katika Jimbo la Mvomero wanakaa katika nyumba za nyasi na miti?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kuhusu kukosa walimu wa shule za msingi, mgawo wa mwaka 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kama nilivyosema, sababu kubwa ilikuwa kwamba uwiano wao ni mzuri zaidi kuliko Wilaya zingine. Katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ambazo zina uwiano kati ya walimu na wanafunzi ni Mvomero, inafuata Morogoro Mjini ambayo sasa

hivi ina uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi ishirini na tisa, tofauti sana na uwiano ule wa Kitaifa wa moja kwa hamsini na moja.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba, tofauti hiyo lazima itakuwepo, huu ni uwiano ndani ya Halmashauri na Halmashauri ina shule nyingi; kwa hiyo, ukichukua wastani unapata uwiano huu mzuri. Lazima kuwe na tofauti kati ya shule na shule na wito wangu ilikuwa kwamba, Halmashauri iangalie sasa namna ambavyo ita-*balance* katika shule mbalimbali. Pale ambapo wamezidi sana, uwiano umekuwa moja kwa thelathini, waondoshwe ili waweze ku-*balance* katika shule zile ambazo zina matatizo makubwa. Sina uhakika wa namba katika Shule ya Msingi ya Ubiri na Kisimagulu, lakini kama kuna tofauti kama hiyo, basi Halmashauri ifanye kazi hiyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za walimu zipo katika kijiji gani; jibu hilo siwezi kumpa sasa hivi, sina taarifa zimejengwa katika Kijiji gani na nina imani kwamba, Mbunge bila shaka anafahamu ni wapi, lakini pesa zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo mbili pamoja na kumalizia zile ambazo zilikuwa zinahitaji kumaliziwa. Sisi tutaendelea kuweka mkazo chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Pili na Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili ili kuhakikisha kwamba, tunajenga nyumba nyingi zaidi kwa ajili ya walimu wetu.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona na kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa huu utaratibu wa kuwagawa walimu kwa uwiano bado umeonesha kwamba kwa wakati tuliona sasa na hasa tunapozidi kuwapokea wanafunzi chini ya Mpango wa MEM, wanaomaliza shule za msingi ni wengi sana na kuwa wengi pia katika shule za sekondari; na kwa kuwa utaratibu huu umekuwa hauleti usawa katika shule nyingi na hasa vijijini:-

Je, Waziri yupo tayari sasa kufanya marekebisho ya ugawaji wa walimu na kuondoa kigezo hiki cha uwiano ambacho kimekuwa kikisababisha matatizo makubwa ili kusaidia shule nyingi za sekondari zipate walimu wengi wa kutosha na ili kusaidia shule za msingi zipate walimu wa kutosha? Je, yupo tayari kurejea upya utaratibu huu ili kuondoa hii kero kubwa sana kwa walimu wenyewe na wanafunzi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ninaomba ujibu kwa kifupi tu, maana muda haupo.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao tulikuwa tunautumia sasa hivi ni kufuatana na upungufu katika shule zetu, kwa maana hiyo tulikuwa tunapeleka walimu katika Halmashauri hizi kufuatana na takwimu za upungufu wa walimu katika shule zinazohusika. Kama hili bado lina mgogoro, ninachukua mapendekezo haya ya Mbunge ili mimi pamoja na Wataalamu katika Wizara, tuangalie namna bora zaidi ambayo itaweza kuleta mafanikio katika shule zetu.

Ujenzi wa Chuo cha VETA

MHE. JUMA A. NJWAYO aliuliza:-

Vyuo vya Ufundi (*VETA*) vimekuwa vikisaidia sana kupunguza tatizo la ajira kwa vijana. Kutokana na ukweli huo, Halmashauri ya Tandahimba imetenga karibu ekari 70 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*:-

Je, ni lini ujenzi wa Chuo hicho utaanza Wilayani Tandahimba ili vijana waweze kufaidika na huduma hiyo?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi hutanguliwa na zoezi la kutambua stadi zinazohitajika kufundishwa katika eneo husika kwa kushirikisha Uongozi wa Wilaya na jamii husika. Zoezi la utambuzi wa stadi za kufundishwa katika Wilaya ya Tandahimba limekwishafanyika. Kwa vile Wilaya ya Tandahimba haipo katika orodha ya Wilaya zitakazojengewa Chuo cha Ufundi Stadi katika awamu ya kwanza, Wananchi wa Wilaya hiyo waendeleo kupata huduma ya mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Stadi cha Mkoa wa Mtwara kilichopo Mtwara Mjini. Wilaya ya Tandahimba ipo katika kundi la awamu ya pili ya kujengewa Vyuo vya Ufundi stadi vya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, ninachukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, aendeleo kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi ambapo Wilaya ya Tandahimba pia inahusika.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kumpongeza Waziri, kwa jibu lake lenye kutia matumaini kwa Wananchi wa Tandahimba kwamba, mambo yanakaribia na kwamba chuo kitakuwepo kule muda si mrefu sana. Hata hivyo, ninapenda kutoa maswali ya ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa kupitia jibu lako tayari Wananchi wa Tandahimba wamepata hamu sasa ya kujua kwamba Chuo kiko njiani kinaletwa; je, haoni kwamba ni vizuri basi zile stadi zilizotambuliwa ziwekwe wazi ili Wadau mbalimbali wa Maendeleo wa Tandahimba waweze kushauri ipasavyo?

(ii) Je, Chuo hicho kitakapokamilika kitadahili wanafunzi wa kuanzia wangapi?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, moja ni kuhusu stahili ambazo zinatambulika katika Wilaya hii. Stahili kama nilivyojibu

katika jibu langu la msingi kwamba, zilihusisha Wananchi wenyewe husika ili kuzitambua stahili gani zifundishwe pale. Kwa taarifa ya Wanajimbo la Mheshimiwa Mbunge, stadi hizi ambazo zimetambuliwa ni ufundi seremala, uwashi, ubanguaji korosho, ushonaji nguo, kilimo na ufugaji, usindikaji wa mazao ya kilimo, ufundi umeme wa majumbani na ufundi wa magari. Kwa hiyo, kuna stadi nane ambazo zimetambulika na kuna stadi kumi na tatu ndiyo zinafundishwa katika Chuo cha Ufundi cha Mkoa kilichopo Mtwara Mjini. Kwa hiyo, katika hizi, kama kutakuwa na tatizo lolote, tuko tayari kupokea maelekezo kutoka Wilayani.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba, tutadahili wanafunzi wangapi; kwa kuanzia hili kwa sasa hivi sitaweza kulisema, tutasubiri mpaka tukiwa tayari kufungua kile Chuo na kukitathmini uwezo wake, tutataja kama ni wanafunzi wangapi tutaanza kuwadahili kwa kipindi hicho.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa lengo la Serikali kuanzisha Vyuo vya VETA ni kuwasaidia vijana kupata ajira kwa kujiajiri; je; ni mkakati gani umewekwa na Serikali wa kuwapatia mitaji ya kuanzisha Miradi mara wanapohitimu hayo mafunzo? (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka Mkakati Maalum wa kujenga Vyuo vya Ufundi katika Wilaya zote 140 za nchi yetu kwa kuhakikisha kwamba, vijana wetu wana taaluma zinazofaa ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi. Kupitia katika Wizara ya Kazi na Ajira, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ambayo itawezesha vijana hawa wanapoweza ku-graduate kuweza kuingia katika soko la ajira wakiwa na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa letu. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamekwisha.

Kwanza kabisa, ninawakaribisha wageni wote mliokuja kutusikiliza, mkipewa nafasi ni haki yenu, lakini sitawatangaza nyote mliopo hapa bali nyote mnakaribishwa. Ninaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi leo hii mara baada ya maswali katika Ukumbi wa Spika. Kwa hiyo, baada tu ya maswali na taarifa, kabla hatujaingia kwenye Azimio, Kamati ya Uongozi tutakuwa na kikao cha dharura.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati yake kwamba, leo hii kutakuwa na kikao saa tano na nusu eneo la kukutania ni *basement* na mnakutana kujadili ratiba ya kazi kwa mwezi Mei, 2011.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika chumba namba 227.

Mwenyekiti wa *TAPAC*; *TAPAC* ni *Tanzania Parliament Aids Coalition*, Umoja wa Kupambana na Ukimwi katika Mabunge. Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa *TAPAC* pamoja na Wabunge wengine wote wanaotaka kujiunga na *TAPAC* kuwa, kutakuwa na kikao leo tarehe 15, saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement*; Wabunge wote wanakaribishwa. Pia nimeona anagawa fomu za kujiunga.

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tumepanga uchaguzi wa Jumuiya ya Madola (*CPA Tanzania*), ufanyike leo mchana; ninadhani Naibu Spika, alitangaza jana, lakini baada ya kushauriana na wenzetu wengine wengi tumekubaliana kwamba, huu Mkutano ufanyike kesho mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge. Tutafanyia Ukumbi wa Msekwa, kwa sababu hiki siyo Kikao cha Bunge, ni Kikao cha Vyama vya Kibunge.

Kwa sababu hiyo basi, kutokana na waliojitokeza kugombea nafasi ya Uwakilishi wa Kamati ya Utendaji wa *CPA*, Tawi la Tanzania kutotosheleza idadi ya Wajumbe wanaotakiwa, tuongeze muda wa kuchukua fomu mpaka kesho saa nne asubuhi na uchaguzi ufanyike kama ilivyopangwa kesho baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge.

Kwa hiyo, ninaomba wale wanaopenda kuingia katika Chama hiki, waendeleo kuchukua fomu mpaka kesho saa nne asubuhi. Ninajua kwamba, Wabunge wengi hamjui maana ya *CPA*, tutawaeleza kesho. Sisi ni Wanachama wa Jumuiya ya Madola kama Bunge Kimataifa, Dokta Shija aliyekuwa Mbunge wetu na Waziri hapa ndiyo Katibu Mtendaji.

Halafu sisi wenyewe *Tanzania Branch* pia ni Mwenyekiti wa *Branch* hii katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, sisi ni Mwenyekiti wa *Branch* ya Bara la Afrika. Kwa hiyo, unakuwa na Bara halafu, unakuwa na tawi la nchi. Sasa tawi la nchi hii ndio anakuwa mwenyeji wa mikutano hiyo mingine yote ndio maana Wajumbe wake walioomba fomu siyo wengi. Kwa hiyo, nawashawishi mwombe, kesho ndio tufanye uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tulipoanza Bunge hapa tulianza tu kwa kukaa kama tulivyokaa. Lakini mnaona ukumbi wetu ni mkubwa halafu sisi wenyewe tuko wengi na bila kuwa na utaratibu wa kukaa hapa, mpaka miaka mitano Spika au Mwenyekiti atakayekaa hapa hatajua nani amekaa wapi au akisimama ni nani. Kwa hiyo, nafikiri jana walitangaza, tunataka kila mtu alipokaa watatoa vikaratasi vidogo, andika tu jina lako pale unapotaka kukaa hapo hapo halafu sisi tutazitengeneza katika *format* tunayoweza ku-*identify*, ukisimama tu hata kama hauonekani, lakini hapa tunajua yule ni fulani. Pia itatusaidia sisi wenyewe kuwajua haraka. Maana sasa nikiwaita kama ilivyokuwa zamani hapa, naita akina Mheshimiwa Khatib Said Haji wala siyo yeye, kumbe amekaa mtu mwingine pale.

Kwa hiyo, tunataka kila mtu aandike kwa sababu wakati fulani kulikuwa pia na matatizo, wengine wanasema mimi nilichagua hapa, mtu ananifukuza, ananiambia niondoke. Andika jina lako, bandika hapo hapo kusudi mtakaporudi Bunge lijalo kila mtu atakuwa na jina lake kwa *blend* ya Metal, kwa hiyo, inakuwa *permanent*. Kwa hiyo, naomba mfanye hivyo wakati mtakapokuwa kwenye shughuli zenu nje ya Bunge.

Kwa hiyo, naamini mtafanya hivyo na wale ambao watakuwa hawajaandika, tutajua kwamba hawakuwepo. Kwa hiyo, pia tutaangalia utaratibu wake. Kwa hiyo, tafadhali zoezi hili mlifanye vizuri kwa sababu inatusaidia sisi kuweza kuwafahamu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kueleza hivyo, ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inampa Spika mamlaka ya kupeleka Muswada wa Sheria kwenye Kamati inayohusika ili kuuchambua na kukusanya maoni toka kwa wadau na wananchi wote kwa kuzingatia Kanuni zetu za Bunge.

Kwa kuzingatia Kanuni hiyo, pamoja na Kanuni nyingine zinazohusiana na utangazaji wa Miswada, tarehe 5 Machi, 2011 niliipeleka Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Marekebisho ya Katiba wa Mwaka 2011 [*The Constitutional Review Bill, 2011*] kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili ipokee mawazo (*public hearing*) kutoka kwa wadau na hatimaye kuyachambua na kuleta mapendekezo Bungeni.

Baada na kuufanyia kazi, tarehe 13 Aprili, 2011 Kamati ilileta taarifa ya maelezo ya awali ya namna ambavyo imeufanyia kazi Muswada huu ikiwa ni pamoja na ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 85(1).

Kwa kuzingatia maelezo na ushauri uliotolewa na Kamati hiyo, na kwa kutumia Kanuni ya 2(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 inayotoa mamlaka kwa Spika ya kuamua utaratibu wa kufuata iwapo Kanuni hazikuweka bayana ni nini kifanyike iwapo Kamati iliyopelekewa Muswada haitakuwa imekamilisha kazi kwa muda uliopangwa; Nanukuu Kanuni ya 2(2) “Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Spika ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo, kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za Nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge na Uamuzi huo utaingizwa katika Kitabu cha Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa Shughuli za Bunge”. Mwisho wa kunukuu.

Ushauri na mambo ambayo Kamati imeomba ni haya yafuatayo:-

(a) Muda zaidi utolewe kwa Kamati na wananchi kuufikiria Muswada huu. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: CCM! CCM! CCM!

SPIKA: Kwanza nawashangaa kabisa! Kwani mimi nimesemaje? Nimesema Kamati inaomba. Sasa mbona sijafanya maamuzi? Nyie mnashangilia wakati bado sijafanya maamuzi? Kamati imesema tunaomba muda zaidi utolewe kwa Kamati na wananchi kuufikiria Muswada huu. Hiyo namba moja. Spika, hamumshinikizi kwa makofi wala kwa nini. (*Makofi*)

Kamati inasema Serikali iandae Muswada huu kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi wenyewe waweze kusoma yaliyomo kwenye Muswada huo badala ya kupewa tafsiri tu na watu wengine.

MBUNGE FULANI: Haya maoni ya CHADEMA.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nawaomba mnyamaze. Tungewapa nafasi wananchi kusikiliza ninachokisema, sasa mki-*interfere*, basi wananchi nao hawatasikiliza. Naomba tutulie mpaka nimalize.

(b) Muswada uchapishwe kwenye magazeti na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya Habari ili kutoa fursa ya kutosha kwa wananchi wengi kuuelewa na kuutolea maoni. (*Makofi*)

(c) Utangulizi wa Muswada huu uwekwe vizuri zaidi ili wananchi waelewe madhumuni ya Muswada huu, kwani imeonekana wazi wananchi wengi wanadhani tayari tumeanza kuandika Katiba, kumbe lengo la Muswada huu ni kutunga Sheria ya Kuunda Tume ya Kukusanya Maoni tu. (*Makofi*)

Baada ya kupitia maelezo ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Ushauri wake, mimi Spika, nimeridhika na nimeona ni busara kutoa muda zaidi kwa Kamati ili iendelee na kazi ya kuuchambua Muswada huu na maoni ya wananchi yaweze kupokelewa zaidi na wadau mbalimbali na kuendelea kukusanya maoni mengine kwa lengo la kuuboesha zaidi Muswada huu ili uweze kuwa na manufaa zaidi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwaomba Watanzania kudumisha mila zetu za utulivu na amani. Muswada kwa Lugha ya Kibunge ni mapendekezo tu, safari hii ni mapendekezo ya Serikali kuhusu namna ya kuanzisha zoezi la kuandika Katiba ya nchi. Bunge linawaomba wananchi wote, wasomi, wafanyakazi, wanawake, wanafunzi, wanavyuo, NGOs, walemavu, wakulima, madhehebu ya dini, Vyama vya Siasa na makundi mengine ya kijamii, wajadili mapendekezo ya Muswada, na tuache malumbano, kuzomeana na maandamano na kupigizana kelele.

Waheshimiwa Wabunge, wanasiasa tuache kushindana majukwaani, tujadili Muswada. Maoni, ushauri na mapendekezo ndiyo yatasababisha kutungwa kwa sheria iliyo nzuri kwa manufaa ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Naomba wananchi muiamini Kamati yangu ambayo imejaa watu wenye uzoefu mkubwa na waliobobea katika taaluma mbalimbali ikiwemo ya Sheria. Nomba muipe ushirikiano ili iweze kutekeleza jukumu lake kikamilifu. (*Makofi*)

Muswada huu sio mali ya Chama chochote cha Siasa. Wao pia tunaamini watatumia busara ya kutoa mawazo yao kikamilifu. Ukisema hili liondoke, uwe tayari kusema badala yake tuweke nini? Kwa hatua hii tuliyofikia siyo wakati wa kulaumu au

kulaumiana bali ni kutoa hoja zenye uzito zinazoweza kusaidia kuandika Muswada mzuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kupitia kwenu nawaomba wananchi waepuke uandikaji wa Muswada kwa kuleta fujo ya aina yoyote ile. Ndiyo maana tunaitaka Serikali ilete Muswada kwa Kiswahili na uandikwe kwenye magazeti mbalimbali ili watu wote wasome wenyewe, waulize maswali waondoe jazba ambazo hazina mantiki. (*Makofi*)

Uandikaji wa Katiba mpya iwe chanzo cha kutuunganisha Watanzania wote na kuimarisha Utaifa wetu, kwani lengo letu ni kuwa na Tanzania moja yenye amani na utulivu ambayo itatupelekea kuleta maendeleo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wananchi wote mnaombwa kuendelea kuleta maoni yenu kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kupitia Ofisi za Bunge zilizopo Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. Aidha, ninaiagiza Kamati iniletee ratiba na utaratibu wa kukamilisha kazi hii ili Muswada huu uweze kusomwa mara ya pili katika Mkutano ujao wa Bunge. (*Makofi*)

Nasisitiza utulivu wakati wote wa kazi hii. Kila mwanakamati ajue kwamba shughuli hii inatawaliwa na Kanuni za Bunge na itaratibiwa na kusimamiwa na Kamati husika na siyo Vyama vya Siasa.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni kwa kunisikiliza. Kama nilivyosema, Muswada huu uko ndani ya Bunge, hauko Serikalini. Kwa hiyo, fanyeni wajibu kwa utulivu na amani kama ilivyo desturi ya Watanzania. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

UCHAGUZI WA MBUNGE WA SADC

SPIKA: Msimamizi wa Uchaguzi, utaratibu wa uchaguzi.

ND. JOHN N. JOEL - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyowatangazia Waheshimiwa Wabunge na kama *Order Paper* ya leo inavyoonyesha, tarehe 14 Aprili, 2011 tutakuwa na uchaguzi mdogo wa kuziba nafasi ya Mwakilishi wetu katika Bunge la SADC (*SADC Parliamentary Forum*). Nafasi hiyo iliyo wazi ni ya kundi la wanaume kutoka Chama Tawala.

Nafasi hiyo iliachwa wazi na Mheshimiwa Godluck Joseph Ole Madeye ambaye aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi. Hadi kufikia mwisho wa kurudisha fomu za uteuzi tarehe 14 Aprili, 2011 saa 10.00 jioni ni Waheshimiwa Wabunge wanne tu waliojitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha. Nao ni Mheshimiwa Dr. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Titus Kamani, Mheshimiwa Dr. Faustine Ndungulile na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 8(2)(b) ya nyongeza ya pili, mgombea atapewa fursa ya kufika mbele ya wapigakura na kujieleza. Aidha, kama kutakuwa na maswali, mgombea atayajibu kwa idadi ambayo utakuwa umeelekeza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Umewataja wanaogombea ili waweze kutoka nje? Kwa hiyo, hawa wagombea Dr. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Titus Kamani, Mheshimiwa Dr. Faustine Ndungulile na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo watoke nje. Dr. Charles Tizeba anaweza kubaki. Mtoke kwa haraka mbona mnakuwa wanyonge?

We will also debate in English because a language of media there, is English. Honorable Dr. Charles J. Tizeba, you are given three minutes to explain yourself to this August Assembly then we shall ask you three questions if any.

HON. DR. CHARLES J. TIZEBA: *Madam Speaker, Honorable Prime Minister, Honorable Freeman Mbowe - Leader of the Opposition camp in the house, dear colleagues, Ladies and Gentlemen: My name is Charles Tizeba from Buchosa Constituency. Having gone through the reasons and why we are being represented in this board, and endue consideration of the other contestants, I am giving way to my good friend Dr. Titus Kamani and ask you guys whoever wanted to support me to put his support to that good friend of mine. Thank you very much.*

SPEAKER: *We are accept your removal of the name but we don't accept the other proposal which you are saying we will judge him according to how he is going to represent himself here.*

HON. DR. CHALRES J. TIZEBA: *And that is why Madam Speaker I said I am begging.*

SPEAKER: *Thank you very much. So I am calling upon Honorable Dr. Titus Kamani. Dr. Titus Kamani, the rules did not chance to clap or to do anything. Dr. Titus Kamani you are given three minutes to explain yourself about whatever you want to say to this August Assembly, then we shall give you three minutes to answer three questions if any.*

HON. DR. TITUS M. KAMANI: *Thank you Madam Speaker, Honorable Prime Minister, Honorable Leader of the Opposition, Honorable Ministers, Distinguish Honorable Colleagues Members of Parliament: Standing here in front of you, I am Dr. Titus M. Kamani, a Member of Parliament from Busega Constituency. I am here to vie for the post of the representative of this House to the SADC Parliamentary Forum. This is an important Board where the Member of Parliaments for different member state of the SADC Region where they can discuss issues, policies and advise head of states or the summit in general on the way to move forward and to improve various policies and implementation of the activities of the welfare of the SADC people. This is the organ basically intended to advice on the way to integrate the region the SADC countries into to economic, political and social unit.*

So, I am here to ask for your votes. I have the experience, I have worked in different Government and Public institutions and I believe I will not let you down. I therefore kindly ask you to give me your votes and I am sure I will represent this house effectively for the benefit of our country.

SPEAKER: *Okay. You have the first question from Honorable Engineer Mohamed Mnyaa who is already member of the SADC forum.*

HON. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: *Honourable Speaker, thank you. In fact I have only a small question I would like to ask the candidate. In some books and papers it is mentioned that Seychelles is a member of the SADC but Seychelles has never signed or rectified any of the protocols. Do you have any opinion or can you say something about that? Thank you.*

HON. DR. TITUS M. KAMANI: *Thank you Honourable Mnyaa for the nice question. Surely the SADC country do pass a number of resolutions and protocols and the country as a sovereign state as the right to scrutinise this protocols according to the their conditions and then signed or rectified but as a member of this legislative organ of the SADC, I will use my ability working with the members of the SADC Parliamentary Forum of this country to advise this other country like Seychelles to rectify this important protocol for the well being of our region integration. (Applause)*

SPEAKER: *Second question can be asked by Honourable Mangungu.*

HON. MURTAZA A. MANGUNGU: *Thank you Honourable Speaker. I didn't have my glasses on that why. I would like Honourable Kamani, I have heard that he is Dr. Kamani, what profession are you holding?*

HON.DR. TITUS M. KAMANI: *Honourable Speaker, thank you. Because of the time, surely I couldn't explain all the details of my academic background but I have passed my flyers. For the interest of this House, I have a Degree in Vetenary Medicine at Sokoine University of Agriculture and this gives me an advantage of the livestock policies or the economic policies but I have also got a Masters Degree in livestock economics which is a key bone factor of the economy of this country but for most of the SADC countries, but also I have a Postgraduate Diploma in Wildlife Management and Tourism which all these factors are very important for our country even when I attend this Parliamentary Forum to be able to argue professionally in issues for the nation of the country.*

SPEAKER: *Thank you. The last question, I saw Honourable Kombo.*

HON. MUSSA HAJI KOMBO: *Honourable Speaker, thank you. May I have one question to the candidate? Could you please tell us the Tanzania Policy Constitutionally for SADC Parliament, what is relevant provision?*

SPEAKER: *In our constitution, there is no relevant provision on SADC. Can we have another question? (Applause)*

MEMBER OF PARLIAMENT: *Honourable Speaker, thank you. Could you Doctor Kamani tell this House why do you think that you are right candidate for this position?*

SPEAKER: *Yes, this is a good question?*

HON. DR. TITUS M. KAMANI: *Thank you Honourable Speaker. Actually as I said before, because of my academic and profession background and the working experience, I can surely tell you that I have the competence and may be the best among the other member who are fighting for this thing, but the other SADC policy promotes even our country for equitable sharing of opportunities and resources and as I stand here, this is the only time I have asked for any post in this House. So I think I have the consideration of other people to make sure that we are represented equitable. Thank you.*

SPEAKER: *Thank you very much Dr. Titus Kamani, you can now ask for the votes.*

HON.DR. TITUS M. KAMANI: *Thank you Honourable Speaker, the Honourable Prime Minister, Honourable Leader of the Opposition, Honourable Members of this House, kindly trust in me give me your votes. You have the right, you have the final decision and I really need you, I will not let you down, surely.*

SPEAKER: *Thank you very much, take your seat. Now I am calling Honourable Dr. Faustine Ndugulile. Honourable Dr. Faustine Ndugulile you are given three minutes to explain yourself to this august assembly and then we will ask you three questions if any.*

HON. FAUSTINE E. NDUGULILE: *Honourable Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Leader of Opposition, Honourable Ministers, my fellow Members of Parliament. My name is Dr. Faustine Ndugulile. I am a Member of Parliament of Kigamboni Constituency. I stand here before you to kindly request for your votes to represent this August House to the SADC Parliamentary Forum. I have a medical background and a medical specialisation. I have worked with the Ministry of Health but I have also worked extensively in the SADC region and my technical capacity in the health sector. Honourable Members of the House, I kindly request your votes to be your representative in the SADC Forum.*

SPEAKER: *Question? Who will ask the first question? Honourable Leticia Nyerere.*

HON. LETICIA M. NYERERE: *Thank you so much Honourable Speaker. Could you please give me a list of three SADC objectives?*

HON. FAUSTINE E. NDUGULILE: Thank you Honourable Nyerere. SADC started in 1980 as a front line state with the aim of liberating the countries but it came to be in current shape and form in 1992. The current objectives now is economic integration within the regions to be promote peace and prosperity, but also to promote social justice and also economic integration and prosperity of the people within the region.

SPEAKER: The second question. Who is that one? Can you ask that question?

A CERTAIN MEMBER OF PARLIAMENT: Thank you Honourable Speaker. Honourable Dr. Faustine Ndugulile, can you tell us more about your educational background?

SPEAKER: Can you answer the question Dr. Faustine?

HON. FAUSTINE E. NDUGULILE: Could you repeat your question Sir?

A CERTAIN MEMBER OF PARLIAMENT: Honourable Speaker, your education background Sir.

HON. FAUSTINE E. NDUGULILE: Thank you Honourable Speaker. As I mentioned earlier, I am a medical doctor by profession. I am a public specialist, also infection diseases specialist. I have worked with the Ministry of Health as Head of Diagnosis Service but also as the Program Manager for Blood Transfusion Services. In the last three years, I was a Resident Advisor in South Africa, advising the Government of South Africa, but also quite of number in some other countries within the SADC Region but I am also in the International Forum. I am a Representative of Africa in the International Aids Society. (Applause)

SPEAKER: Ok. The second question, Dr. Mwanjelwa.

HON. MARY M.MWANJELWA: Honourable Speaker, thank you for having an eye on me. Dr. Ndugulile you have just mentioned your profession that you have a medical background. As you know the SADC Forum is totally under the economic diplomacy as well as integration: can you convince this House how are you going to tackle your activities under this SADC for the benefit of this country as well as for this House of Assembly? Thank you.

HON. FAUSTINE E. NDUGULILE: Thank you Honourable Dr. Mwanjelwa. SADC is not limited only to economic integration, there are so many other things that fall under SADC including the health desk among of which HIV/AIDS, maternal and child health are one of the areas that being held. So I think I can utilise my experience as a Medical Doctor and my extensive experience within the region for some of these activities.

SPEAKER: Thank you very much. The last question. Oh, they are finished? Ok, I was overwhelmed by the answers.

HON. FAUSTINE E. NDUGULILE: Honourable Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Leader of the Opposition, Honourable MP's, I kindly request for your votes. Thank you very much.

SPEAKER: Thank you very much, take your seat and now I am calling on the last candidate. Honourable Selemani Saidi Jafo, we are giving you three minutes to explain yourself to this August Assembly and then we will ask you three questions if any.

HON. SELEMANI S. JAFO: Honourable Speaker, thank you, Prime Minister, The Head of the Opposition and Honourable Member of Parliament. My name is Suleiman Said Jafo, a Member of Parliament from Kisarawe Constituency in coast region. Currently I have to explain my age because someone once saw me and said what is your specific age? My age is 38 years old and I am an economist, I am a holder of Masters of Science and Community Economic Development from southern new emptier. I decided to ask for this position as to make sure that I am bringing the effort of Tanzania to SADC Parliamentary meeting.

What I believe is that if the SADC Parliamentary meeting is a forum which just comprises the Member of Parliament from various SADC countries so as to share experience regarding the good governance and other issues related to the economic integrations. What I have to say to you is just believe me, I am going to represent you in this forum, very effectively because I am very competent in all keys management areas, I am very competent in financing, in program implementation in all issues related to the policy as well as economic development in various area. Thank you very much.

SPEAKER: So, the first question goes to Honourable Sadifa.

HON. SADIFA JUMA KHAMIS: Honourable Speaker, thank you for giving me this juridical and marvellous opportunity to ask my question. My question is that, please can you tell us at least one achievement for Tanzania being a member of SADC?

HON. SELEMANI S. JAFO: Honourable Speaker, Honourable Sadifa, achievements of SADC which we achieved through this SADC, we have a lot especially on the economic development in our country. As you see that currently we have various negotiations regarding economic development in our areas, so, if we have this sharing it means that is the main achievement that we have in our country and we have to be proud of. Apart from that, our colleagues are proud of us because we have peace and security in our country. They are very proud of us. This is a better achievement and sharing achievement in our country. So what I want to say is that, you have to believe me, I am very energetic, am a very young boy, I am honest, I will represent you in that board of forum.

SPEAKER: *The second question will be asked by another young boy, Machali. (Laughter)*

HON. MOSES J. MACHALI: *Honourable Speaker, thank you for giving me this opportunity to question my colleague MP, young boy as me. My question is what does SADC stand for?*

HON. SELEMANI S. JAFO: *Honourable Speaker, SADC is South African Development Community, but this formally was SADC (South African Development Coordination Conferences). Currently, now when you say SADC it is South African Development Community but before it was South African Coordination Conferences relating to the liberation to Southern countries.*

SPEAKER: *The last question Dr. Kigwangala today you have put a really good suit, we can't even recognise you. (Applause)*

HON. DR. HAMIS A. KAGWANGALA: *Honourable Speaker, thank you very much for your compliment. I would very much want to ask my colleague, Honourable Selemani the following question. You seem to be very confident and very competent in your knowledge and academic background. I would like to ask, how are you going to utilise all that competence that you have in representing this good country in the SADC? Thank you very much.*

SPEAKER: *It is the last question, can you answer it please.*

HON. SULEIMAN S. JAFO: *Thank you Honourable Hamis Kigwangala. First of all I want to give you a valid experience. Now I have five months, I try a lot in my level best to solicit funds for my country. As you heard, I think two month ago, Mr Jafo got an accident during a visit with the Chinese. I wrote a very big project from China and my District Kisarawe, currently we are going to construct one Primary School and support one secondary school. Apart from that, with the Minister for Education we did a lot. So, what I am going to do is just to bring my effort to the SADC countries for the sharing and putting the effort to other people so as to grow together. Thank you very much.*

SPEAKER: *So, this was the last question and I give you a chance to ask for votes. I am giving you a final chance to ask for votes.*

HON. SULEIMAN S. JAFO: *Thank you Honourable Speaker. As I said, formally I am an economist master holder. I am very competent in all key management areas. I need you just to give me votes so as to represent you in SADC countries. Thank you. I wish you all the best, I need your votes.*

SPEAKER: *Thank you. This was the last candidate. Now you can take your seat please. Haya, tunaomba mpige kengelele ili watu wote waingie. Idadi ya Wabunge mmeshahesabu muanze kugawa karatasi? Tufanye haraka ni zoezi dogo.*

ND. JOHN JOEL - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI: Mheshimiwa Spika, karatasi inayogawiwa sasa hivi ina majina manne, lakini jina la kwanza lifutwe kwa sababu mgombea amejitoa. Yatabakia majina matatu, la Mheshimiwa Dr. Titus Kamani, Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile pamoja na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo. Kati ya hao watatu anapigiwa kura mmoja tu.

(Hapa Kengele ililia kuwaita Waheshimiwa Wabunge)

SPIKA: Gaweni karatasi haraka haraka na mnaopiga kura pigeni haraka tuendelee na *other business*.

(Hapa karatasi za kura ziligawiwa)

SPIKA: Anzeni kukusanya kura na wanaogawa makaratasi wamalize kugawa upesi.

(Hapa upigaji kura ulianza)

SPIKA: Mnaoandika andikeni upesi kusudi tumalize upesi zoezi hili. Abdallah pita hapa, chukua pale na pale. Nenda kwa AG. Kuna aliyekosa kura? Nani kakosa? Mnaokusanya kura, fanyeni haraka.

Waheshimiwa Wabunge, nani bado ana karatasi? Anayeangalia kule nani? Mshirikiane, hizi karatasi zimesambaa.

(Hapa karatasi za kupigia kura zilikusanywa)

SPIKA: Kama tumekusanya kura zote, Mheshimiwa Dr. Titus Kamani, nani *agent* wako?

MHE. DR. TITUS M. KAMANI: *Sorry, Madam Speaker there is free voters here we are just getting.*

SPIKA: *Who have done what? They have not voted? Who are these? Have you seen those three? Wapeni karatasi kule nyuma. Karatasi ngapi? Tatu.*

MHE. DR. TITUS M. KAMANI: *Two, Mama Anna.*

SPIKA: *The four please stand up so that we can see you. Mama Anna Abdallah and Shellukindo and the others.*

MHE. DR. TITUS M. KAMANI: *I haven't collected vote Madam Speaker.*

SPIKA: *Uncollected votes. Can you lift it up. Hebu angalieni watu mnaohusika. Mbona hamwangalii? Watu wanaohusika, mbona hamwangalii watu wanaouliza hawajakusanya kura? Kule watu wana kura kule. Uncollected votes, nyie, that side.*

Naomba mkusanye kura, sijui kwa nani kule. *Okay! I was asking Dr. Kamani, can you have your agent or you can go yourself? I don't know.*

MHE. DR. TITUS M. KAMANI: *Thank you. I do appoint Honorable Esther Midimu of Special Seats as my agent.*

SPIKA: *Honorable Esther, then Dr. Faustine Ndugulile. Who is your agent.*

HON. DR. FAUSTINE E. NDUGULILE: *I do appoint Dr. Esther Bulaya to be my agent. (Applause)*

SPIKA: *The good neighbor. Honorable Sulemani Saidi Jafo, who is your agent?*

MHE. SULEMANI SAIDI JAFO: *Honourable Sadifa Juma Khamis, will be my agent.*

SPIKA: *Honourable Sadifa, where are you? Okay. Nyie vipi? Naomba mshiriki ma-box mpeleke kule ndani. Msimamizi wa Uchaguzi, naona unaniangalia. So you are going inside there?*

*I have some few announcements. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo - Mheshimiwa Simbachawene, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake waende Basement wakakamilishe kazi ya Muswada uitwao *Judicial Administrative Bill*. Naomba mwende sasa hivi kwa sababu tutakuja jioni.*

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba watakutana saa 7.00 mchana kwenye Ukumbi wa Msekwa C. Halafu mgombea huyu, Mheshimiwa Dr. Titus Kamani anaomba kama mtu ataiona simu yake imeanguka humu Ukumbini, *it will be generous to give it back to him. Amedondosha simu yake in this House.* Kwa hiyo, muwe tayari kumpa hiyo simu yake.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza, nina Kamati ya Uongozi sasa hivi. Kwa hiyo, nitaomba Mwenyekiti wa Bunge - Mheshimiwa Jenista Mhagama anipokee wakati tunaendelea na Kikao hicho. *(Makofi)*

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Naomba kwa kuwa nimekaa hapa Mezani kwa mara ya kwanza, niendeleo kuwashukuru tena kwa ushirikiano wenu na baada ya kukabidhiwa Kiti hiki, kwa mara ya kwanza nimwombe Katibu atupe utaratibu ili tuendeleo na agenda inayofuata. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

**Azimio la Bunge la Kurekeisha Mfuko wa Kutoa Mikopo (*Advance Fund*)
kwa Wabunge na Kuunda Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi
wa Serikali Kuu**

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la kumwezesha Waziri wa Fedha kurekebisha Mfuko wa Kutoa Mikopo ujulikanao kama *Advances Fund* na kuunda Mfuko wa Mikopo kwa watumishi wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda - Mbunge wa Handeni kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili. Napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Kamati kwamba michango yao tunaithamini na tutaendelea kuifanyia kazi ipasavyo katika kuuboresha Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu wa *Advances Fund* ulianzishwa kama *Revolving Fund* chini ya iliyokuwa Sheria ya *Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961 ambayo ilifutwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura ya 348 (*Republic Finance Act*), kwa madhumuni ya kuwakopesha Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Serikali vyombo vya usafiri pamoja na vyombo vya nyumbani ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi katika huduma ya kutoa mikopo, Serikali imeona kuna umuhimu wa kurekebisha *Advances Fund* ili uhudumie Waheshimiwa Wabunge pekee na kuunda Mfuko wa Mikopo kwa watumishi wa Serikali utakaojulikana kama Mfuko wa Watumishi wa Serikali Kuu, yaani *The Public Service Advances Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Serikali inazingatia umuhimu wa kuleta mazingira bora ya kazi, kuongeza ufanisi na tija kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali;

NA KWA KUWA Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia Waheshimiwa Wabunge mikopo ya fedha za kununua vyombo vya usafiri;

NA KWA KUWA Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia watumishi wa Serikali mikopo ya fedha kwa ajili ya kununua vyombo vya usafiri, vyombo vya nyumbani na matengenezo wa vyombo vya usafiri;

NA KWA KUWA kumekuwepo na Mfuko uitwao *Advances Fund* ambao mtaji wake ni kiasi cha shilingi bilioni 43 ulioongezwa kwa mara ya mwisho mwaka 2010

kupitia Azimio la Bunge Na. 7, 2010 ambao awali ulikuwa ukitumika kwa kukopesha Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wa Serikali; na

KWA KUWA Serikali ina nia ya kuporesha utoaji wa mikopo kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Serikali; na

KWA KUWA Serikali imeona umuhimu kwa Mfuko wa *Advances Fund* kufanyiwa marekebisho ili uweze kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge pekee; na

KWA KUWA Serikali imeona pia umuhimu wa kuanzisha mfuko maalum utakaohudumia Watumishi wa Serikali Kuu pekee; na

KWA KUWA upo mchakato wa kuboresha Mifuko ya Mikopo kwa Serikali ya Mitaa; na

KWA KUWA Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ana mamlaka ya kuanzisha Mfuko anapona inafaa kwa manufaa ya umma chini ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za umma Sura ya 348; na

KWA HIYO BASI, madhumuni haya maalum, Bunge hili katika Mkutano wa Pili, linaazimia kwamba:-

Kwanza, Mfuko uliopo sasa ujulikanao kama *Advances Fund* utumike kwa ajili ya kutoa fedha za mikopo ya vyombo vya usafiri kwa Waheshimiwa Wabunge ambao utakuwa chini ya Ofisi ya Bunge.

Pili, mtaji wa Mfuko wa Mikopo kwa Waheshimiwa Wabunge uongezwe kutoka shilingi bilioni 14.8 hadi kufikia shilingi bilioni 32.7. Hivyo, ongezeko la shilingi bilioni 17.9 litatolewa na Mfuko Mkuu wa Serikali. Vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Mikopo kwa Waheshimiwa Wabunge itakuwa ni kama ifuatavyo:-

Fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, yaani *Exchequer Account*, gharama ya kuhudumia mkopo *service charge* asilimia tatu itozwe kwa kila mkopo ambayo itatumika katika uendeshaji wa mfuko.

Tatu, faida itokanayo na kuwekeza fedha za marejesho ya mikopo kutoka kwenye mishahara ya Waheshimiwa Wabunge, yenye dhamana na amana ya muda mrefu na muda mfupi.

Nne, vyanzo vingine kwa kadri itakavyojitokeza, kiwango cha mkopo kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na taratibu za uendeshaji wa Mfuko zifafanuliwe kwenye mwongozo wa mfuko, yaani *operation manual* utakaoidhiniwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (*Paymaster General*). Kutakuwa na msamaha wa asilimia 50 ya mkopo kwa Waheshimiwa Mbunge atakayekopa. Mbunge atatakiwa kuweka bima ya mkopo kuiwezesha Serikali kupata fidia kama itatokea Mbunge ameshindwa kesi ya uchaguzi ama kifo au janga lolote linaloweza kutokea.

Utaratibu uandaliwe kati ya Wizara ya Fedha na Makampuni yanayotoa huduma ya bima kwa ajili hii. Kiasi cha asilimia moja ya mtaji kwa Mfuko wa Mkopo kwa Waheshimiwa Wabunge kiwe ni gharama ya uendeshaji wa Mfuko. Kiasi hicho kitajumuishwa kwenye mtaji. Gharama za mfuko ziainishwe kwenye mwongozo wa mfuko, yaani *Operation Manual*. Uundwe Mfuko wa Mikopo utakaowahudumia watumishi wa Serikali Kuu utakaoitwa Mfuko wa Watumishi wa Serikali Kuu, yaani *Public Service Advances Fund* kwa ajili ya kutoa fedha za mikopo ya kununua vyombo vya usafiri, vyombo vya nyumbani na matengenezo ya vyombo vya usafiri.

Mfuko huu utakuwa chini ya Wizara ya Fedha. Mfuko wa Watumishi wa Serikali Kuu uwe wa mzunguko, yaani *Revolving Fund*. Mtaji wa Mfuko wa Mikopo kwa watumishi wa Serikali Kuu uongezwe kutoka shilingi bilioni 27.8 hadi kufikia shilingi bilioni 65.3. Mtaji huo wa awali wa shilingi bilioni 27.8 utahamishiwa katika Mfuko wa Mikopo wa watumishi wa Serikali Kuu. Ongezeko la shilingi bilioni 37.4 itatoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Vyanzo vya mapato ya Mfuko wa Mikopo kwa watumishi wa Serikali Kuu itakuwa ni kama ifuatavyo:-

Fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, yaani *Exchequer Account* wakati wa kuongeza mtaji wa mfuko, gharama ya kuhudumia mkopo, yaani *service charge* asilimia tatu itozwe kwa kila mkopo utakaotolewa ambao utatumika katika uendeshaji wa mfuko. Fedha zitokanazo na mauzo ya vyombo vya usafiri na vifaa chakavu vya Serikali kama ilivyoainishwa katika Waraka Na. 5 wa mwaka 1995 wa mwongozo wa 2009 wa Katibu Mkuu, Idara Kuu ya Utumishi wa Umma kuhusu utaratibu wa kuwauzia, kuwakopesha watumishi wa umma vyombo chakavu vya Serikali.

Ada ya wakala *agency fee* ya kukusanya marejesho ya mkopo ya mikopo ya watumishi wanaokopa kwenye Taasisi ya Fedha ambayo zitatumika katika uendeshaji wa mfuko. Faida inayotokana na kuwekeza *investment* kwenye dhamana na amana za muda mfupi na vyanzo vingine ambavyo vitakuwa vinajitokeza. Viwango vya mikopo kwa watumishi wa Serikali Kuu pamoja na taratibu za uendeshaji wa mifuko zitafafanuliwa katika mwongozo wa mfuko, yaani *operation manual* utakaoidhinisha na Mlipaji Mkuu wa Serikali (*Paymaster General*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imekwishaungwa mkono. Sasa kwa mujibu wa Kanuni, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Azimio hili ama Mwakilishi wake.

MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI – MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Azimio la Kurekebisha Mfuko wa Kutoa Mikopo (*Advances Fund*) kwa Wabunge na Kuunda Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu wa *Advances Fund* ulianzishwa kama *Revolving Fund*, chini ya iliyokuwa Sheria ya *Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961 ambayo ilifutwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 kwa madhumuni ya kuwakopesha Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali vyombo vya usafiri pamoja na vyombo vya nyumbani ili kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeona umuhimu wa kurekebisha Mfuko wa *Advances Fund* ili uhudumie Waheshimiwa Wabunge pekee na kuunda Mfuko wa mikopo kwa Watumishi wa Serikali kuu utakaojulikana kama *Employees Advances Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inakubaliana na Azimio hili kwa kuwa Serikali ina nia ya kuboresha utoaji wa mikopo kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali Kuu, aidha utekelezaji wa Azimio hili utanza mara baada ya kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaiunga mkono Wizara kwa kuwasilisha Azimio hili lenye lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeafiki na inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuweka Mfuko wa *Advances Fund* chini ya Ofisi ya Bunge. Utaratibu huu utatoa madaraka kwa Bunge kama Mhimili, kufuatilia kwa karibu mikopo ya Wabunge, na kadhalika. Aidha, kuanzishwa kwa Mfuko wa Mikopo kwa watumishi wa Serikali kuu utatoa fursa kwa Watumishi wengi zaidi kupata mikopo hiyo tofauti na ilivyokuwa awali. Hatua hizi zitasaidia kujenga mazingira bora ya utendaji kazi pamoja na kuongeza ufanisi na tija kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile inaisisitiza Serikali iharakishe mchakato wa kuboresha Mifuko ya Mikopo katika Serikali za Mitaa iliyopo kwenye Halmashauri mbalimbali kwa kuwa utendaji wa mifuko hiyo kwa sasa hauna usimamizi madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marejesho ya fedha yanayokatwa kwenye mishahara ya Waheshimiwa Wabunge yanatumika kuwekezwa kwenye dhamana za muda mfupi kwa lengo la kupata faida. Hii itasaidia kupunguza pengo la kiasi ambacho hakitarejeshwa kwa Waheshimiwa Wabunge kutokana na msamaha uliotolewa na Serikali wa asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ndiye mkopeshaji, fedha hizi hazina riba. Mkopaji anahitajika kulipia gharama ya kuhudumia mkopo (*service charge*) asilimia tatu tu pindi anapochukua mikopo ambayo itatumika katika uendeshaji wa Mfuko. Hivyo Kamati yangu inatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wa Serikali kukopa fedha hizi kwa ajili ya vifaa vya nyumbani pamoja na vyombo vya usafiri hasa ikizingatiwa kuwa mikopo hii ni ya masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu umeboreshwa. Mheshimiwa Mbunge sasa anatakiwa akate Bima ya Mkopo ili Serikali iweze kupata fidia iwapo kutatokea majanga ya kushindwa kesi za uchaguzi au kifo. Hapo awali wakati majanga haya yakitokea hapakuwa na utaratibu mzuri wa marejesho ya bakaa ya mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatimaye Kamati imetoa angalizo kwa Serikali kubuni utaratibu endelevu wa kuendesha mifuko hii ikizingatia mabadiliko ya thamani ya fedha, mfumuko wa bei, na kadhalika ili kuepokana na utaratibu wa kuandaa Maazimio haya mara kwa mara kutokana na mabadiliko ya bei husika ya vyombo vya usafiri pamoja na vyombo vya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Abdallah Omari Kigoda, ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa -Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Oseler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Dr. William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amour Amina Abdulla, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Alhaj. Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumshukuru, Mheshimiwa Mustafa Mkullo - Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Gregory Teu - Mheshimiwa Pereira A. Silima, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati - Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.
(*Makofi*)

MWENYEKITI – MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati kwa taarifa hiyo ya Kamati. Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naona anakuja Mheshimiwa Lucy Owenya.

MHE. LUCY F. OWENYA (K.N.Y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu za dhiti kwa kupata fursa hii ya kusimama hapa na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Wizara ya Fedha kuhusu Azimio tajwa kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka Azimio liboreshwe. Azimio linalotamka kwamba Wabunge watapewa msamaha wa asilimia 50 ya mkopo, tunapendekeza lirekebishwe badala yake Serikali ifanye maamuzi ya kuwa Mbunge atapewa mkopo (*loan*) wa asilimia 50 na Serikali itoe ruzuku (*grant*) ya asilimia 50 iliyobaki ili kuwezesha Wabunge kupata vyombo vya usafiri vya kuwawezesha kufanya kazi ya kuutumikia umma kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka Azimio la kuweka mfuko husika chini ya Ofisi ya Bunge liambatane na kuwekwa kwa mfumo thabiti wa usimamizi wa fedha na kuhakisha mahesabu husika yanakaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama sheria na kanuni zinavyohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kwamba kilichotajwa kwenye azimio kuwa ni kuongezwa kwa mtaji katika mfuko husika kutoka shilingi bilioni 14.8 mpaka shilingi bilioni 32.724 siyo kitu kipya kwa sababu katika Mkutano wa Tatu wa Bunge, kikao kimojawapo kilijulishwa kuwa kiasi hicho cha fedha ndicho kitakachotumiwa na Serikali kwa ajili ya mikopo ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani inataka Azimio hilo liboreshwe ili kuingizia maazimio mahususi ya kuboresha Mifumo ya Mikopo wa Serikali za Mitaa ili kuwezesha pia Madiwani na Watumishi wa Serikali za Mitaa, kuweza kupata mikopo kwa wakati ya kuwawezesha kupata vyombo vya usafiri kuwezesha kutumikia umma kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakati wote katika kutenga fedha za Mifuko ya Mikopo ya vyombo vya usafiri kwa viongozi na watumishi wengine wa umma, maamuzi yafanyike na kuhakikisha kwamba vipaumbele vingine vya umma haviathiriki kutokana na fedha kutengwa kwa ajili ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Ahsanteni kwa kunisikiliza na Mungu awabariki.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lucy Owenya kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Naamini kwa kweli Bunge hili linabarikiwa na Mungu kwa sababu tunasali kila siku asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza maoni ya Kambi ya Upinzani na baada ya kupata maoni ya Kamati, kinachofuatia sasa ni mchango wa jumla. Naomba nimwite Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, yeye ndio mchangiaji wa kwanza na atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Hamisi Kigwangala.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuchangia Azimio lililoko mbele yetu ambalo ni Azimio la Bunge la Kurekebisha Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wabunge. Kabla ya kuanza kuchangia ningeomba kwa unyeyekevu mkubwa..., naomba nirudie. “Kwa unyeyekevu mkubwa” na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki, niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuwa Serikali sikivu, kwa kuweza kukubali matakwa na maoni ya wananchi na Watanzania wote ili wapewe nafasi ya kuweza kutoa maoni yao zaidi, waweze kuchangia kwenye Marekebisho ya Katiba, ambacho ni chombo cha Watanzania, kwa hiyo, Serikali ikasikia matakwa ya wananchi. Leo tumesikia hapa Mheshimiwa Spika, akitoa Kauli au Hoja ya Serikali kwamba Serikali imekubali kilio cha wananchi. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa Serikali sikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia. Sisi ni Wabunge wa kuchaguliwa na wananchi. Wananchi wanapotuchagua wanategemea tuwafanyie kazi wanazozitegemea za kuwaletea maendeleo ndani ya Majimbo na ndani ya Taifa hili. Wengine wetu ni Wabunge wa Majimbo, wengine ni Wabunge wa Viti Maalum, wana maeneo. Kwa kweli hawawezi kuikamilisha kazi hii bila ya kuwa na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi Jimbo langu lina Kata 15, Kata 10 ziko kwenye milima mirefu, Kata tano zipo kwenye tambarare kidogo. Wananchi wangu hawategemei niwafikie juu ya milima ile kwa kutembea na miguu, ni lazima wanategemea kama nilivyoomba kura, nizunguke tena niwashukuru, nizunguke tena niwahudumie, nisikilize kero zao na niwafikie wote kwa ujumla wao. Sasa inapofikia hatua hii ya kupata mikopo, ni kweli lazima turidhie Azimio kama hili. Nina uhakika na wananchi wenyewe wanaunga mkono Wabunge wao wakipata vyombo vya kuwafikia kwa sababu, tusipowafikia, ina maana hatutaweza kuwatendea haki na hatutaweza kufanya kazi walizotutuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupitia Azimio hili, ninaomba pia Watanzania wapate ujumbe wangu. Serikali iliposema kwamba sasa Wabunge wanapewa shilingi milioni 90 kulitokea kauli za kupotosha Watanzania kwamba sasa Wabunge wanapewa pesa na Serikali. Naomba Watanzania waelewe kwamba zile shilingi milioni 90 mlizokuwa mnaambiwa, tunapewa na wenzetu ambao wao walijiweka kando kama vile wao hawatachukua, ilikuwa ni mkopo. Serikali inakopesha Wabunge wake ili waweze kuwatumikia wananchi kwa ufanisi. Tulikuwa hatupewi pesa zile kwa kupewa kama ahsante sijui ya kitu gani, tulikuwa tunakopesha na Serikali ili tuweze kuwatumikia

wananchi wetu. Wengine walitoa kauli ambazo zilianza kuwafanya wananchi wasituelewe sisi Wabunge. Naomba wananchi wote, Watanzania wote, wananchi wetu mliotuchagua mwelewe kwamba huu ni mkopo na tunakatwa kwenye mshahara wetu mwisho wa mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiunge mkono Kamati ya Fedha, kifungu cha 2.3, naomba nikinukuu: “*Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza Serikali ihakikishe kuwa inaharakisha mchakato wa kuboresha mifuko ya mikopo katika Serikali za Mitaa iliyopo kwenye Halmashauri mbalimbali.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Fedha imezungumza kitu cha muhimu sana. Sisi Wabunge tunapata mikopo, lakini na sisi Wabunge hatuna uwezo wa kufanya kazi Majimboni peke yetu, tuna Wasaidizi wetu ambao ni Madiwani. Tunaisihi Serikali ya Chama cha Mapinduzi na ninaomba niisihika kabisa ione umuhimu wa kuharakisha mikopo kwenye *Local Government* kwenye Serikali za Mitaa ili na wale Madiwani wenzetu ambao wanatusaidia kufanya kazi ya Watanzania ambao wako karibu na wananchi, ambao sisi Wabunge tunawategemea na wao waweze kupata mahali pa kukopea, waweze kununua vyombo vya usafiri kulingana na uwezo wao. Hili siyo jambo dogo na wala siyo jambo la kupuuzwa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba wakati Mheshimiwa Waziri wakati anatumia, aseme ana mkakati gani katika hili? Kwa sababu tusijione sisi Wabunge ni muhimu peke yetu, lakini kazi ya kutumikia wananchi kwenye Majimbo yetu hatuwezi kuifanya wenyewe bila ya kushirikiana na Madiwani ambao ni viongozi wanaotusaidia sana kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kutenganisha hii mifuko, upo na unaonekana wazi. Kwanza sisi ni Viongozi wa kuchaguliwa na wananchi. Wale wenzetu ni watumishi wa Serikali ambao wameajiriwa, lakini na wao wana umuhimu wao. Lakini ili Serikali iweze kufanya kazi vizuri ni vyema Wabunge tukawa kwetu, watumishi wa Serikali upande wao, na utakapokuja mfuko wa *Local Government* nao uwe umesimama wenyewe.

Kwa heshima na taadhima, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza. Naomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. DR. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kikubwa kilichonisukuma mimi leo hii kutoa mchango wangu ni haswa suala zima la upotoshaji wa mikopo ya vyombo vya usafiri kwa Waheshimiwa Wabunge. Bahati mbaya ningeweza kusema, mwenzangu amenifilisi kwa mchango wake, lakini naomba na mimi niendeleo ku-*cement* palepale ambapo mwenzangu ameongelea, kwa maana kubwa ya kwamba Waheshimiwa Wabunge, tuna *jurisdiction* kubwa sana ya kuwafikia wananchi wetu ambao ndio wapigakura wetu ambao ndio waajiri wetu; na usipofika huko, wanakasirika kweli kweli. Nilisikitika sana baada ya sisi kupewa mikopo, kusikia kauli mbalimbali za upotoshaji kutoka kwa wenzetu. Mimi nikidhani kwamba pengine

wao hawatakuja kusaini fomu za mikopo kwa sababu labda wao hawahitaji magari kwa ajili ya kuwafikia ndugu zetu wapigakura, lakini bahati mbaya sana fomu zile za kisheria za mikopo zilizokuwa na rangi ya njano, niliwashuhudia wao wakiwa ni wa kwanza kwenda kuzichukua na kuzisaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzisaini hawakuishia pale, waliendelea tu kutoa kauli za kupotosha kwenye vyombo mbalimbali vya habari, wakidai kwamba Wabunge wanapeana pesa. Serikali inawapa pesa Wabunge, mimi nikasema, sasa Wabunge ni akina nani? Ni Wabunge wa CCM peke yake au ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Tunapoongelea Mbunge anapewa mkopo wa usafiri, ni kitu gani kipya na cha ajabu hapo? Kwa sababu, pengine mimi ningetegemea labda Wabunge na wao wangepata tu magari ya Serikali, ya Ofisi ya Bunge yakawepo pale tayari kwa ajili ya kuwasaidia kufanya shughuli zao. Lakini leo hii tunapewa mkopo ambao unakatwa katika mishahara yetu, mtu bado analalamika! Vipi ingekuwa tunapewa vyombo vya usafiri, tunapewa ofisi ipo tayari na vyombo vya usafiri na kila kitu, wewe ukichaguliwa kuwa Mbunge unaingia kwenye gari unanza kufanya kazi? Ingekuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unapewa gari na bado unakatwa kwenye mishahara wako, maana yake ni kwamba kila mwezi unasikilizia maumivu ya kukatwa pesa kwenye mishahara wako. Lakini kwa sababu za kisiasa na kwa utamaduni mpya ambao unajengeka katika Taifa letu ambapo watu wengine wamekuwa na tabia ya kupotosha wengine na ya kulalamika kwa lengo la kupata umaarufu wa kisiasa, basi kauli mbalimbali za kupotosha zimekuwa zikiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana na endapo tutaendelea namna hii kama Taifa hatuwezi kufikia mustakabali mwema wa maendeleo ya kiuchumi na kiuongozi katika nchi yetu. Ningependa nitumie fursa hii kutoa ushauri kwa wenzetu, waache kauli za kuwapotosha Watanzania waongee mambo ya haki, palipo na haki wasimame kwenye ukweli mahali palipo na ukweli na sio kupotosha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba niungane na mchangiaji aliyepita kwa kusema kwamba ifike mahali sasa Serikali itoe tamko na ifanye maamuzi ya kuangalia ni jinsi gani itawawezesha Waheshimiwa Madiwani nao wapate mikopo ya vyombo vya usafiri na mikopo mingine mbalimbali. Kwa sababu kimsingi ni kweli wanasikitika sana na wanalalamika pengine labda hawana mahali kwa kusemea, pengine hawana mahali pa kulalamikia lakini leo hii naomba niwe sauti ya Madiwani, nao pia niwaombe mchakato wa kuwapa mikopo ya vyombo vya usafiri ufanyike haraka ili nao waweze kuwafikia wananchi kwa uharaka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja ni juzi mimi niko Bungeni naendelea kuhudhuria kikao cha Bunge, huko Jimboni kumetokea mtafaruku TRA wamevamia biashara wamefunga, wanamtafuta Mbunge wao nani, niko Bungeni sipatikani, lakini Mheshimiwa Diwani aliwahi kufika eneo la tukio akawahi kusuluhisha huo mgogoro. Hii inaonyesha ni jinsi gani Mbunge anafanya kazi karibu zaidi na wananchi kwa kupitia Mheshimiwa Diwani. Hivyo nadhani siyo suala la busara kuwaacha Madiwani wetu

wakihangaika wakiwa hawana vyombo vya usafiri na maisha yao yakiendelea kuwa duni siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda wako, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuchangia Azimio hili. Kwanza kabisa, kabla sijaingia kwenye hoja yenyewe nichukue nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili, niwashukuru sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Spika pamoja na Wabunge wote wa Bunge hili pamoja na Watanzania wote kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa jinsi ambavyo walituunga mkono na kutufariji kwa hali na mali wakati tumepata ajali ya mabomu katika Jimbo letu la Ukonga. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia katika sehemu mbili kwenye maazimio haya, kwanza niungane na Wasemaji wawili ambao wamepita kwa jinsi ambavyo wamechangia vizuri hii hoja na kufafanua vizuri hii hoja ya kupewa mkopo wa magari kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tulifedheheka vya kutosha Wabunge kwa sababu ya kupotoshwa kwa kupatiwa mikopo ya magari kwa Wabunge. Namshukuru Mheshimiwa Anna Killango, amefafanua vizuri kwamba ile ni mikopo ambayo tunakatwa kwenye mishahara yetu. Lakini hata hivyo ameeleza vizuri umuhimu wake kwamba ni vyombo ambavyo vinatuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi katika shughuli za kila siku tukishirikiana na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia katika jambo hilo, mimi nije tena kuchangia kwenye kile kipengele ambacho wana Kamati wamesema kwamba Serikali ihakikishe kwamba inaharakisha ili mikopo hii iweze kuwafikia katika ngazi za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nishuke chini zaidi ikiwezekana hata baada ya Madiwani kupata fedha hizo, basi ziweze kushuka mpaka chini kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Wenyeviti wa Serikali za Mitaa pia na wao ni Watendaji wazuri ndiyo wanaokaa Mtaani pamoja na wananchi, ndiyo wanaoshughulikia pia kero kubwa sana za wananchi, kwa hiyo, ikiwezekana zishuke mpaka kule hata waweze kupata hata pikipiki zenyewe ili wao pia waweze kuwashughulikia wananchi waliowachagua kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende haraka pia nizungumzie kile kipengele cha 2(6) ambacho kinaeleza kwamba kutakuwepo na utaratibu wa Wabunge waliokopeshwa magari kutakiwa kukata bima ili kuweza kuzinusuru fedha hizo iwapo Mbunge atakufa au labda anaweza akawa ameshindwa kesi iliyomfanya mpaka akaingia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na ombi au wazo kwamba ikiwezekana Serikali iangalie utaratibu mwingine kwa sababu fedha hizi tunazopewa tunatumia kununulia vifaa. Kwa hiyo, kama tunaendelea kukatwa kwa sababu hatukwenda kuzifanyia biashara, basi kuna uwezekano mkubwa sana Mbunge akawa anaendelea kuumia kwa sababu wengine mpaka sasa hivi kama tumechukua mikopo yote, basi hata kukatwa ni kwamba tunabakia na kiwango kidogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa na wazo kwamba uangaliwe utaratibu mwingine ambao unaweza ukaiweka mikopo hii katika *security* nzuri badala ya kuendelea Mbunge kulundukiwa mzigo huo wa kuendelea kukatwa bima kwa ajili ya mkopo wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi nami niweze kuchangia Azimio hili. Kimsingi napenda sana kuipongeza Serikali kwa majukumu makubwa ambayo yanaikabili, lakini wakati huo huo kutufikiria sisi Wabunge ili tuweze kutimiza wajibu wetu ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu ambao wamesema kwamba Azimio hili limefika kwa wakati muafaka na katika Azimio hili niseme kwamba mawazo ambayo yametolewa na Kamati ya Fedha, lakini pia yaliyochangiwa na Kambi ya Upinzani kwamba huduma hii sasa iteremke mpaka kwenye Serikali zetu za Mitaa kiasi kwamba pia Waheshimiwa Madiwani na ikiwezekana Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wapewe huduma hii ni muhimu sana jambo hili likaangaliwa kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona nafasi hii inasaidia pia kwetu kutoa ufafanuzi kwa wananchi kuhusiana na taarifa mbalimbali au mawazo ambayo mara nyingi wanakuwa wanayo. Nimekuwa nikisikia wananchi wakihoji kwa nini wananunua magari ya bei mbaya sana kama *ma-Land Cruiser* badala ya kuchukua kama Suzuki, zikaweza kusaidia ili mradi amepata chombo. Niseme tu kwamba ndugu zetu mnaotusikiliza kwa kweli jiografia ya nchi yetu ni kubwa sana. Nichukulie mimi Stella Manyanya Mbunge wa Mkoa wa Ruvuma ambaye pia sitoki Ruvuma - Songea Mjini, natoka kule Kijijini Kinagara. Kutoka Dodoma mpaka Songea nazungumzia kilomita takribani 1100. Nikienda Mbinga Mbambabay mpaka Kinagara unaongeza tena kilomita 250. Kwa hiyo, unazungumzia karibu kilomita 1400 na wakati huo huo kwa mwaka kwa safari zangu za halali inabidi niende siyo chini ya mara nane, ukizungumzia kwenda na kurudi ukiacha safari ambazo ni za papo kwa hapo zinazoweza kujitokeza kuna dharura niende na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliwahi kuwa mtukutu kipindi kilichopita nikasema sitaki kununua *Land Cruiser* kubwa, nikijiangalia umbo langu mdogo mdogo, nikasema nataka na gari yangu iwe ndogo, ninunue *Harrier*. Lakini matatizo niliyokuwa nayapata ninapokwenda Vijijini ni makubwa. Unakuta njia zetu nyingine hazipitiki kirahisi, unakwenda na *Harrier* inakuwa imekaa chini kwenye tope huwezi kwenda. Wananchi wanakusubiri uende ukafanye Mkutano wamekaa mpaka saa 8.00 mchana,

hujatokea wanasema huyu Mbunge hana adabu, hawajibiki ipasavyo, unawakosa wananchi wanakuwa wamechukia.

Kwa hiyo, sio hivyo tu, hata kwa afya zetu unapokuwa na gari ambayo haiwezi kuhimili kwa muda mrefu na ikiwa ni gari ambayo haikupi fursa ya kukaa vizuri kwa safari ambazo unazitumia mara kwa mara, kwa kweli pia ni hatari kwa afya zetu sisi wenzenu. Kwa hiyo, naomba wananchi mtuelewe katika hilo na kwa yeyote atakayebahatika kuwa Mbunge kwa sababu tunapokezana, naamini na yeye atayaona hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ambayo nimesema tu ,nitoe ufafanuzi huu, niseme tu kwamba sisi wote ni kitu kimoja, ni vyema pale inapotokea mambo ya msingi tukawa wote kitu kimoja. Lakini kubwa zaidi nililofurahi ni hili la kutenganisha mifuko, kwa sababu inapofikia Wabunge wapewe sasa mikopo ya magari unakuta hela zote zinakombwa kwenye Mfuko na Wafanyakazi wenzetu, watumishi wanakuwa hawana pesa za kufanyia shughuli zao kwa wakati huo. Kwa hiyo, tunakuwa tunachanganya matumizi. Ni vyema kwa kweli kama Serikali ambavyo imeona itutenganishe ili kila watu wapewe mahitaji kutegemeana na hali inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nitakuwa siyo mwingi wa fadhila kama sitalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kunirejesha tena mimi kuwa katika Bunge la SADC ambalo halijawa Bunge kamili bado liko kwenye *transformantion*, tunategemea kuna siku litakuwa Bunge kamili kwa kuniamini na hivyo kunirejesha katika Kiti cha uenyekiti ambacho nilikuwa nakihudumia kule katika Bunge la SADC. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge lile inayohusika na Utawala Bora, Demokrasia na Jinsia. Naamini Wabunge wenzangu walikuwa wananiombea na walikuwa wananihitaji, kwa hiyo, nitaendelea kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kung'ara katika nchi za Jumuiya za Afrika ya Kusini, lakini hali kadhalika kuendeleza tabia njema ya Tanzania pamoja na mshikamano amani na uhuru wa mawazo ambao tunao. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. DR. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mada hii iliyo mbele yetu. Azimio hili la Serikali ni zuri, nianze kwa kusema naliunga mkono. Lakini kama walivyotangulia kusema Wasemaji wawili watatu, suala hili la maslahi ya viongozi wachaguliwa linapata msisitizo sana katika nafasi hii ya Ubunge, wenzetu watumishi wa kuchaguliwa (Madiwani) wameachwa achwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita, Bunge la Tisa tulikuwa tunafuatilia sisi ambao tulikuwa nje ya hilo Bunge, mara kadhaa yaliletwa maombi ndani ya Bunge kwamba Waheshimiwa Madiwani nao sasa waanze kulipwa mishahara. Majibu yaliyotolewa na Serikali nadhani yanafahamika, kwamba muda bado, jambo hili linaangaliwa na hivi na hivi.

Kwa hiyo, wenzetu hawa wanaendelea kufanya kazi kwa kweli katika mazingira ambayo hayaridhishi sana na kwa hiyo, ufanisi wa usimamizi wa shughuli za

Halmashauri unakuwa unapungua kwa sababu maslahi yao hayawekwi vizuri kama inavyostahili. Leo tunajadili mfuko huu uboreshwe uweze kuwahudumia Wabunge na watumishi wa Serikali Kuu vizuri, lakini naamini ingependeza sana kama sambamba na hili tungekuwa tunajadili na namna ya kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, simwoni Mbunge yeyote humu wa Jimbo atakayefanya kazi vizuri *effectively* kwenye Jimbo lake bila kuwahusisha Madiwani. Madiwani wanaachwa wakabane na Mkurugenzi wa Halmashauri kupata mikopo, tunaona wanahangaika, wanakopeshwa baadhi na nini, lakini ni mikopo kutoka kwenye Halmashauri ambazo kimsingi hazina fedha ya kutosha. Hizi *covers* zote tunazowekewa Wabunge wao hawawekewi, Madiwani wanakopa lakini hakuna bima kama Halmashauri imekubali kuwakopesha. Hakuna bima! Akitokea kupatwa na tatizo asiendelee na Udiwani, kale kananii kake ka mwisho kanakoma, tofauti na ilivyowekwa katika huu Mfuko wa Bunge. Mimi niombe sana, yawezekana isiwe leo, lakini kwa kweli Serikali iangalie utaratibu kuhakikisha kwamba na wenzetu hawa wachaguliwa na wao wapate nafuu za namna hii kuwafanya waweze kutekeleza wajibu wao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine katika mfuko huu fedha, hii *advance* imegawanywa kwenye sehemu mbili. Moja, kuwahudumia Wabunge, lakini na kuwahudumia watumishi wa Serikali Kuu. Nimekuwepo Serikalini muda mrefu, fedha hii inayotengwa kwa ajili ya watumishi wa Serikali Kuu ni ndogo sana. Kwa hiyo, niombe kwanza mfuko huo upande ule wa Watumishi wa Serikali Kuu uongezwe ili uweze kuwafikia watumishi wa kada zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiuliza Serikali itoe takwimu ni watumishi wa ngazi gani wamewahi kunufaika na mfuko huu, utasikitika. Utakuta ni Wakurugenzi, Makatibu Wakuu, katika Wizara basi. Lakini kwanini usitafute utaratibu na ukawekwa wazi katika sheria au kanuni ambao utawezesha hata watumishi wa kada za chini kabisa kuweza kupata mikopo hii na wao wana mahitaji kama watumishi wengine ambao wako ngazi za juu?

Niombe sana wakati Waziri anafunga mjadala, basi angalau aseme ni utaratibu gani wa makusudi kabisa utawekwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba watumishi wa kada za chini chini na wao waweze kunufaika na mfuko huu. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Dr. Tizeba.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio hili. Mfuko huu unaimarishwa na zaidi ya hapo Madiwani nao wapewe mikopo. Serikali pia iimarisha utaratibu wa kukusanya madeni ili uendelee kuimarika.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yetu Tukufu kwa kuleta Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa magari wanayokopeshwa Wabunge ni magari ya kazi sawasawa na magari yanayotumika katika Halmashauri zetu, nadhani Serikali ichukue jukumu la kuweka bima kwa magari hayo kwani magari hayo huwa ya mikopo mpaka deni litakapomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani ni wafuatiliaji walio karibu zaidi na wananchi katika kutekeleza Ilani ya Serikali ya Chama Tawala. Nashauri bajeti ijayo ya Serikali wafikiriwe kupata mikopo ya vyombo vya usafiri ili kuwawezesha kufuatilia miradi ya maendelo kwa urahisi zaidi. Pamoja na mikopo hiyo, wafikiriwe kuongezwa maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niunge mkono hoja ya kusaidia mikopo kwa Halmashauri zetu kwa ajili ya Madiwani, ni jambo la muhimu sana kwani Kata nyingi ziko mbali sana na maeneo ya kazi. Jimbo langu ziko Kata 19, kwa hiyo, nasisitiza ufanyike haraka mpango huu.

MHE. DR. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6 cha Azimio hili kiondolewe na badala yake Serikali itafute utaratibu mwingine wa kuweka dhamana, kwa sababu kipengele hiki kitaleta *bureaucracy* na *some degree of uncertainty* kwa Waheshimiwa Wabunge.

MHE. AMINA A. CLEMENT: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mfuko huu kwa kuwa ni muhimu sana kwa vile Mbunge anatakiwa awe anatembelea mara kwa mara Jimbo lake pia linawasaidia wananchi wakati wakiwa na shida zao za ugonjwa au harusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo huo unatakiwa utolewe haraka sana, baada ya Mbunge kuapishwa apatiwe ili aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Pia Serikali ifikirie tena makato ya mkopo wakate robo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI O. JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Pili, mchango unaanza kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili la kutenganisha mfuko huu wa mkopo kwa Wabunge ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na wale watendaji wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi walioko chini ukiacha Wabunge ni Madiwani, naiomba Serikali basi iharakishe mchakato wa kuhakikisha kwamba Madiwani nao wanafaidika na mikopo hii kwani nao wana kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siko mbali na maoni ya Kamati kwamba kuwepo kwa Mfuko huu chini ya Ofisi ya Bunge kutasaidia Waheshimiwa Wabunge kufuatilia mikopo yao kwa karibu na kuepuka usumbufu unaotokea hivi sasa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napingana na kipengele cha 2.6 cha maoni ya Kamati kwamba Waheshimiwa Wabunge wakate bima ya mikopo hiyo. Naiomba Serikali iandae utaratibu mwingine kwani Waheshimiwa Wabunge tutawekwa katika mazingira magumu zaidi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi nilizotoa zile za nyongeza nadhani zinatutosha kwa kuwa hoja hii inatupasa tuihitimisha kipindi hiki hiki cha asubuhi ili jioni tuingie kwenye hoja nyingine tena nayo kama itakuwa imeshakamilika iweze kuwekwa Mezani. Kwa hiyo, sasa naomba nimwite moja kwa moja Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kuendelea na utaratibu wa kuhitimisha hoja ili tuweze kukamilisha taratibu nzima. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sija-respond hoja za Waheshimiwa Wabunge ningeomba kwa fursa hii nitumie nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuwa hapa nilipo hivi sasa.

Vilevile nichukue fursa hii kuwakumbuka wananchi wa Jimbo langu la Mpwapwa kwa ridhaa ambayo walinipa kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni na kufanya kazi ya umma kama navyoendelea kufanya hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua nafasi hii kuishukuru sana Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Mahesabu ya Serikali inayongozwa na CAG kwa kunilea muda wote na kunipa moyo hata kuingia Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa kazi yao wanayoifanya kwamba ni kubwa na nzuri na sisi tunaiona na hivi juzi tu walileta hesabu zao hapa na tunatambua kwamba kazi uliyonayo ni kubwa, kwa hiyo, naomba Serikali iwatambue ofisi hiyo na endapo ni vema basi tuwawezeshe ili waweze kuendelea kufanya kazi hiyo nzuri kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa kazi hii ya kuweza kumsaidia katika kuleta maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba niingie kwenye hoja lakini awali ya yote kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kutoa shukurani za

dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Azimio hili kwa kuzungumza na kwa maandishi.

Naomba niwatambue kwa majina Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza kama ifutatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati yake kwa michango yao. Vilevile namtambua Mheshimiwa Lucy F. Owenya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa maoni waliyotoa, namtambua Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Dkt. Hamis A. Kigwangalla, Mheshimiwa Eugene E. Mwaiposa, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya na Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba. *(Makofi)*

Pia waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour kwa pamoja nawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa maoni na ushauri waliotupa na kwa kuunga mkono azimio hili. Aidha, napenda kutoa shukurani zangu kwa Kambi ya Upinzani kwa maoni na ushauri wao na naahidi kwamba Serikali itayafanyia kazi maelekezo na mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Kambi ya Upinzani. Naomba sasa nianze kujibu hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri wachangiaji wote maelekezo yao yamekwenda kwenye mkakati ambao unafanywa katika Halmashauri ili kuweza kuboresha mifuko ya mikopo kwa watumishi wa Halmashauri wakiwemo Madiwani, Wenyeviti na hata Maafisa Watendaji.

Kauli ya Serikali ambayo naweza nikasema ni kwamba, kwa marekebisho ya Sheria ya Fedha, Serikali imetambua umuhimu huo na sasa imeamua kwamba itatoa nafasi au itateua mtu ambaye atajulikana kwa jina la *Assistant Accountant General* ambaye atahusika na *Local Government*. Kwa hiyo, tunamtegemea huyu ambaye atateuliwa na Mheshimiwa Rais na atafanya kazi chini ya Mhasibu Mkuu wa Serikali atasimamia vizuri Mfuko huu wa Halmashauri na kutoa miongozo mizuri ya Halmashauri na kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuwakopesha wafanyakazi wa Halmashauri wakiwemo Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na hata Maafisa Watendaji. Kwa hiyo, huyu kiongozi ambaye atapewa wadhifa huu wa kumsaidia *Accountant General* wa Serikali Kuu na yeye atashughulika *specifically* kwa Halmashauri tu, tunategemea ataboresha hili kwa kiwango kitakachoridhisha na malalamiko yenu Waheshimiwa Wabunge ambayo mmeonyesha yatatatuliwa kwa njia hiyo. *(Makofi)*

Lingine ambalo amechangia mjumbe wa Kambi ya Upinzani ni kwamba Sheria ya Mfuko wa Bunge chini ya Ofisi ya Bunge ukaguliwe na *CAG* ili aweze kusimamia vizuri, ni lazima kuwepo na udhibiti. Nimesema kwamba kauli ya Serikali ni kuwa,

Mfuko huu umeanzishwa chini ya *Public Finance Act* ya 2011, Sura ya 12 na utakaguliwa na CAG chini ya Sheria hiyo ambapo pia hesabu za Halmashauri zitakaguliwa na CAG, ni kweli chini ya Sheria hii ambayo nimeitaja hapa na mwongozo ndivyo ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo ambayo kwa kweli kama nilivyosema ni kwamba wachangiaji wengi mawazo yao yamefanana na wengi wamechangia kwamba mikopo katika Halmashauri iboreshwe zaidi. Kama nilivyosema Serikali imeshaliangalia hilo kwa kumteua mtu ambaye atashughulikia hayo na wengi wametoa msisitizo kwamba mikopo hii ambayo Wabunge wamepewa wananchi wajue kwamba ni mikopo ambayo imetolewa na Serikali na wala siyo vinginevyo. Wananchi waelewe kwamba mikopo hii inarejeshwa. Wabunge wengi wamesisitiza hilo na mimi nazidi kusesitiza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*
WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja Ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Bunge la Kurekebisha Mfuko wa Kutoa Mikopo (Advances Fund) kwa Wabunge na Kuunda Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Serikali Kuu liliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na imepitishwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri, basi tunaomba utekelezaji wake uanze kwa kufuata utaratibu ili hiki kilichopitishwa leo kiweze kuwanufaisha kweli watumishi wengine wa Serikali, lakini na Waheshimiwa Wabunge kwa nyakati tofauti kwa kadri Bunge letu litakavyokuwa linadumu katika nchi yetu ya Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitisha hoja hiyo, naomba kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Mheshimiwa Spika nitoe matokeo ya uchaguzi tulioufanya leo asubuhi.

MATOKEO YA UCHAGUZI

MWENYEKITI: Kura zilizopigwa hapa ndani kwa ajili ya kumchagua mwakilishi wa Bunge la SADC kwa nafasi za wanaume kutoka Chama Tawala zilikuwa 236, kura zilizoharibika zilikuwa ni nne na matokeo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Faustine Ndungulile amepata kura 72 na alikuwa mshindi wa tatu, Mheshimiwa Seleman Said Jafo amepata 73 na alikuwa mshindi wa pili na Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani amepata kura 87 na amekuwa mshindi wa kwanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima ya Bunge hili, naomba sasa kumtangaza Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani kuwa ni mwakilishi wetu kupitia Kambi ya Chama Tawala kwenye Bunge la *SADC* na kuanzia sasa anaweza kuanza kujipanga na masanduku kuelekea kwenye vikao vya Bunge la *SADC*. (*Makofi*)

Hayo ndiyo matokeo ya uchaguzi na yamesainiwa na kuidhinishwa na wale waliokwenda kusimamia kura katika chumba cha kuhesabu kura.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa tangazo lingine kwamba Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla niwatangazie Wabunge kwamba kesho kutakuwa na mechi ya mpira wa miguu na mpira wa pete kati ya timu ya Bunge na wenzetu wa *LAPF* na mechi hiyo itafanyika saa 10.00 jioni katika uwanja wa *Jamhuri Stadium* hapa Dodoma.

Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* ameendelea kuomba Wabunge wote kujitokeza kwa wingi ili kwenda kuishangilia timu ya Bunge na kuitia moyo ili iweze kushinda kwa kishindo kwenye mechi dhidi ya wapinzani wao.

Lakini ameomba sana ile Kamati ya ufundi inayoongozwa na Prof. Stephen N. Majimarefu iendelee kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha timu hizo zinapata ushindi wa kishindo. (*Makofi*)

Kesho baada ya shughuli ya mechi hiyo, Mheshimiwa Spika kwa kushirikiana na wadau wengine ameandaa tafrija kwa ajili ya Wabunge wote na itafanyika jioni katika viwanja vyetu vya Bunge na utaratibu rasmi mtaelezwa. Kwa hiyo, baada ya kushinda kwa kishindo huko *Jamhuri Stadium* basi tutakuwa na nafasi ya kupongezana jioni hapa hapa yaani tutakuwa na *dinner and dance* katika viwanja vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyopata. Kwa hiyo, kwa kuwa shughuli ambayo tuliipanga kwa kipindi cha asubuhi imekamilika, basi naomba nitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.30 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama wa Mwaka 2011 [*The Judiciary Administration Bill, 2011*]

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye

kupitisha Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama wa mwaka 2011 yaani, *The Judiciary Administration Act, 2011*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuelezea vifungu vya sheria inayopendekezwa, napenda kuchukua fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwa Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa katika kipindi cha hivi karibuni tangu kumalizika kwa Mkutano wa Pili wa Bunge lako Tukufu, hususan wakazi wa Gongo la Mboto na viunga vyake ambao walipoteza ndugu zao na mali nyingi kuharibiwa kufuatia milipuko ya mabomu iliyotokea katika Kambi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi iliyopo Gongo la Mboto, Dar es Salaam. Aidha, natoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu wasanii wa kikundi cha muziki wa Taarabu cha *Five Star Modern* Taarab waliopata ajali tarehe 21 Machi, 2011. Mwenyezi Mungu awarehemu wote waliopoteza maisha yao katika matukio hayo na kuwapa moyo wa subira na matumaini ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kutumia fursa hii pia kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema kwa ushauri wake mzuri ambao umefanya kazi yangu kuwa nyepesi. Nawashukuru pia Waandishi wa Sheria na Watumishi wengine wa Wizara yangu kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa maandalizi ya Muswada huu. Kwa moyo mkunjufu kabisa, napenda kumshukuru Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Mohamed Othman Chande, Jaji Kiongozi Mheshimiwa Fakihi Jundu na Majaji wote kwa michango yao mizuri waliyoitoa katika kuboresha Muswada huu. Niseme tu kuwa michango yao tumeipokea na kuifanyia kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu angalau kidogo kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Ulanga Mashariki kwa kunipitisha bila kupingwa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kunirudisha tena kwenye Baraza la Mawaziri na kunitewa katika nafasi hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Nina uhakika kwamba nitaweka historia katika nafasi yangu hii kwamba ni mmojawapo wa watu walioanzisha mchakato wa Katiba mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako pia naomba kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa George Simbachawene na Kamati yake kwa ushauri na mapendekezo mazuri ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha maudhui ya Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililotolewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa mujibu wa mgawanyo wa mamlaka ya nchi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mujibu wa Ibara ya 4(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Sura ya 2), Mahakama ndiyo chombo kilichopewa jukumu la utoaji haki nchini kwa uhuru na bila kuingiliwa na chombo chochote, kwa azma ya kuenzi dhana ya uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya utekelezaji wa dhana hiyo, Bunge lilitunga Sheria ya Utumishi wa Mahakama ya Mwaka 1962 ambayo ilifutwa kwa Sheria ya Utumishi wa Mahakama ya 2005 ambayo kwa sasa, imeonekana kuwa na upungufu unaosababisha utekelezaji wa Sheria hiyo kuwa mgumu. Muswada huu unakusudia kuweka namna bora ya utekelezaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977, kuhusu uhuru wa uendeshaji wa Mahakama kwa kuanzisha Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama (*Chief Court Administrator*); Msajili Mkuu (*Chief Registrar*); kuinisha Mfumo wa Utumishi wa Mahakama na Uanzishaji wa Mfuko wa Mahakama (*Judiciary Fund*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, Muswada huu unapendekeza kuboresha shughuli za Mahakama kwa kuweka masharti yatakayowezesha kada ya Maafisa wa Mahakama kutoshughulikia masuala ya utawala. Badala yake shughuli hizo za utawala zitatekelezwa na wataalam wa masuala ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na:-

(a) Kuanzisha mfumo wa Utumishi wa Mahakama unaojitegemea kwa kuanzisha Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli zote za utawala pamoja na usimamizi wa fedha za Mahakama;

(b) Kuinisha utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(c) Kuanzisha Mfuko wa Mahakama utakaosimamiwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kuboresha dhana ya uhuru wa Mahakama;

(d) Kuweka utaratibu utakaoiwezesha Mahakama kuandaa na kuidhinisha Mpango wa Muda wa Kati wa bajeti ya Mahakama kwa kila mwaka wa Fedha;

(e) Kuweka masharti yatakayoweka bayana Mamlaka ya Ajira na Udhibiti wa Nidhamu kwa watumishi wasio maafisa wa Mahakama chini ya Tume; na

(f) Kuweka mfumo wa kitaasisi utakaosimamia masuala ya ajira, nidhamu na rufaa za watumishi kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa. Sehemu ya Kwanza inahusu masuala ya utangulizi, ambayo yanajumuisha jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi ya Sheria inayopendekezwa na tafsiri ya baadhi ya istilahi na maneno yaliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili, inapendekeza kuweka masharti yanayohusu uendeshaji na usimamizi wa Mahakama. Sehemu hii inaainisha masharti yanayomhusu Mtendaji Mkuu wa Mahakama, mamlaka yake na kazi zake, uteuzi wa baadhi ya watumishi wa

Mahakama na uhamisho wa wafanyakazi wengine ambao si Maafisa Mahakama ambao ajira zao zilikuwa chini ya Utumishi wa Umma kujiunga na Utumishi wa Mahakama. Sehemu hii inaainisha mamlaka za nidhamu za Maafisa wa Mahakama na ambao si wa Mahakama. Pia inaainisha masharti yanayohusu Tume ya Utumishi wa Mahakama, wajumbe wake, Katibu wake na wafanyakazi wa Tume. Pamoja na hayo, inaweka masharti yanayohusu nafasi ya mawasiliano ya Tume na kinga kwa wajumbe wa Tume.

Sehemu ya tatu, inaweka masharti ya Ofisi ya Jaji Mkuu, Msajili Mkuu na Wasajili wengine. Inaainisha mamlaka na kazi za Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Msajili Mkuu na Wasajili wengine. Aidha, Ibara hii inaweka masharti yanayohusu maelekezo yanayoweza kutolewa na Jaji Mkuu kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yanayohusu Tume ya Utumishi wa Mahakama yanawekewa masharti katika sehemu ya nne. Sehemu hii inabainisha kazi za Tume kama zilivyoainishwa katika Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na masharti ya kukasimu baadhi ya kazi zake pamoja na mamlaka ya kufukuza kazi kwa manufaa ya umma yanayozungumziwa katika Ibara ya 35. Katika Sehemu hii, Tume imepewa mamlaka ya kupitia masharti ya utumishi pamoja na kupitia mishahara na posho mbalimbali za watumishi kama yanavyoainishwa katika Ibara ya 32.

Sehemu ya tano, inapendekeza masharti yanayohusu uanzishaji wa Kamati za nidhamu. Masuala ya uanzishaji wa Kamati ya Maadili ya Majaji, Kamati ya Maadili ya Maafisa Mahakama, Kamati ya Maadili ya Mahakama ya Mkoa, Kamati ya Maadili ya Mahakama ya Wilaya, kazi za kamati hizo, mamlaka, mikutano na taratibu za kazi za Kamati hizo yanazungumziwa kwa undani katika sehemu hii. Sehemu hii inatoa pia maelekezo ya jinsi ya kuwasilisha malalamiko na taratibu zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kutoa malalamiko na jinsi Tume au Kamati zitakavyoanzishwa chini ya Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya sita, inahusu masharti ya masuala ya fedha. Sehemu hii inaweka masharti yanayohusu uanzishaji na usimamizi wa Mfuko wa Mahakama, kuainisha vyanzo vyake vya mapato, hesabu na ukaguzi wa hesabu hizo. Sehemu hii pia inaainisha taratibu za kuanzisha, kutayarisha na kuwasilisha bajeti na makisio ya bajeti kwenye Bunge.

Sehemu ya Saba, inapendekeza masharti ya jumla yanayojumuisha makosa mbalimbali yanayoweza kufanywa katika Sheria inayopendekezwa pamoja na adhabu zake. Sehemu hii inatoa makatazo ya jumla kwa afisa yeyote wa Tume au Kamati kuhusu utoaji wa taarifa yoyote ya Tume au Kamati.

Sehemu ya nane, ina masharti ya jumla yanayohusu majukumu ya Mtendaji Mkuu chini ya Sheria hii inayopendekezwa. Sheria hii pia inaipa Tume mamlaka ya kutunga Kanuni na mwisho inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Utumishi wa Mahakama (Sura 237) pamoja na kuainisha masharti ya mpito.

Sehemu ya tisa, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha (6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma (Sura 298) kwa lengo la kumtambua Mtendaji Mkuu wa Mahakama ndani ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, kwa ridhaa yako naomba kuliomba Bunge lako Tukufu kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua mbili yaani Kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa Mara ya Tatu. Ni imani yangu kuwa Bunge lako litaridhia Muswada huu ili uwe Sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada huu ama mwakilishi wake ili aweze kutoa maoni ya Kamati. Namwona Mheshimiwa Boniface Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua na kutoa maoni ya Muswada huu. Mheshimiwa Simbachawene tafadhali.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE – MWENYEKITI WA KAMATI YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na nguvu za kuweza kulitumikia Bunge hili, wananchi waliotuchagua na Taifa letu kwa ujumla.

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuuleta kwenye Kamati yangu Muswada huu muhimu katika eneo la misingi la utoaji haki. Ni dhahiri uliamini kuwa Kamati hii inaweza kuuchambua kwa umakini na kisha kutoa maoni yake yatakayosaidia kuboresha Sheria inayopendekezwa kutungwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba nitoe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama wa Mwaka 2011(*The Judiciary Administration Bill, 2011*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), tarehe 6 Aprili, 2011 Kamati ilikutana na Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema na wataalam wengine wa Wizara ili kupata maelezo ya awali kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilialika wadau mbalimbali ili kuweza

kufika na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi. Wadau walipata fursa ya kusikilizwa na Kamati siku ya Jumatatu tarehe 11 Aprili, 2011 pamoja na kutoa maoni yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho, ambacho pia Mtoa Hoja alihudhuria, Kamati ilielezwa kuwa, Muswada huu unapendekezwa ili, pamoja na madhumuni mengine, kufuta Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Sura ya 237 iliyokuwa ikitumika hapo awali, ambayo imeonekana kuwa na upungufu na pia utekelezaji wake kuwa mgumu. Aidha, Muswada huu unaweka masharti bora ya utekelezaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusiana na Uhuru wa Uendeshaji wa Mahakama kwa kuanzisha Ofisi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama (*Chief Court Administrator*) na Msajili Mkuu (*Chief Registrar*) pamoja na kuainisha mfumo wa Utumishi wa Mahakama na uanzishaji na usimamizi wa Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau waliopata nafasi ya kutoa maoni yao ni pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*Tanzania Women Lawyers Association*) pamoja na Ujumbe wa baadhi ya Waheshimiwa Majaji na Wasajili wa Mahakama Kuu wakiongozwa na Jaji Kiongozi Mheshimiwa Jaji Fakihi Abdallah Rheno Jundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Kamati uliotumika uliwapa fursa ya kuelezea maoni yao na kisha kuyawasilisha kwa maandishi ili yafanyiwe kazi. Napenda nilijulisha Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu huu ni mzuri na unawashirikisha wananchi kwa karibu zaidi katika mchakato wa utungaji wa Sheria na kwa hakika unasaidia sana kuboresha Sheria zinazotungwa na Bunge.

Naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote waliotoa maoni na mapendekezo yao katika kusaidia uboreshaji wa Muswada ulio mbele yetu. Kamati inaheshimu na ilizingatia kwa umakini michango ya wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu utungaji wa sheria ni lazima uzingatie masharti ya Katiba na mahitaji ya kisheria kwa wakati unaokusudiwa. Kamati ilipokuwa ikijadili na kuuchambua Muswada huu ilipenda kujiridhisha kuhusu masuala ya msingi ikiwemo kasoro za kisheria zinazokusudiwa kurekebisha na kuboreshwa pamoja na Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilihoji mambo mbalimbali ya msingi pamoja na kutafakari kwa kina maelezo na mapendekezo ya Serikali pamoja na yale ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayohusu uwezo wa Kamati kufanya marekebisho katika Muswada kwa kumshauri Waziri kufanya mabadiliko, ilitumika ipasavyo na ndio maana mtoa hoja amewasilisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho. Naomba kusema kuwa kwa sehemu kubwa maoni ya Kamati kuhusu ibara mbalimbali yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati imeridhika kuwa, iwapo Bunge litapitisha Muswada huu pamoja na kuzingatia ushauri wa Kamati, litakuwa limeweka

masharti bora ya utekelezaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 na utekelezaji wa dhana ya Uhuru wa Mahakama (*The Independence of The Judiciary*). Aidha, ni imani ya Kamati kuwa Sheria inayopendekezwa itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwa na Mfuko wa Mahakama unaosimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Kamati cha tarehe 13 Aprili, 2011 Kamati ilikuwa na mjadala wa kina kuhusu maoni ya baadhi ya wadau na wajumbe waliokuwa na mtazamo wa kuweka kiwango cha asilimia ya Pato la Taifa (*Gross Domestic Product*) kama kanuni ya kuupa fedha Mfuko wa Mahakama unaopendekezwa kuanzishwa. Maoni haya yalikuja kama sehemu ya uchambuzi wa Ibara ya 52(2) inayohusu Hazina kutoa fedha kwa ajili ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ilithamini maoni hayo na kuona umuhimu wake katika kufanikisha mantiki, shabaha na sababu za kupendekezwa kwa sheria hii. Hata hivyo, jambo lolote bora linapaswa kutolewa uamuzi kwa kuzingatia mambo mbalimbali yanayoambatana nalo kwa ufanisi wake. Ni kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa taarifa kuhusu mwenendo wa Pato la Taifa, mahitaji halisi ya fedha kwa ajili ya Mfuko huu mpya na uwiano wa ukuaji wa mahitaji hayo ikilinganishwa na ukuaji wa Pato la Taifa ni miongoni mwa mambo ya kufanyiwa utafiti kabla ya kuweka kanuni hiyo kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika na wengi, chombo kinachohusika na utoaji wa haki kinapaswa kuonekana kuwa huru ili kiweze kuaminika na wanaohitaji haki kutoka katika chombo hicho. Uhuru huo haupatikani kwa utungaji wa sheria tu bali kuna mambo mengine zaidi ya sheria. Kamati inashauri kuwa, pamoja na utungaji wa sheria mambo yote ya msingi kwa ajili ya uhuru wa uendeshaji wa Mahakama yanapaswa kuzingatiwa ipasavyo ili kuimarisha zaidi misingi ya utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa sheria nyingine, utekelezaji wa sheria inayopendekezwa utategemea kwa kiasi kikubwa kanuni zitakazotungwa chini ya ibara ya 22 ya Muswada huu. Kwa sababu hiyo Kamati inashauri kuwa utungaji wa kanuni hizo uzingatie namna bora ya usimamizi wa Mfuko wa Mahakama bila ya kuathiri utekelezaji wa dhana ya uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Kamati, Mtoa Hoja alikubaliana na Kamati kuhusu marekebisho yaliyopaswa kufanywa kwenye ibara mbalimbali za Muswada huu, lakini bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kufanya marekebisho zaidi katika maeneo yafuatayo:-

Katika ibara ya tatu (*interpretation clause*), katika tafsiri ya neno “*Committee*”, maneno “*Non-Judicial Officers Committee*” yanajirudia hivyo Kamati inashauri yale yanayojirudia yafutwe.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 11, Mapendekezo “G” aya ya (e) yanayojitokeza katika Jedwali la Marekebisho hayajataja kifungu kinachorekebishwa. Hivyo Kamati inashauri kuwa kifungu kinachohusika kitajwe. Aidha, katika ibara ya 14, Jedwali la Marekebisho, ibara ndogo ya (5), yaongezwe maneno “*by inserting sub-*

clause” kabla ya kuanza ibara ndogo ya (5) kuonyesha kuwa ibara ndogo mpya imeongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 16, ibara ndogo (4) katika Jedwali la Marekebisho, Kamati ina maoni kuwa, neno linalopaswa kufutwa katika Muswada ni “*of the Secretariat*” na sio “*of the secretary*” kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 28 ibara ndogo (5), Kamati ina maoni kuwa mapendekezo yaliyomo katika Jedwali la Marekebisho katika aya (d) yaangaliwe na kuandikwa upya ili kuleta maana katika ibara hiyo.

Katika ibara ya 29 (b), kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, kinachopaswa kufutwa ni “*comma*” na sio “*semicolon*” kama aya (c) ya marekebisho hayo inavyosema:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 50 ya Muswada, kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, mapendekezo ni kuwa ibara ndogo za (3) na (4) zifutwe. Kamati inashauri yatajwe mapendekezo yanayopaswa kuwepo baada ya maneno “*and substituting for it the following.*” Aidha, Kamati inashauri ibara ya 51 kwa Mujibu wa Jedwali la Marekebisho, uandishi wa namba za ibara ndogo ndani ya ibara hiyo ziingaliwe na kuandikwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, katika Jedwali la Marekebisho kunaonyesha uwepo wa *Fifth Schedule*, lakini katika Muswada huu hakuna *Fifth Schedule*. Kamati inashauri kuwa, ni vyema masahihisho yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kutuamini na kutupa kazi ya kufanya uchambuzi wa Muswada huu muhimu. Aidha, napenda pia kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndugu George M. Masaju, wataalam wote wa Serikali na wadau wote waliotoa maoni yao, ambao kwa ujumla wao wameisaidia Kamati katika kufanya uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii ambao, bila kuchoka walifanya kazi hii kwa umakini na kwa uvumilivu mkubwa. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mwenyekiti; Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mjumbe; Mheshimiwa Maida Hamadi Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa David Mciwa Mallole, Mjumbe; Mheshimiwa Philipa Geoffrey Mturano, Mjumbe; Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mjumbe;

Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mjumbe na Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mjumbe. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, bila kuwasahau Makatibu Kamati, Ndugu Haika Mtui, Ndugu Yona Kirumbi na Ndugu Athuman Hussein, chini ya uongozi wa Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Simbachawene Mwenyekiti wa kamati kwa kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani nimeona vyema niwataje wale wachangiaji watakaoanza kuchangia mjadala huu kusudi kama hawako katika maeneo haya ya Bunge waweze kujiandaa na kusogea ndani ya Ukumbi wa Bunge wakati mwakilishi wa Kambi ya Upinzani akitoa maoni ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah na Mheshimiwa Kombo K. Kombo ajiandae. Baada ya kutaja Wabunge hao wa mwanzo sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani ili aweze kutoa maoni ya Kambi hiyo.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Utawala wa Mahakama, 2011, (*The Judiciary Administration Act, 2011*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa Bunge una thamani kubwa sana na kwa sababu hiyo Waheshimiwa Wabunge watanisamehe na natumaini Watanzania watanisamehe iwapo nitaendelea kuzungumza kile ambacho nimekileta hapa bila kupoteza muda muhimu wa Bunge kwa kutoa salamu na shukrani na vitu kama hivyo. Hata hivyo, naomba ieleweke kwamba itifaki yote imezingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ya Sheria ya Utawala wa Mahakama, 2011 (*The Judiciary Administration Act, 2011*) umechapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 11 Machi, 2011 na kusomwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muswada huu umeletwa chini ya Hati ya Dharura na kwa mujibu wa kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, unatakiwa kushughulikiwa katika hatua zote tatu katika Mkutano huu wa Bunge. Kabla ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya malengo na maudhui ya Muswada, naomba nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya utaratibu uliotumika kuuleta Muswada huu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutunga sheria kwa kutumia Hati ya Dharura unatambuliwa na Kanuni za Kudumu chini ya kanuni ya 93(3). Utaratibu huu unakubalika pia kama sehemu ya mila na desturi za Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola. Hata hivyo, utaratibu wa kutunga sheria kwa hati ya dharura, kama jina lake linavyoashiria, ni jambo la pekee au lisilofuata kawaida (*exception*) katika utaratibu wa kawaida wa kutunga sheria uliowekwa na Sehemu ya Nane ya Kanuni za Kudumu. Lengo na athari kuu ya matumizi ya hati ya dharura ni kufupisha muda unaotumika katika mchakato wa utungaji wa sheria kwa kudhibiti mijadala Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa kutunga sheria ukifupishwa maana yake ni kwamba Wabunge na wadau mbalimbali hawatapata muda wa kutosha wa kuusoma, kuuchambua, kuuelewa Muswada wa Sheria na kuchangia katika uboreshaji wake. Kwa sababu hizi, utaratibu huu hutumika tu ili kupitisha sheria zinazohitajika wakati wa maafa, vita au dharura nyingine za aina hiyo. Kwa maana nyingine, utaratibu wa kutumia hati ya dharura katika kutunga sheria ni utaratibu usiokuwa wa kidemokrasia lakini ambao unahalalishwa pale kunapokuwepo na dharura ya kweli inayohitaji Bunge litunge sheria haraka ili kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni ya Kambi ya Upinzani tumeelezea kwamba hata katika nchi ambako tumepata hizi mila na desturi za Mabunge utaratibu wa kutunga sheria kwa hati ya dharura huwa unatumika mara chache sana na mwandishi wa kitabu maarufu cha kanuni, mila na desturi za Bunge la Uingereza, *Erskine May's Treatise on the Law, Privileges, Proceedings and Usage of Parliament, 18th Edition, 1971*, ukurasa 553 anatoa mifano ya sheria ambazo zimewahi kutungwa na Bunge la Uingereza kwa kutumia hati ya dharura na anasema kwamba mara ya mwisho Bunge la Uingereza lilitunga sheria kwa kutumia Hati ya Dharura tarehe 1 Septemba, 1939.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao kidogo historia yao kidogo imeanza kuota kutu tarehe 1 Septemba, 1939 ni siku ambayo Vita Kuu ya Pili ya dunia ilianza. Katika Tanzania utaratibu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu hebu endelea na taarifa yako, naomba sana uzingatie maneno yaliyoandikwa kwenye taarifa ya Kamati na sidhani kama hayo unayoyaongeza ya wenye kumbukumbu kutu na nini...

MBUNGE FULANI: Na aache kutukana watu.

MWENYEKITI: Kama yapo kwenye taarifa hii. Kwa hiyo, naomba sana ufuate utaratibu wa kikanuni, hebu zingatia yale yaliyoandikwa katika taarifa na uondoe hayo maneno ambayo hayapo.

MHE. TUNDU A.M. LISSU – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hayo maneno ya kumbukumbu ya kutu Mheshimiwa Mwenyekiti nayaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia utaratibu wa matumizi wa Hati ya Dharura katika Bunge la Tanzania na maoni yangu yako kwenye ukurasa wa tatu wa hii niliyoandika. Nasema kwamba katika nchi yetu ya Tanzania tumetumia matumizi ya Hati ya Dharura kwa namna ambavyo isivyo. Tumetumia Hati ya Dharura kupitisha Miswada ambayo ilikuwa inahitaji mjadala mkubwa. Kwa mfano, Sheria ambazo zimepitishwa na Bunge hili kwa kutumia Hati ya Dharura, Sheria ya Kuweka Watu Kizuizini bila ya kuwapeleka Mahakamani mwaka 1962, Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964, Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973, Katiba tuliyonayo leo ya mwaka 1977, Sheria ya Wahujumu Uchumi ya mwaka 1984 na sheria nyingine iliyotungwa na Bunge hili mwaka jana Sheria ya Gharama za Uchaguzi pamoja na marekebisho yake. Hizi sheria zote zilikuwa muhimu sana lakini zilipitishwa haraka haraka na wana historia wanatuambia kwamba zimekuwa na madhara makubwa nimeyazungumzia kwa kirefu katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa ridhaa yako nizungumzie huu Muswada wa Sheria ya Utawala wa Mahakama. Nianze kwa kuzungumzia kifungu cha (4) cha Muswada kinapendekeza kuundwa kwa ‘Tumishi ya Mahakama’...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, sasa utusaidie uko ukurasa gani?

MHE. TUNDU A.M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa saba, kifungu cha 4 cha (*Judiciary Service*), itakayojumuisha watumishi wa kimahakama na wasiokuwa wa kimahakama. Maneno ‘Tumishi ya Mahakama’ (*Judiciary Service*) hayajatafsiriwa katika Muswada huu. Hata hivyo, neno *Service* (Tumishi) limetafsiriwa na kifungu cha (3) kumaanisha “Tumishi ya Mahakama iliyoanzishwa chini ya Sheria hii.” Aidha, neno Mahakama (*Judiciary*) limetafsiriwa kumaanisha, Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama zilizo chini yake. Kwa hiyo, pamoja na kukosekana kwa tafsiri ya maneno yote mawili, ‘Tumishi ya Mahakama’ inaelekea kumaanisha Tumishi ya Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu na Mahakama zilizo chini yake itakayoanzishwa chini ya Sheria ya Utawala wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tafsiri hii ni sahihi, basi kuna mkanganyiko mkubwa na wa kimsingi unaotokana na mapendekezo ya Muswada huu. Kwanza, Tumishi ya Mahakama kwa maana hii inaonekana kama ni taasisi au chombo kinachojitegemea. Hii ni kwa sababu kila moja ya maneno ‘Tumishi’, Mahakama na Tume lina tafsiri yake tofauti katika kifungu cha tafsiri cha Muswada. Lakini kama ni taasisi au chombo kinachojitegemea, Tumishi ya Mahakama haiwezi kuanzishwa na Muswada huu. Hii ni kwa sababu Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ni vyombo vya kikatiba kwa maana ya kuanzishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Aidha, Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu ya Tanzania zimeanzishwa chini ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

Pili, kwa upande mwingine, Tumishi ya Mahakama inaonekana kama ni jina lingine la chombo kinachoitwa Tume ya Utumishi wa Mahakama kilichoundwa na ibara ya 112(1) ya Katiba. Chombo hicho ni “... Tume ya Ushauri wa Uteuzi wa Majaji na

Ajira ya Mahakimu wa Mahakama za Tanzania Bara...” Chini ya ibara ya 113(1) ya Katiba, moja ya majukumu ya Tume ni pamoja na kuajiri Mahakimu na kusimamia nidhamu yao. Aidha, ibara ya 113(4) inaweka wazi kwamba, madaraka ya kuajiri, kuwathibitisha kazini, kudhibiti nidhamu na kuwaondoa kazini Mahakimu wa Mahakama za Tanzania Bara yatakuwa mikononi mwa Tume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa kunahitajika *clarification*, je, Tumishi ya Mahakama ni kitu hicho hicho kama Tume ya Utumishi wa Mahakama au ni kitu kinachojitegemea.

Kifungu cha 13(1) cha Muswada huu kinapendekeza kuendelea kuwepo kwa Tume hii, wakati kifungu cha 14(1) kinapendekeza Tume iongezewe madaraka ya kuajiri, kuwathibitisha kazini, kuwapandisha vyeo na kudhibiti nidhamu ya maafisa wasiokuwa wa kimahakama. Hawa kwa mujibu wa tafsiri ya maneno, Maafisa wasiokuwa wa kimahakama ni watumishi wanaofanya kazi zisizokuwa za kimahakama. Zaidi ya hayo, kifungu cha 15 kinapendekeza Mtawala Mkuu wa Mahakama awe ndiye Katibu wa Tume mwenye mamlaka ya kuwezesha utekelezaji wa maamuzi yote ya Tume.

Swali hapa ni je, Tume ni sehemu ya Tumishi ya Mahakama au la? Kama jibu ni ndiyo, basi inabidi Muswada uliweke hilo wazi kwa njia ya kupanua tafsiri ya maneno Tume au Mahakama au Tumishi kwa lengo la kuijumuisha Tume katika tafsiri ya maneno hayo. Lakini kama jibu ni hapana, basi itabidi Muswada uonyeshe uhusiano katika Tume na Tumishi ya Mahakama kwani, kama tulivyoonyesha mwanzoni, Tume ndiyo inayoajiri na kudhibiti nidhamu ya Mahakimu na sasa Muswada unapendekeza ipewe uwezo kisheria wa kuajiri wafanyakazi wasiokuwa wa kimahakama. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 4(3) cha Muswada watumishi hawa wanakatazwa kupokea maelekezo kutoka kwenye mamlaka nyingine yoyote nje ya Tumishi. Kwa maana nyingine, kama jibu la swali ni hapana, watumishi wa Tumishi ya Mahakama ambao wengi wao wameajiriwa na Tume na wanawajibika kwayo katika masuala ya kinidhamu hawatakiwi kupokea maelekezo yoyote kutoka Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie nafasi ya Mtawala Mkuu wa Mahakama. Kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Muswada, Tumishi ya Mahakama itaongozwa na Mtawala Mkuu wa Mahakama ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu watatu watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama. Kifungu cha 7(3) kinapendekeza sifa za Mtawala Mkuu huyo kuwa ni awe ameshikilia nafasi ya juu katika utumishi wa umma, awe na ujuzi uliothibitika na uzoefu katika Nyanja za utawala na fedha na awe na uadilifu wa hali ya juu na tabia njema.

Kwa mujibu wa kifungu cha 8, kazi za Mtawala Mkuu wa Mahakama ni pamoja na uendeshaji wa jumla wa Tumishi, kuandaa na kuwasilisha taarifa za kila robo mwaka juu ya uendeshaji wa Tumishi na kufanya kazi nyingine na kutekeleza mamlaka mengine aliyopewa na kifungu cha 53 cha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna uwezekano wa kupata maji hapa nitasema ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Sawa endelea ombi lako limezingatiwa.

MHE. TUNDU A.M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kifungu cha 8(2) kinakataza Mtawala Mkuu wa Mahakama kufanya kazi ambazo zimepewa Maafisa wa Kimahakama na sheria. Kifungu cha 53(1) kinapendekeza Mtawala Mkuu wa Mahakama aweze kupokea, kwa niaba ya Mahakama, misaada inayotolewa kwa Mahakama na Serikali za nchi za nje, Mashirika na/au Taasisi za Kimataifa au mtu binafsi. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa kifungu cha 52(3) cha Muswada, Mtawala Mkuu wa Mahakama ndiye atakuwa na mamlaka ya uendeshaji na udhibiti wa Mfuko wa Mahakama unaopendekezwa kuundwa na kifungu cha 52(1) cha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vilivyoainishwa hapo juu vinahitaji kuangaliwa upya kwa sababu vinaweza kudhoofisha zaidi utendaji wa Mahakama. Kwanza, pamoja na umuhimu wa kuwa na mtu mwenye sifa zilizotajwa katika kifungu cha 7(3) cha Muswada huu, ni muhimu vilevile mtu anayependekezwa kupewa mamlaka makubwa katika uendeshaji wa Tumishi ya Mahakama awe na ufahamu mkubwa na uzoefu wa kutosha wa uendeshaji wa Mahakama. Mtu huyo sharti awe na ufahamu mkubwa wa sheria, utamaduni, mila na desturi za kimahakama na nafasi ya Mahakama katika mfumo wetu wa kikatiba na kiutawala.

Kwa mfano, katika mfumo wetu wa kikatiba na kiutawala, Mahakama zinatakiwa kuwa huru katika kufanya maamuzi yanayohusu haki na wajibu wa watu na Serikali, taasisi za umma na za binafsi. Mtawala Mkuu wa Mahakama asiyejua sheria, utamaduni, mila na desturi za mfumo wetu wa kikatiba anaweza asielewe pale atakapona matendo ya mamlaka za Kiserikali yakihojiwa Mahakamani au watendaji wakuu wa Idara za Serikali kama Mawaziri na/au Rais aliyemteua na mwenye mamlaka ya kinidhamu juu yake wakifikishwa Mahakamani kwa sababu za utendaji wao wa kazi au kwa sababu nyingine. Mtawala Mkuu wa Mahakama wa aina hiyo anaweza kutumia udhibiti wake wa Mfuko wa Mahakama kuinyima Mahakama fedha kwa lengo la kuwalinda mabosi wake hao wa kisiasa. Hii ni hatari sana kwa nchi inayoamini katika utawala wa sheria. Aidha, Mtawala Mkuu wa Mahakama sharti awe mtu anayefahamu mahitaji mahsusi ya Mahakama ambayo yako tofauti na mahitaji ya vyombo vingine vya dola kama Bunge na Serikali. Kwa mfano, Mahakama zinahitaji kuwa na vitabu vya sheria, majarida ya kisomi ya kisheria na Ripoti za Maamuzi ya Mahakama za sehemu mbalimbali duniani na zinahitaji Ripoti za Maamuzi yake kuchapishwa kila mwaka kwa ajili ya matumizi ya kila siku ya Mahakimu na Majaji. Mtawala Mkuu wa Mahakama asiyejua Sheria anaweza asifahamu mahitaji mahsusi kama haya na matokeo yake ni kutoyapa kipaumbele katika Bajeti ya Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie juu ya masuala ya fedha yaliyoko katika Muswada huu. Masuala tunayoyazungumzia hapa sio mambo ya nadharia au ya kufikirika tu kwani moja ya matatizo makubwa yanayokabili Mahakama zetu nchini ni pamoja na vipaumbele vyake kutozingatiwa katika migawanyo ya bajeti za Serikali za kila mwaka. Kwa mfano, wakati lengo ni kuwa na Kanda ya Mahakama Kuu katika kila

Mkoa wa Tanzania Bara, hadi sasa kuna Kanda kumi na tatu nchi nzima na Divisheni tatu, yaani Divisheni ya Biashara, ya Kazi na ya Ardhi ambazo zote ziko Dar es Salaam. Hii ina maana kwamba kuna mikoa kumi na tatu ambayo haina Kanda za Mahakama Kuu na watu watokao katika mikoa hiyo wanalazimika kuingia gharama na usumbufu mkubwa kwenda kwenye kesi zao katika Kanda za Mahakama Kuu zilizoko mikoa mingine. Aidha, wenye kesi za biashara au za ajira au za ardhi inabidi waamue kufunga safari kwenda Dar es Salaam kufungua kesi zao kwenye Divisheni za mambo hayo au vinginevyo wasubiri Majaji wa Divisheni hizo watembelee Kanda za Mahakama Kuu zilizo karibu nao kwa ajili ya kusikiliza kesi zao. Hii ndio sababu kubwa ya mrundikano wa kesi zisizokwisha katika Kanda za Mahakama Kuu. Hali ni mbaya vilevile katika Mahakama za chini. Kwa mfano, katika Mahakama za Wilaya 125 zilizopo hadi hivi sasa, ni Mahakama 105 tu ndizo zinazofanya kazi pamoja na zinazotembelewa. Aidha, kuna Mahakama za Mahakimu wakazi 25 na Mahakama za Mwanzo 1105 zinazohudumia nchi yenye watu zaidi ya milioni 40. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya zaidi kwa upande wa watumishi wa Mahakama hizi kutoka Mahakimu, Makarani, wahudumu hadi walinzi. Kwa mfano, kuna Mahakimu Wakazi na Wasajili 346 na Mahakimu wa Wilaya 29 wanaofanya kazi katika Mahakama 25 za Mahakimu Wakazi na Mahakama 105 za Wilaya. Aidha, wakati mahitaji halisi ya Mahakama za Mwanzo ni kuwa na Mahakimu 2,210, idadi halisi ya waliopo ni Mahakimu 759 wanaohudumia Mahakama za Mwanzo 1105. Kwa maneno mengine, badala ya kuwa na Mahakimu wawili kwa kila Mahakama ya Mwanzo, kuna Hakimu mmoja kwa Mahakama za Mwanzo 759 na kuna Mahakama za Mwanzo 346 ambazo hazina Hakimu hata mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika migawanyo ya fedha kwenye bajeti za Serikali za kila mwaka, vipaumbele vya Mahakama vimekuwa havizingatiwi vile vile. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2010/2011, mahitaji halisi ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania yalikuwa ni shilingi 52,795,000,000. Hata hivyo, ukomo wa bajeti ya Serikali kwa Mahakama hiyo uliowekwa na Hazina ni shilingi 7,364,000,000 tu, ikiwa ni takriban 14% ya mahitaji halisi.

Vile vile, mahitaji ya Mahakama Kuu katika kipindi hicho hicho yalikuwa ni shilingi bilioni 55 lakini ukomo wa bajeti ni shilingi 11,627,736,136.00 ikiwa ni takriban 21% ya mahitaji halisi. Hali iko hivyo hivyo katika Mahakama za Wilaya na za Mwanzo ambako mahitaji halisi yalikuwa ni shilingi bilioni 31 lakini ukomo wa Hazina ni shilingi 6,949,00,000 sawa na takriban 22% ya mahitaji halisi. Kwa Divisheni zote tatu za Mahakama Kuu, mahitaji yao halisi yalikuwa ni shilingi 8,204,000,000 lakini ukomo wa bajeti uliowekwa na Hazina ni shilingi 3,036,148,000.00 sawa na 37% ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mahakama kupangiwa bajeti ndogo sana ukilinganisha na mahitaji yao halisi, utoaji wa fedha hizo ni mdogo zaidi. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2009/2010, mahitaji halisi ya Mahakama Kuu yalikuwa shilingi bilioni 43 wakati ukomo wa bajeti uliowekwa na Hazina ulikuwa ni shilingi 18,925,000,000 au 44% ya mahitaji halisi. Hata hivyo, kiasi halisi kilichotolewa kilikuwa shilingi 15,266,000,000 ambacho ni sawa na 35.5% ya mahitaji halisi. Kwa upande wa

Mahakama za Wilaya na za Mwanzo, mahitaji halisi yalikuwa shilingi bilioni 62 wakati ukomo uliowekwa ulikuwa shilingi 23,353,000,000 au 38% ya mahitaji halisi. Hata hivyo, kiasi halisi kilichotolewa kilikuwa shilingi 15, ambacho ni takriban 24% ya mahitaji halisi na kwa Mahakama ya Rufani, mahitaji halisi yalikuwa shilingi bilioni 53 wakati ukomo ulikuwa shilingi 29,948,000,000, ambayo ni 57% ya mahitaji halisi. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa kilikuwa shilingi 17,775,000,000, sawa na 33.5% ya mahitaji halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kuzinyima mahakama fedha zinazolingana na mahitaji yao halisi na hata zinazolingana na ukomo wa chini uliowekwa na Hazina, Mahakama zimelazimika kujiingiza katika mambo ambayo yanapunguza hadhi na heshima yake kwa jamii. Mahakama ya Tanzania imekuwa ni mdeni mkubwa na sugu. Kwa sababu ya kunyimwa fedha kama tulivyoonyesha, Mahakama zetu zimekuwa na matatizo makubwa ya kushindwa kulipia vifaa, huduma na stahili mbalimbali za Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama. Takwimu zilizopo kuhusiana na jambo hili zinasikitisha na kwa kweli, ni fedheha kwa nchi inayodai kwamba inaheshimu utawala wa sheria, uhuru wa Mahakama na mgawanyo wa madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, deni la Mahakama ya Rufani ya Tanzania kutokana na kushindwa kulipia vifaa, huduma na stahili za watumishi wa Kimahakama na wasiokuwa wa Kimahakama lilikuwa shilingi 2,725,000,000. Kwa upande wa Mahakama Kuu, deni lake kutokana na kushindwa kulipia vifaa, huduma na stahili za watumishi wa Kimahakama na wasiokuwa wa Kimahakama lilikuwa shilingi 1,633,000,000 na kwa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo, deni lao kwa wagavi wa vifaa, huduma na stahili za watumishi wa Mahakama hizo lilikuwa shilingi 1,600,000,000. Jumla ya madeni yote ya Mahakama ya Tanzania kwa mwaka huu wa fedha ni shilingi 5,958,000,000, zinazodaiwa na wagavi wa vifaa na huduma muhimu za uendeshaji wa Mahakama na zinazotokana na kushindwa kulipa stahili za Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa kada mbalimbali wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania ina mamlaka kikatiba na kisheria ya kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za aina mbalimbali zikiwemo za biashara na ajira za watu binafsi au taasisi zinazodaiana au kati ya waajiri na wafanyakazi wao. Aidha, Mahakama ya Tanzania ina uwezo wa kuamuru wadaiwa walioshindwa kulipwa madeni wanayoamriwa kulipa na Mahakama wafilisiwe au mali zao zikamatwe na kuuzwa au wafungwe jela kama wafungwa wa kiraia. Sasa kama tumeruhusu Mahakama zetu kuwa wadeni wakubwa na sugu kiasi hiki, wagavi wa vifaa na huduma mbalimbali muhimu kwa uendeshaji wa Mahakama ambao madeni yao hayalipwi kwa sababu Mahakama hazipewi fedha zinazolingana na mahitaji yao watakwenda wapi kudai haki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kama Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama wenyewe hawalipwi stahili zao halali kwa mujibu wa mikataba yao ya ajira, waende wapi kulalamika na wamshtaki nani? Ni Mahakama ipi nyingine inayoweza kusikiliza madai ya Majaji wetu au Mahakimu wetu au watumishi wetu wa Mahakama

ambao hawajatendewa haki na mwajiri wao? Mahakama zitapata wapi mamlaka ya kiuadilifu (*moral authority*), kama sio mamlaka ya kisheria, kuamuru wadeni wengine wanaopelekwa Mahakamani wakamatiwe mali zao au wafilisiwe au wafungwe jela wakati Mahakama yenyewe ni mdeni mkubwa na sugu! Kama huku sio kuifanya Mahakama ya Tanzania idharaulike na kuishushia heshima machoni kwa wananchi ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ushahidi huu wa mgawo wa bajeti ya Mahakama, kuna hoja kuu kadhaa zinazojitokeza wazi. Hoja ya kwanza ni kwamba, tatizo kubwa linalozikabili Mahakama zetu sio uhaba wa uwezo wa kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili yao, bali ni uhaba wa fedha zenyewe! Pili, tatizo la uhaba wa fedha linaweza kuwa linasababishwa na ukosefu wa fedha zenyewe au linasababishwa na ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama. Tatu, tatizo la ukosefu wa uelewa wa mahitaji halisi ya Mahakama linaweza likawa linasababishwa na ukosefu wa watu wanaoelewa mahitaji hayo Serikalini au ukosefu wa wafanya maamuzi ya migawanyo ya fedha wanaofahamu mahitaji halisi ya Mahakama. Kama ni hivyo, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, dawa ya matatizo ya uendeshaji wa Mahakama sio kuwa na Mtawala Mkuu wa Mahakama mwenye sifa zinazopendekezwa na Muswada huu bali ni kuzipatia Mahakama fedha zinazolingana na mahitaji yake halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui nina muda kiasi gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuzinyima Mahakama fedha zinazolingana na mahitaji yake halisi yamekuwa ni kuzinyima uwezo wa kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuwa “mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano”, kutumia maneno ya ibara ya 107A(1) ya Katiba. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mahakama ya Rufani ilipanga kufanya vikao ishirini na mbili vya kusikiliza kesi za rufaa. Hata hivyo, kutokana na kutokupatiwa fedha kulingana na mahitaji yake halisi, Mahakama hiyo iliweza kufanya vikao kumi na sita tu hadi kufikia mwezi Machi, 2011. Vile vile, Mahakama Kuu katika Kanda mbali mbali kumi na tatu zilipanga kufanya jumla ya vikao 124 katika kipindi hicho. Hata hivyo, kutokana na kutokupatiwa fedha zinazolingana na mahitaji halisi ya vikao hivyo, Mahakama Kuu iliweza kufanya vikao kumi na tano tu na Kanda sita hazikufanya kikao hata kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, hii ndio moja ya sababu halisi ya Magereza kufurika mahabusu ambao kesi zao haziishi. Hii ndio moja ya sababu halisi ya migomo ya mahabusu inayoanza kushika kasi katika magereza mbalimbali hapa nchini. Dawa ya matatizo haya sio kutunga sheria nyingine ya utawala wa Mahakama bali ni kuhakikisha Mahakama zinapatiwa vitendea kazi zinavyohitaji ili kutekeleza wajibu wao wa kikatiba. Katika hili, Muswada huu una mapungufu makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za Mahakama, Kifungu cha 52 cha Muswada huu kinapendekezwa kuundwa kwa Mfuko Maalum utakaoitwa Mfuko wa Mahakama na ambao fedha zake zitatokana na malipo kutoka Hazina. Vyanzo vingine vya fedha za Mfuko huu vinapendekezwa kuwa misaada ya Serikali za nje, Taasisi za

Kimataifa na za Kitaifa na hata watu binafsi. Vyanzo hivi vingine vinatakiwa kuzingatia masharti ya Sehemu ya V ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134 ya Sheria za Tanzania (*The Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974*). Kifungu cha 15(1) cha Sheria hiyo kinampa Waziri anayehusika na masuala ya fedha mamlaka ya kupokea misaada yoyote inayotolewa na Serikali za nchi za nje au na watu wengine kwa niaba ya Serikali. Waheshimiwa Wabunge baada ya maelezo hayo, naomba sasa nitishe shughuli hizi za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine, Muswada unapendekeza fedha na misaada itakayotolewa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama kwa mujibu wa kifungu cha 53(1) cha Muswada zipokelewe na Waziri wa Fedha. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, masharti haya yanaendeleza utegemezi wa Mahakama ya Tanzania kwa Serikali na yanafisha uhuru wa Mahakama na uwezo wake wa kutekeleza wajibu wake wa kutenda haki. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba misaada kwa Mahakama ipelekwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa Mahakama bila kupitia kwenye Mifuko ya Waziri wa Fedha ambaye anaweza kuzichelewesha au kuzizuia fedha na misaada hiyo na hivyo kuhujumu uwezo na uhuru wa Mahakama katika utekelezaji wa majukumu yake kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 57 kinampa Mtawala Mkuu wa Mahakama wajibu wa kuandaa mapendekezo ya bajeti ya kila mwaka ya Mahakama kwa ajili ya huduma zinazotolewa kwa Mahakama; mishahara na malipo mengine ya watumishi wa Kimahakama na wasiokuwa wa Kimahakama na mahitaji mengine ya Mahakama. Katika kuandaa bajeti hiyo, Mtawala Mkuu wa Mahakama anatakiwa kuzingatia aina, kiasi na viwango vya huduma zinazohitajika kwa ajili ya uendeshaji mzuri wa Mahakama na zinazohitajiwa na watumishi wa Kimahakama na wasiokuwa wa Kimahakama katika utekelezaji bora wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalotia wasiwasi katika maandalizi ya bajeti ya Mahakama ni pendekezo la kifungu cha 57(3) cha Muswada kinachoelekeza kwamba: “Mtawala Mkuu wa Mahakama atatakiwa kuandaa makadirio ya Mahakama ndani ya ukomo wa bajeti wa mwaka wa fedha husika”. Kama tulivyoonyesha kwa kirefu, masharti ya ukomo wa bajeti yanayowekwa na Hazina yamekuwa hayazingatii mahitaji halisi ya Mahakama. Aidha, tumeonyesha jinsi ambavyo Hazina yenyewe haitoi fedha kwa Mahakama kulingana na ukomo wa bajeti iliyoiwekea. Maana halisi ya pendekezo hili ni kuendeleza mambo yale yale ambayo yamethibitika kuhujumu uwezo wa Mahakama wa kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuzinyima fedha za kuendesha shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, pendekezo hili ni ushahidi wa wazi wa kutokuwepo kwa nia ya dhati ya kutatua matatizo ya fedha ya Mahakama. Badala ya kuziwekea Mahakama masharti ya ukomo wa bajeti ambao hata hivyo hauheshimiwi na Serikali yenyewe, ni bora Muswada huu uweke kanuni ya wazi kwamba bajeti ya Mahakama iandaliwe kutokana na mahitaji halisi ya Mahakama. Kufanya hivyo kutathibitisha nia yetu ya kulinda uhuru wa Mahakama, utawala wa sheria na mgawanyo wa madaraka ambazo ndio nguzo kuu za mfumo wetu wa kikatiba na

kiutawala. Kufanya hivyo kutapunguza msongamano wa kesi na mateso wanayoyapata watu wetu kwa sababu ya Mahakama kushindwa kufanya kesi kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio kwa uhuru wa Mahakama, mfumo wa kikatiba na kiutawala unatambua dhana ya utawala wa sheria na uhuru wa Mahakama. Dhana ya utawala wa sheria imeangikwa katika msingi kwamba Mahakama ndio chombo cha utoaji haki katika nchi inayofuata demokrasia na Serikali iliyodhibitiwa (*limited Government*). Ndio maana Ibara ya 107A(1) inatamka wazi kwamba: “Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.” Aidha, Ibara ya 107B inazingatia umuhimu wa uhuru wa Mahakama katika utekelezaji wa utawala wa sheria kwa maneno yafuatayo: “Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, Mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi tuliouonyesha, inaelekea kuna masharti mengine ambayo pamoja na kuwa nje ya Katiba yanaathiri kwa kiasi kikubwa uhuru na kauli ya Mahakama katika kutekeleza mamlaka yake ya utoaji haki. Masharti hayo ni pamoja na Mahakama kutopewa fedha kulingana na mahitaji yake halisi wala kulingana na ukomo wa bajeti uliowekwa na Hazina bali kupewa fedha kulingana na vigezo visivyojulikana wazi kwa umma lakini vinavyotegemea fadhila na/au busara za Hazina. Muswada huu unapendekeza kuweka masharti haya wazi katika sheria kwa mujibu wa pendekezo la kifungu cha 57(3) cha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mapendekezo mengine ambayo pia yanatishia uhuru wa Mahakama. Haya ni mapendekezo yanayohusu utaratibu wa nidhamu za watumishi wa Kimahakama. Kifungu cha 46 kinapendekeza kuanzishwa kwa Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Kimahakama ambayo, kwa mujibu wa kifungu cha 47(1)(a) itashughulikia malalamiko dhidi ya watumishi wa Kimahakama wasiokuwa Majaji wa Rufaa, Jaji Kiongozi au Majaji wa Mahakama Kuu. Kwa upande mwingine, kifungu cha 50(5) kinapendekeza kuzipa Kamati za Maadili ya Watumishi wa Kimahakama za Mikoa wajibu wa kushughulikia nidhamu za Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu Wakazi wa mikoa husika. Hii ina maana kwamba Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Kimahakama itashughulikia masuala ya nidhamu ya Wasajili, Wasajili wa Wilaya na Manaibu Wasajili wa Mahakama ya Rufani na wa Mahakama Kuu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ina wajumbe ambao wote ni watumishi wa Kimahakama (kifungu cha 46(2)). Hata hivyo, utaratibu unaopendekezwa kwa ajili ya kushughulikia nidhamu ya Mahakimu Wakazi na wa Wilaya una hatari kubwa ya kuingiliwa na wanasiasa. Hii ni kwa sababu Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Kimahakama ya Mkoa inaundwa na kuongozwa na Mkuu wa Mkoa. Wajumbe wengine wa Kamati hiyo ni Katibu Tawala wa Mkoa, Hakim Mkazi Mfawidhi wa Mkoa, wajumbe wawili wa kuteuliwa na Mkuu wa Mkoa na watumishi wengine wawili wa Kimahakama watakaoteuliwa na Jaji Mfawidhi (kifungu cha 50(1)).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, mapendekezo ya kuwafanya wanasiasa kama Wakuu wa Mikoa Wenyevidi wa Kamati za Maadili ya Watumishi wa Kimahakama za Mikoa inahatarisha uhuru wa Mahakama. Wakuu wa Mikoa karibu wote ni makada wa Chama cha Mapinduzi na wajumbe wa Kamati za Siasa za CCM katika mikoa yao. Makada hawa wa CCM wana tabia ya kuingilia utendaji wa Mahakama zetu na mara nyingi ni wakiukaji wa sheria na taratibu za nchi yetu. Mara nyingi Mahakama ni vyombo pekee katika mikoa vyenye mamlaka kisheria ya kuwadhibiti pale wanapokiuka miiko ya kisheria ya kazi zao. Watu hawa hawafai kushika nyadhifa kubwa kama kuwa wasimamizi wa nidhamu ya watumishi wa Kimahakama ambao wanaweza kusimamia kesi dhidi yao.

Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba utaratibu wa kudhibiti nidhamu ya Mahakimu Wakazi na wa Wilaya uongozwe na watumishi wa Kimahakama kama ilivyo kwa Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Kimahakama ili kusiwe na matabaka katika utaratibu wa kushughulikia nidhamu za watumishi wa Kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti mengine ambayo hayako kwenye Katiba wala sheria za nchi lakini ambayo Mahakama zetu zinatakiwa kuyazingatia ni pamoja na kukopa vifaa na huduma kutoka kwa wagavi bila kuwepo uhakika wa namna gani na lini madeni hayo yatalipwa na hivyo kuzigeuza Mahakama zetu kuwa wadeni wakubwa na sugu sawa na wadeni wengine wanaopeleka kesi zao katika Mahakama hizo hizo. Aidha, Mahakama inatakiwa izingatie masharti yasiyokuwa kwenye sheria kwamba sio lazima sana kwa Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wasiokuwa wa Kimahakama kulipwa stahili zinazotokana na mikataba na masharti ya kisheria ya ajira zao. Kumbesio muhimu sana kwa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu au Mahakama za chini kuendesha vikao vya kesi kwa sababu ya kunyimwa fedha kwa ajili hiyo. Katika mazingira haya, kutegemea kwamba Mahakama zitatekeleza majukumu yao ya kikatiba kwa uhuru na kwa ufanisi ni kutegemea miujiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwapi Mgawanyo Wa Madaraka? Mfumo wetu wa kikatiba na kiutawala pia umejengwa katika misingi ya mgawanyo wa madaraka na uwajibikaji iliyowekwa na Katiba. Ibara ya 4(1) na (2) ya Katiba inaweka msingi wa kikatiba wa mgawanyo wa madaraka baina ya vyombo vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki na pia vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Muswada huu unatishia msingi huu muhimu katika utekelezaji wa shughuli za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, chini ya Muswada huu, Rais anaendelea kuwa na kivuli kirefu katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Kimahakama. Chini ya kifungu cha 7(1) cha Muswada, Rais ndiye atakayemteua Mtawala Mkuu wa Mahakama na si Bunge wala chombo kingine cha uwakilishi na usimamizi chenye mamlaka ya kuthibitisha uteuzi huo. Vile vile kwa mujibu wa kifungu cha 7(6), Rais ndiye anayeamua masharti ya ajira ya Mtawala Mkuu wa Mahakama. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha (9), mamlaka ya nidhamu juu ya Mtawala Mkuu wa Mahakama ni Rais. Hata pale ambapo Jaji Mkuu anamteua mtu mwingine kukaimu nafasi hiyo kwa sababu ya

kutokuwepo kwa muda mfupi kwa Mtawala Mkuu wa Mahakama ni sharti Jaji Mkuu amtaarifu Rais [kifungu cha 10(2)].

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Muswada huu unapendekeza kumpa Rais hata mamlaka ya kuanzisha au kuvunja nafasi za Kimahakama na zisizokuwa za Kimahakama. Kifungu cha 21(1) kinapendekeza Rais kuomba ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhusu "... jukumu lolote la kuanzisha na kufuta nafasi yoyote ya Kimahakama au isiyokuwa ya Kimahakama na Tume itawajibika kumshauri Rais juu ya jambo ililopelekewa." Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, pendekezo hili linakwenda kinyume na mamlaka ya Rais kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaliyowekwa na Ibara ya 36(1) ya Katiba. Hii ni kwa sababu mamlaka hayo yanatakiwa kutekelezwa: "Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na sheria nyingine yoyote...." Nafasi za Kimahakama kama Majaji na Mahakimu zimewekwa na ama Katiba yenyewe au na sheria nyinginezo na kwa hiyo Rais hana mamlaka ya kuzianzisha au kuzifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo mengine ambayo yasiporekebishwa na/au kuondolewa yanaweza kuleta migongano ya kitaasisi isiyokuwa na sababu yoyote ya msingi na hivyo kuathiri utendaji wa Mahakama zetu. Kwa mfano, wakati kifungu cha 7(4) kinapendekeza Mtawala Mkuu wa Mahakama awajibike kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama, kifungu cha 7(5)(b) kinapendekeza awajibike kwa Jaji Mkuu! Aidha, kifungu cha (9) kinamlazimu Mtawala Mkuu wa Mahakama kuwajibika kwa Rais kama mamlaka yake ya kinidhamu. Katika hali halisi, atakapokabiliwa na uamuzi juu ya afuate maagizo ya mamlaka ipi kati ya hizi tatu, ni wazi Mtawala Mkuu wa Mahakama atawajibika kwa mamlaka inayoweza kumnyang'anya ajira yake, yaani Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya maoni haya. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Simbachawene, kwa michango yao mbali mbali wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue fursa hii kuwashukuru wasaidizi wa Kambi Rasmi ya Upinzani; Msaidizi wa Masuala ya Kisheria Stella Bwimbo, Msaidizi wa Masuala ya Kibunge Oliver Mwikila na Msaidizi wa Masuala ya Kiutawala Frank Mbumi kwa msaada na ushauri wa kitaalam uliofanikisha maandalizi ya hoja hii. Mwisho naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Matukio ya siku ya leo, ambapo Muswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba ya mwaka 2011 umeondolewa Bungeni, yamethibitisha usahihi wa msimamo

wetu juu ya masuala muhimu katika mustakabali wa nchi yetu. Tunawaomba waendeleo kutuunga mkono na kututia nguvu katika siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na kwa vile muda umekwisha, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: *People's! People's!*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge, tunapoendelea na mjadala huu, naomba nichukue dakika zenu mbili nitambue uwepo wa Viongozi wanaohusiana na Muswada huu kuwepo hapa ndani wakiwa pamoja nasi kuona mjadala wetu unavyoendelea. Wageni hawa ni wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Oliver Mhaiki, yeye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; Mheshimiwa Mary Shangari, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma; Mheshimiwa Sivangilwa Mwangesi, Jaji wa Mahakama Kuu Dodoma; Bwana Lenatus Rutatinisibwa, Msajili wa Wilaya Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma na Bwana George Masaju, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Baada ya kuwatambua wageni hawa, sasa naomba kama nilivyosema, nimwite msemaji wetu wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Rashid Abdalla ajiandae. Mheshimiwa Silinde tafadhali!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kwanza kabisa katika kuchangia Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mahakama ni miongoni mwa mihimili mitatu ya Dola kwa maana ya Serikali (*Executive*), Mahakama yenyewe (*Judiciary*) pamoja na Bunge (*Legislature*). Kwa kuwa kila mhimili una majukumu yake, kwa maana ukija Bunge maana yake jukumu lake ni kutunga sheria na Mahakama jukumu lake ni kutafsiri sheria ili haki iweze kupatikana, basi Serikali jukumu lake kubwa ni utawala zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka sasa 50, Mahakama ilikuwa haitambuliki kama mhimili wa Dola kwa kuwa ilikuwa ndani ya Serikali. Sasa kinachohitajika kwa kuwa Muswada umeletwa mbele yetu ili tuweze kuupitisha ama tuweze kuhoji, tuuboreshe pale inapohitajika, sasa tunahitaji kuona kweli kabisa kinachokwenda kuzungumzwa na Wabunge kinazingatiwa bila kufuata itikadi za vyama, bali tuzingatie uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, tunahitaji zaidi uende kuzingatia haki ambazo zinatendeka kwa kutafsiri sheria ndani ya Mahakama zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ningependa zaidi kuchangia katika sehemu ya nne inayohusiana na masuala mazima ya fedha ambayo yanapelekea kuunda Mfuko Maalum wa Mahakama. Hapa zaidi ningezungumzia jambo la kwanza kuhusiana na vyanzo vya mapato vya Mahakama, lakini lingine ni kuhusiana na usimamizi wa fedha za Mfuko Maalum wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, suala la vyanzo vya mapato, kabla Mahakama ilikuwa inategemea zaidi fedha kutoka Serikalini, lakini sasa ili Mahakama iweze kutenda kazi zake kikamilifu, kinachohitajika ni kupata fedha moja kwa moja kutoka katika Mfuko wa Hazina ambapo sasa itakuwa na uwezo wa kujitegemea kwa maana kwamba itakuwa na nafasi ya kujipangia mishahara yake, itakuwa na nafasi ya kuajiri watumishi na itakuwa na nafasi ya kuwekeza katika masuala mengine yanayohusiana na Mahakama kwa maana ya utendaji mzima wa kazi za Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kama hili halitoshi, tunahitaji sasa...kwa kuwa Mfuko na fedha zote zinazotoka Hazina zinatakiwa ziwe chini ya usimamizi wa Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hapa ninapomzungumzia CAG, ni kwamba pamekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kwamba CAG amekuwa akishindwa kupata taarifa kamili katika Sekta na Idara mbalimbali za Serikali. Sasa inapokuja katika *case* ya Mahakama ambako wao kwa hali ya kawaida wanaonyesha kabisa kwamba kwa mfumo wa kisheria, panakuwepo na tishio la kawaida, maana mahali popote panapoitwa Mahakama, watu wanakuwa na hofu. Sasa, hata watendaji wa CAG wanaweza wakawa na hofu ya kuhoji pale inapotokea Mfuko Maalum wa Mahakama unapokuwa umekwenda kinyume na taratibu za fedha ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, pawepo na Kanuni ambazo zitaruhusu Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, awe na *accessibility* ya kuingia na kukagua zile fedha bila kipingamizi chochote. Kwa hiyo, hili ningependa kabisa kwamba lichukuliwe kwa undani zaidi na Waziri wa Sheria pamoja na Kamati, hili ni lazima mlizingatie na sheria hiyo lazima ipitishwe katika Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba fedha zote zitakazokuwa zinakwenda sasa katika mhimili wa Mahakama, zinahitaji sasa kwenda katika vile vipaumbele husika ambavyo Watanzania wamekuwa wakilalamika kwa muda. Tunalalamika kwamba nchi imekosa Mahakama kwa maana kwamba hatuna Mahakama za Mwanzo, hatuna Mahakama za Wilaya za kutosha, hatuna watendaji kwa maana ya watumishi wa kutosha katika kuendesha shughuli za Kimahakama. Sasa hizi fedha zitakazokuwa zinapelekwa katika Mfuko Maalum wa Mahakama, zielekezwe zaidi katika vipaumbele ambavyo vitapelekea kutenda haki na kupunguza zile kesi ambazo zimekuwa zikienda kinyume na utaratibu na kusababisha katika Magereza yetu kwa maana ya Mahabusu na wafungwa wamekuwa wengi kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachohitaji kuzungumzia ni kwamba, tunahitaji sasa kukifanya Chombo Kikuu cha Mahakama kiwe huru ili tupate ile dhana ya uhuru wenyewe (*Independent Situation*). Hapa ninachokizungumzia ni kwamba, sasa tutakuwa

na nafasi ya kuilaumu Mahakama endapo itashindwa kutekeleza wajibu wake kwa sababu sasa hivi ukiwaambia kwamba jamani Mahakama ni kwa nini mnaifanya moja, mbili, tatu, wao watakachokueleza ni kwamba tumekosa fedha za kuendesha hii kesi kwa sababu Serikali imetunyima ama tumekosa kwa sababu Serikali kushindwa kuleta kwa wakati muafaka. Sasa hivi tunahitaji, kile watakachokiomba wapatiwe ili na sisi tuweze kuwanyoshea mkono endapo watashindwa kutekeleza majukumu yao kama walivyokuwa wamepanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningehitaji kulizungumzia ni kuhusiana na Mtawala Mkuu wa Mahakama. Mtawala Mkuu wa Mahakama, amepewa mamlaka naona ni makubwa kidogo, utafikiri ni Jaji Mkuu wa Serikali. Nafikiri sasa tunahitaji kutengeneza *structure* mpya ya kiutawala kwa maana kwamba pawepo na Jaji Mkuu, aeleweke *structure* yake na *functions* zake pale, Mtawala Mkuu, ieleweke na katika masuala ya fedha si lazima Mtawala Mkuu akaingia pale, pawepo na *Chief Accountant* ambaye ni *General* katika Masuala mazima ya Mahakama, ambaye atakuwa na *knowledge* zote mbili kwa maana ya uelewa katika sheria za Kimahakama pamoja na mambo ya Kiuhasibu ambapo itakuwa ni rahisi kuendesha shughuli za Kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa uchache ningependa niishie hapo, lakini naunga mkono hiyo hoja. (*Makofi*)

(*Hapa taa za Ukumbini zilizimika*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa David Silinde. Ningeomba sana Timu yetu ya Ufundi mtusaidie kurudisha mwanga ndani ya Ukumbi wa Bunge. Baada ya Mheshimiwa Silinde, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Rashid Ali Abdalla na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo atafuatia.

MHE. RASHID ALI ABDALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Leo sitokuwa na mashaka na vifungu mbalimbali vya Muswada huu kwa sababu nilikuwa kwenye Kamati iliyopitia Muswada huu. Ningeomba tu uniruhusu nieleze kidogo vidokezo au msisitizo kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili la mabadiliko ya Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama liliazimiwa tokea mwaka 1977. Mwaka 1977 hadi sasa ni miaka 34. Kipindi chote hicho cha miaka 34, Mhimili Mkuu wa Dola ulikuwa unaombaomba. Ie *financial independence* ilikuwa haipatikani. Kwa maana hiyo basi, kipindi chote hicho kimepita na Muswada umeletwa Bungeni leo. Kutokana na hali hiyo, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali iliyopo kwa kupitia Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati wa Bunge, Muswada huu umeletwa Bungeni na maana yake wameletewa Watanzania, waipе mamlaka Mahakama iweze kufanya kazi vizuri kupitia Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Muswada huu ni kuiweka Mahakama katika mazingira yaliyo bora na mazuri na ya ufanisi ili Majaji wetu waweze kufanya

kazi kwa utulivu na sehemu zote za maendeleo ya Mahakama zishughulikiwe na anayehusika (*Chief Court Administrator*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wamesema kwamba huyu *Chief* amepewa madaraka makubwa, lakini huyu yuko chini ya *Commission*. Kwa hiyo, *Commission* ndiyo yeye mamlaka ya mwisho kabisa katika uendeshaji wa Mahakama hizi. Kwa hiyo, wasiwe na hofu kwamba labda *Chief* huyu atatumiwa kwa njia nyingine, *Commission* ndiyo ambayo itakuwa inawajibika. Ombi langu, namwomba Mheshimiwa Waziri kuweka mazingira mazuri katika Idara hii ya Mahakama ili iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 52(1) ambacho kimetoa mamlaka kuwa na Mfuko wa Mahakama ambao utasimamiwa chini ya Kifungu 82(3). Serikali iwe makini kuhakikisha Mfuko huu unaendeshwa vizuri na kuondoa matatizo ambayo yameikabili Mahakama hii. Kwa mfano, majengo ya Mahakama, ukielezwa kuwa hili ni jengo la Mahakama, kama hiyo itakuwa ndiyo ofisi ya Hakimu, basi utaona hapa hakuna haki. Lile jengo lenyewe tu linakupa picha halisi. Naomba Mfuko huu utumike vizuri ili kuweza kuleta heshima kwa Mahakama zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri, Mahakimu wetu wanaposafiri, wanasafiri na watu ambao wamewaweka rumande wao wenyewe wamo kwenye gari. Watu ambao wamewafunga wao wenyewe, wanasafiri nao. Kwa hiyo, inakuwa usalama wa Mahakimu wetu unapotea na ni hatari sana. Kwa hiyo, nadhani Waheshimiwa Wabunge, mkiujadili Muswada huu, mtaweza kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi, tunao vijana wetu ambao wako rumande. Ukienda kule rumande, utafikiri labda huko nje hakuna watu. Ukiuliza, utaambiwa hatuna pesa za mashahidi. Mahakimu siku zote wanaendesha kesi na kuendesha kesi ni kuita ushahidi na mashahidi lazima walipwe. Angalieni ni Mahakama ngapi Tanzania zipo ambazo zinahitaji fedha kila siku katika uendeshaji wake ili kuwezesha uendeshaji mzuri. Waheshimiwa Wabunge, zingatieni Muswada huu ili upite na kesi zetu ziweze kusikilizwa vizuri na vijana wetu kule waweze kuondolewa tabu ambayo wanaipata kule rumande. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine zaidi, Mahakama zina matatizo hata vitu vya utendeaji kazi, yaani hata *stationeries*. Mahakama inakwenda kuomba karatasi katika Wizara, katika Idara fulani. Mahakama ile *tag* ya ku-*file*, wanakwenda kuomba, wanafungua uzi. Hiyo ni aibu kweli kwa Taifa la Tanzania. Naomba kwa heshima kabisa, Waheshimiwa Wabunge tuupitie Muswada huu ili hili tatizo tuweze kuliondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rashid Abdalla. Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nikushukuru kuweza kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, niseme kwamba Upinzani si kupinga kila kitu na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwamba hawako katika kupinga lakini wako katika kuelekeza. Kwa hiyo, tuielekeze Serikali ili iweze kuendesha nchi yetu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda moja kwa moja nianze na Kifungu cha 4(2) cha Muswada huu ambacho kimeonyesha nia ya mgawanyo wa mamlaka ya kiutawala katika Mahakama zetu. Katika Kifungu hiki, mamlaka ya kiutawala kwenye Kifungu cha 4(2) kimegawika katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwanzo limefafanuliwa kuwa ni Maofisa wa Mahakama ya Rufaa, Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Majaji wote, Mahakimu wote, Wasajili wote pamoja na Makarani na Watumishi wengine wa Mahakama. Eneo la pili, katika mgawanyo wa mamlaka ya kiutawala ni kundi la *Non-Judiciary Officers*. Hawa ni wafanyakazi ambao wanafanyakazi Mahakamani lakini hawana mamlaka ya kuweza kutoa hukumu katika Mahakama zetu.

Hili ni suala la msingi kwani litatoa fursa kwa Majaji na Mahakimu wetu kuweza kufanya kazi zao kwa uangalifu na kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni *Judiciary Service Commission*, hiki ni chombo ambacho kipo, lakini kinaonesha kwamba kimebadilishwa kiutawala, mfano ukienda kwenye Kifungu cha 13 cha Muswada huu, kumeelezwa kwamba kazi za *Commission* hii ni kumshauri Rais katika mambo yafuatayo:- Kwanza, kufanya uteuzi wa Jaji Kiongozi na Majaji wa Mahakama Kuu. Pili, kuteua *Chief Court Administrator*, kumteua *Chief Registrar* na *Registrar of High Court*. Ukienda Sehemu ya Nne katika Kifungu cha 29(1)(a) kinatoa tena fursa ya kumshauri Rais kwa kutumia mamlaka yake na uwezo wake aweze kuondoa wale Majaji ambao watathibitika kwamba hawana uwezo wa kutumikia sehemu walizopo kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni mmoja kwamba inawezekana kuna wafanyakazi ambao wana uwezo katika sehemu ile lakini watu ambao wamewekwa au amewateua Rais katika kumshauri ikawa hawawapendi watu wale waliopo pale licha ya kwamba wana uwezo wakajenga fitina ili waweze kuondolewa. Katika hili naamini Rais ana uadilifu mkubwa na kwa hiyo katika washauri wake pia awe na vyombo vingine ambavyo vitaweza kuchunguza endapo kesi kama hizi zitatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hicho cha 29(e) *Commission* itakuwa na uwezo wa kuwapandisha Vyeo Mahakimu, vilevile kuna Mahakimu ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu, ni waadilifu, ni wafanyakazi bora lakini nafasi za kupandishwa vyeo kwao ni za mbinde. Nikitumia Kiswahili cha mbinde wengine hawatafahamu, lakini

kupandishwa vyeo kwa wao kuna ugumu. Hivyo basi naomba na nashauri, namtaka Kiongozi wa *Commission* hii ambaye ana mamlaka aweze kuangalia wafanyakazi na kuwapatia haki zao stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 52(1)(2)(3), kila msemaji amechangia Kifungu hiki kutokana na umuhimu wake. Suala la kuwepo Mfuko wa Mahakama ni suala muhimu na linahitaji uwezeshwaji. Tunasema kwamba nchi yetu inaongozwa na mihimili mitatu, Serikali, Bunge na Mahakama, ni ukweli usiopingika kwamba Mahakama zetu bado hazijawa huru kwa sababu ni ombaomba. Nikubaliane na kauli aliyoitoa Mheshimiwa Khalifa juzi kwamba wengine wanaomba na tai na wengine wanaomba na 'Nongo'. Ukimtazama Hakimku kwenye Mahakama namna alivyovalia tai basi utafikiria anapoishi ni pazuri kweli kweli, lakini nenda hapo anapofanya hiyo kazi ya mahakama, utashangaa. Sasa umefika wakati Mahakama sasa kiwe ni chombo ambacho kinajitegemea. Siku zote Mahakama inategemea ruzuku kutoka Serikalini kwa nini? Umefika wakati sasa Mahakama zetu ziwezeshwe na kama kuna madeni ya aina yoyote zitafutwe njia zozote yalipwe ili heshima ya nchi iweze kubakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kutoa mchango wangu kwa Muswada uliopo mbele yetu. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wakati huu maana utasaidia sana kuongeza ari na nguvu ya Mahakimu na Watendaji wengine waliopo katika Mahakama. Kama wenzangu walivyosema kwenye taasisi hiyo kuna matatizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wafanyakazi waliopo kwenye maeneo hayo kwa namna wanavyofanya kazi katika mazingira magumu lakini wamekuwa wakidai haki zao kwa utaratibu ulio mzuri sana. Maana wengine wamezoea jambo dogo tu wanaandamana lakini hawa wametumia busara na umahiri wa hali ya juu katika kudai kile kilicho stahili yao, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, taasisi hii ina tatizo la vifaa, Mahakimu wachache, ina matatizo ya aina nyingi, nashukuru kwa kuleta Muswada huu lakini napenda kusema ndugu zangu Roma haikujengwa siku moja, ndiyo maana Muswada huu umeletwa ili tufanye marekebisho kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa. Naamini nia ya Serikali ni kuepukana na matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka nina mchango wa Muswada wenyewe kama ifuatavyo. Naomba kuishauri Serikali kwenye Kifungu cha 7(1) pale Mtendaji Mkuu anapopewa sifa nyingi kama zilivyoorodheshwa katika Kifungu cha 7(3), naomba liongezwe suala la kwamba Mtendaji huyu ni lazima awe na *knowledge* ya sheria angalau Digrii ya Kwanza, kwa sababu anafanya kazi na watalaam walioboea kwenye sheria, itakapohitaji majadiliano ya msingi na ya hoja kama hatakuwa aliyeboea kwenye sheria

watamuacha mbali sana. Kwa hiyo, nashauri Mtanzania yeyote mwenye uwezo lakini *knowledge* ya sheria iwe *mandatory* kwa mtendaji huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni Kifungu cha 9 pale inapotajwa kuwa Mtendaji Mkuu, mamlaka yake ya nidhamu iwe Rais, mimi naomba tufanye mabadiliko kidogo, mamlaka ya nidhamu iwe Tume na *appellate board* ya Mtendaji huyu iwe *President* ambapo itakuwa ni *final and conclusive*. Kwa kufanya hivi tutaijengea heshima Tume yenyewe na watafanya kazi kwa umahiri na heshima na kusimamia ile Tume ya Mahakama lakini kitu kidogo kwa Rais, mimi naona haipendezi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tatu ni kuhusu Kifungu cha 10(b) pale Mtendaji Mkuu akiwa hayupo kwa siku thelathini basi Jaji Mkuu ashauriane na Tume kwa ajili ya kumteua mtu kukaimu nafasi hiyo. Ninavyoona kazi za mtu huyu zitakuwa nyingi na mara nyingi atakuwa anasafiri, sasa kila wakati Jaji Mkuu anapeleka kwenye Tume, wanafanya vikao, nashauri tumwekee mtu ama *Deputy* Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili asipokuwepo anafanya kazi zake mara moja au hata *Registrar* wa *High Court* tumweke kwenye sheria kwamba Mtedaji Mkuu asipokuwa basi yeye atakaimu nafasi ile ili kuondoa *unnecessary delay* ya mambo ya msingi yanayotakiwa kufanywa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa kwa wananchi kukosa haki na kufuata haki zao mbali na wanapoishi. Watanzania wengi wanaishi vijijini lakini huduma hii ya kupata haki kwao ni shuruba. Naishauri Serikali iongeze fungu la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo na nyumba za Mahakimu kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Sehemu ya Sita kuna kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama katika sheria hii, lakini hii isiwe tu kwa sababu tumeweka hapa tukawa tunawapelekea fungu dogo, tuhakikishe jitihada za makusudi tunafanya ili wenzetu hawa hasa kule vijijini waweze kufanya kazi *comfortably*, wana matatizo makubwa. Juzi hapa baadhi ya Mahakimu wamepata pikipiki lakini wanashindwa kupata posho ya mafuta wala posho ya matengenezo ya pikipiki hizo, bado hali ni ngumu. Nadhani Serikali iamue kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ulinzi wa Mahakimu na Majaji wetu hawa, mambo yamebadilika sana, tulikuwa tuna amani nzuri Watanzania lakini kuna dosari ndogondogo hapa zimeshaanza kujitokeza. Tusipowapa ulinzi wa kutosha siku moja tutakuja kujilaumu hapa. Ni vema tuhakikishe tunawatengeneza mazingira mazuri ya ulinzi Mahakimu na Majaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kushauri, kwa sasa tuna watalaamu wengi sana wenye Shahada za Sheria za Vyuo Vikuu au Diploma lakini wanasaga lami pale Mjini hawana kazi, kwa nini wasomi hawa tusiwapeleke basi kwenye ngazi ya Mahakama ila tuwalipe mshahara unaofanana na taaluma zao, maana kwa kwenda kule watatusaidia kupunguza kurundikana kwa kesi zilizopo kule na vilevile kufuata mbali huduma hiyo. Nami naomba tufanye juhudi za makusudi hata Mawakili sasa waende kwenye Mahakama za chini ili wasaidie kupunguza matatizo yaliyopo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na mchango huu, nakushukuru sana, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

MHE. CHIKU A. AMBWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, napenda nimpongeze sana Spika, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Spika, nampongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote watatu ukiwemo wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie fursa hii kuwapongeza viongozi wangu wa CHADEMA kwa jinsi walivyoweza kukiendesha chama chetu vizuri na hatimaye kuweza kupata Wabunge wengi kwa kiwango ambacho kinatia moyo katika utendaji wao wa kazi. Natumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa hasa Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Freeman Mbowe ambaye ni Kiongozi wetu wa Upinzani, kwa jinsi anavyotumia hekima na busara kuongoza Chama cha Demokrasia na Maendeleo kwani angekuwa ni kiongozi wa wasiwasi leo nchi hii isingetawalika, amekuwa akituliza ghasia, amekuwa akiwasihi wananchi watulie na yote hayo yanafanyika, nampongeza sana. Mwisho, nimpongeze Msemaji Mkuu wa Masuala ya Kisheria wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa umahiri wake wa uchambuzi wa Miswada, hakika amekuwa msaada mkubwa sana wa kuweka mambo sawa katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu mimi sikuangalia sana kuchangia vipengele vya kisheria ukizingatia mimi siyo Mwanasheria lakini kwa sababu naamini Muswada huu umeletwa ili kuboresha utendaji wa shughuli za Kimahakama na kwa msingi huo mimi nasisitiza ili haki itendeke katika utendaji wa shughuli za Kimahakama, ni lazima wawezeshwe kifedha kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alivyosema kwamba bajeti imekuwa ikipangwa lakini haitoshelezi, hata kwa uchache huo lakini bado haitoki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Mahakama wamekuwa wakilaumiwa sana kwamba hawatendi kazi zao vizuri, kesi haziishi, lakini tatizo ninaloliona ni upande wa Serikali kwa sababu Serikali ingekuwa inawajibika ipasavyo, ingekuwa inatenga na kutoa pesa kwa kiwango cha kutosha, Mahakama zikafanya kazi kwa upana wake, heshima ya Mahakama ingekuwepo, haki ingetendeka, kesi zingekuwa zinaisha hata wao wangekuwa na moyo wa kufanya kazi kwa uhakika zaidi. Ni ukweli usiopingika kwamba Mahakimu wote na Majaji, ni watu wanaostahili kupata pongezi nyingi sana pamoja na kulaumiwa sana na wananchi, kwani wanafanya kazi zao katika umaskini uliokithiri, wanakosa hadhi ndiyo maana wale wenye roho nyepesi wanaweza wakajiingiza hata katika matendo ya kupokea rushwa na zawadi ndogondogo ambazo zinasababisha mtu asitende haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, Serikali inachangia mambo mengi, kuna kesi nyingi ambazo tumeona zinakaa miaka mingi, haziishi kwa sababu ya Mahakama kukosa pesa. Kesi zimekuwa zikiahirishwa kila siku ukiacha taabu wanazopata Watendaji wa Mahakama hata wananchi wanateseka sana kudai haki. Kama alivyoongea Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba hata Mahakama zenyewe ni chache, Kanda za Mahakama Kuu ni chache, watu wanatoka mbali kwenda kufuata Mahakama, wanatumia gharama kubwa hatimaye hata kama alikuwa na haki katika ile kesi anaamua kuacha kwa kuona usumbufu anaoupata, ni bora apate hasara moja inayojulika, kwa sababu hata kesi huna uhakika wa kushinda mia kwa mia. Kwa hiyo, wengi wanaamua kufuta kesi, wanaacha haki zao zinapotea. Mifano, hata kwa kesi za uchaguzi uliopita, kuna kesi ambazo ziko Mahakamani, watu wanadai haki zao ili uchaguzi uweze kurudiwa tena mpaka leo hii tunavyoongea zile kesi imebidi zife kutokana na kupitwa na wakati. Yote haya yanasababishwa na ukosefu wa Mahakama na uwezo wa kifedha wa kuendesha kesi na kufanyakazi kwa ufanisi, matokeo yake haki hazipatikani. Nchi yoyote ikikosa haki siku zote italeti machafuko, amani haitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tudumishe haki inabidi huu Muswada kama ulivyoletwa kwa nia njema kama nilivyosema ya uboreshaji utendaji wa shughuli za Mahakama iwe ni pamoja na kuhakikisha kwamba Mahakama hiki zinaboreshwa, zinapata fedha za kuwawezesha kufanya kazi, Majaji, Mahakimu wapate mishahara mizuri, wafanye kazi kwa kujituma wakiamini kwamba ile kazi inawawezesha na wao kuishi katika maisha yaliyo bora, hali kadhalika haki tutaipata na heshima ya Mahakama itarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliona niseme hilo kwa uzito zaidi ili litiliwe uzito liendane hasa na hii hali nzuri ambayo tumeamua kuboresha Mahakama, siyo kwa maneno ndani ya Bunge hatimaye tunaacha tu Muswada ukishapita hapa utekelezaji hakuna. Matatizo ya Mahakama ni kilio cha miaka yote, toka mimi nimepata akili Mahakama zinalalamika tu, watumishi wa Mahakama wanalia tu, umaskini ndio ule ule, Majaji hawaheshimiki kwa sababu ya umaskini, hawa maskini wadogo ndio usiseme kama alivyoongea Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hata tai zenyewe wanaomba kitu ambacho kwa kweli ni fedheha kwa Taifa letu, Taifa ambalo tumekuwa tukijivunia, Taifa ambalo tunasema sisi tutahakikisha tunaleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Maisha Bora kwa kila Mtanzania hayapatikani kama hatuwajibiki ipasavyo tukiwajibika ndipo maisha bora yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Chiku. Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee na Mheshimiwa Jerome Bwanausi halafu Mheshimiwa Henry Shekifu atafuatia.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria wa

Uendeshaji wa Mahakama. Lakini kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kabisa kuchangia Muswada wa Sheria katika Bunge letu hili, nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Lulindi ambao wamenipa dhamana ya kuwa Mbunge wao na napenda kuwathibitishia kwamba nitafanya kazi kwa nguvu zangu zote na sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia, lengo kubwa la Muswada huu ni kuona ni jinsi gani tunaboresha shughuli za Mahakama. Kwa kweli niipongeze Serikali ya CCM kwa kuamua kuleta Muswada huu kwa wakati huu kwa sababu hii ni ishara tosha kuonyesha ni jinsi gani Serikali yetu ilivyo sikivu pale inapoona kuna jambo muhimu la kuweza kulirekebisha kuweza kuleta Muswada ili kufanya marekebisho pale ambapo mambo hayaendi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hali ya mwenendo kwenye Mahakama zetu ukianzia watumishi pamoja na Majaji, Mahakimu hali si nzuri sana. Inahitaji uboreshaji mkubwa sana ili hawa wanaotoa haki kwenye nchi yetu waweze kufanya kazi hiyo kama ilivyotarajiwa. Tatizo kubwa sana ni ukosefu wa fedha za kuendesha shughuli za Mahakama. Kwa kuwa Serikali imetuletea Muswada huu ambao unaonyesha kutakuwa na Mfuko wa Mahakama ni dalili tosha kwamba inawezekana yale ambayo yalikuwa ni kero na matatizo kwenye Mahakama yakapata ufumbuji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nipongeze Muswada huu kwa kuamua kumweka Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Ni kweli kabisa ilikuwa ni mzigo mkubwa kwa Maafisa wa Mahakama kushughulikia masuala ya Mahakama lakini wakati huo huo kushughulikia mambo ya utawala. Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, kwa kuuleta Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la ukosefu wa fedha limepelekea moja kwa moja pia kumgusa mwananchi wa kawaida. Ninao mfano hai kwenye Jimbo langu la Lulindi, wananchi wanalalamika ni kwa jinsi gani wanagharamia shughuli za Mahakama ambazo zingeweza kufanywa na Serikali kwa kuwapelekea fedha za kutosha. Mfano huu ni kwamba wananchi wanagharamia gharama zote kuanzia mtuhumiwa anapopeleka kwenye Kituo cha Polisi, yule aliyepeleka tuhuma hizo anapaswa apeleke chakula kumpeleka mtuhumiwa lakini hata anapokwenda Mahakamani mwananchi huyu anapaswa atoe fedha za kumsafirisha mtuhumiwa hadi Mahakamani, kibaya zaidi hata kule Mahakamani akishahukumiwa bado mwananchi yule yule aliyepeleka hoja anapaswa atoe fedha za kumsafirisha mtuhumiwa kwenda gerezani. Hii imepelekea baadhi ya wananchi ambao hawana uwezo baada ya mtuhumiwa kutuhumiwa, baada ya siku mbili, tatu, mtuhumiwa anaachiwa kwa sababu hakuna fedha za kumpeleka gerezani. Kwa hiyo, kwa kweli Mfuko huu ambao unaanzishwa ulete marekebisho ambayo mwananchi wa kawaida kule kwenye Mahakama za Mwanzo pia anufaike na Mfuko huu. Hoja sio kuwa na Mfuko na kuwa na fedha lakini kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha ni jambo lingine. Kwa hiyo, ni vizuri sana Mfuko huu ukishapata hizo fedha kuwe na nidhamu ya matumizi ambayo itapeleka kila eneo kupata fedha kulingana na mgawanyo uliotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, mimi nina imani kubwa kwamba Muswada huu tukiupitisha na ukasimamiwa vizuri utaweza kuleta mabadiliko

makubwa kwenye masuala yetu ya Mahakama na kuwawezesha Majaji, Mahakimu na Watumishi kufanya kazi kwenye mazingira mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Bwanausi.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nikushukuru wewe lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Lushoto kwa sababu na mimi ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Muswada, kwa kunirejesha kuwa Mbunge wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze na wale wote ambao wamechaguliwa katika nafasi mbalimbali kuwakilisha Bunge lakini pia niwapongeze wale wana CCM wenzetu waliochaguliwa kuingia kwenye Halmashauri Kuu ya Chama chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Waziri wa Sheria na Katiba kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri, kwa ufupi na kwa kueleweka. Pengine mimi niseme Waziri ana bahati mbaya au bahati nzuri maana suala hili la kuifanya Mahakama kuwa na Tume yake na kujitegemea yenyewe limejadiliwa kwa kipindi kirefu sana. Pengine wengine hatuelewi maana ya hili jambo, lakini ni jambo muhimu sana. Sasa leo mama Kombani ndio amelileta kwa kipindi chake na sasa hivi anakabiliwa tena na kutuletea mabadiliko ya Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamke kwamba mwaka 1995 nilipoingia Bungeni, mfumo wa Mahakama ulikuwa ni Idara. Sisi pia Bunge tulikuwa kama Idara, tulipambana tukafika mahali tukaiomba Serikali, ikaundwa Tume na Bunge likaanza kujitegemea matokeo yake ni haya leo tunaweza kupanga kwa kila tunachokipata kwa yale mahitaji yetu. Sasa leo Mahakama wanapata nafasi hii kwa wale wenzetu ambao walikuwa wanasema kwamba ni kwa nini hili imekuja kwa *Certificate of Urgency*, naamini ni shabaha ya Serikali kwamba jambo hili likamilike na ikiwezekana kabla ya bajeti ijayo basi Mahakama ipewe bajeti yake, ijitegemee na ijifanyie kazi kufuatana na mahitaji yake, naamini ndio lengo. Sasa mtu asiyependa hivyo basi hatutakii mema. Mimi sioni tatizo maana Bunge hili ndilo Bunge la kwanza kutunga Sheria tangu mwaka jana mwezi wa sita, sasa ulitegemea tufanye nini? *Obvious*, ni lazima ije sasa ili tuingize mabadiliko katika bajeti ijayo, ndio lengo la Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa, tunaunga mkono na mimi nitamke mapema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 kwa sababu manufaa ya kuwa na Tume nayafahamu na sisi wote tumekaa kwenye mjengo huu wa heshima zote, umejengwa huu kwa utaratibu wa kuwa na Tume. Tuliamua tukaletewa mpaka na ramani, tukaipitisha kwa kupiga makofi leo tuko kwenye mjengo, tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kuchangia katika maeneo machache, la kwanza ukurasa namba nane, Kifungu cha 7 pale ambapo *the Chief Court Administrator shall hold office on such terms and conditions as the President shall determine*. Mimi nikubaliana lakini pengine ule muda wa kuwa yeye *administrator* ungetamkwa. Uzoefu umeonyesha kwamba mtu anapokaa katika kile Kiti bila kutamka muda ili akajua kwamba kuna *renewal* anazama kwenye Kiti anajisahau. Kwa hiyo, ni vizuri muda ukatamkwa kama ni miaka mitatu, miaka mitano, ukifika muda anajua na saa zote ataangalia muda ili mkataba wake uwe *renewed*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwa haraka haraka katika Kifungu cha 5, suala la nidhamu. Chombo chochote na heshima ya Mahakama ni nidhamu. Bahati nzuri wenzetu hawa wana mfumo, mfumo huu umetamkwa vizuri katika ukurasa wa 20, *Judicial Officers Ethics Committee*, imetamkwa kuanzia Majaji kwenda Kamati za Mkoa na Kamati za Wilaya, utaratibu huu ni mzuri. Nina uzoefu wa Kamati za Mkoa, zilikuwa hazifanya kazi kwa sababu bajeti ilikuwa ndogo. Tunaomba Tume ipeleke fedha za kutosha ili kusimamia nidhamu ya Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kuna eneo lililosahaulika, kuna watu wanaofanya kazi na Mahakimu, Mawakili, sijaona Kamati inayotamka Mawakili hapa. Mawakili wana matatizo, kati yao wako wazuri na wako wabaya. Kuna Mawakili wanatunga kesi ili wapate fedha. Sasa ni vizuri kukawa na Kamati hizo ili kukiwa na malalamiko, Mawakili hawa wafikishwe mahali waambiwe mnavunja sheria. Najua hawa wako chini ya Jaji Mkuu lakini hakuna utaratibu ambao ni *transparent* kwamba huko kwa Jaji Mkuu ni nani wanamsaidia Jaji Mkuu? Kwa mfano, katika ngazi ya Mkoa ni nani anasimamia nidhamu ya Mawakili? Hivi leo Wakili anaweza akaona tu kwamba hii kesi haiendi vizuri akaamua kuichelewesha, anaitwa mbele ya Jaji au mbele ya Hakimu basi anatoa sababu zisizo za msingi kesi mwaka mmoja, wa pili wa tatu, haiishi. Naomba suala hili liangaliwe katika Sheria hii, uwekwe utaratibu ambapo Mawakili *transparently* watawajibika kwa maadili ya utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la Mfuko, ninaamini Mfuko huu unaundwa kwa nia nzuri kwamba sasa kile kidogo kitakachopatikana basi wakigawe kwa kuzingatia umuhimu wa vipaumbele vyao. Ni ukweli usiopingika kwamba si rahisi katika kila maombi yanayopelekwa Serikali yatapata fedha. Hakuna Serikali duniani kote, leo Obama analalamika anakata matumizi ya Serikali, sembuse sisi. Ndugu zangu tuyasikilize haya, tusizungumze tu kwa kulaumu, mnataka kupewa Serikali, mtapewa lakini si rahisi kama mnavyoona. Kile kidogo chenye kupatikana kikigawanywa vizuri ndicho kitaleta tija ndio maana ya mfumo huu wa kuipa Mahakama sasa jukumu la kupanga wenyewe, wapange vipaumbele vyao na wavisimamie kwa ajili ya utekelezaji mzuri, hilo ndio lengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo sasa hivi lina mgogoro mkubwa na kwa kweli wananchi wanalilalamikia sana ni hili eneo la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mahakama nyingi hazina Mahakimu na tatizo kubwa ni kuwapata Mahakimu lakini vilevile tatizo la fedha. Tunacho Chuo cha Mahakama Lushoto, Chuo kile hakijapewa msisimko mkubwa wa kutosha ili tufundishe Mahakimu wa kutosha na

tuondoe pengo hili la Mahakimu. Naiomba Tume katika vipaumbele muhimu ni pamoja na kufundisha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Imefika mahali leo Hakimu anakwenda Mahakama kilomita 20, 30 kusikiliza kesi, anatoka maeneo hayo na pikipiki huku amehukumu, watawamaliza hawa. Tunaomba sana suala hili la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo liangaliwe kwa undani na Chuo cha Lushoto kipewe umuhimu wa kwanza. Naipongeza Serikali hata hapo walipofikia, Chuo kile kilianza na majengo ya zamani sasa hivi juhudi zimefanyika, hosteli zinajengwa na ninaamini tukiongeza juhudi zaidi Chuo kile kitakuwa na ufanisi na tutapunguza pengo la Mahakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni usimamizi wa fedha hizo. Msimamizi/Mtawala Mkuu kazi yake kubwa ni kuangalia utawala. Kulikuwa na hofu kwamba huyu amepewa madaraka makubwa, si kweli, kama ilivyosemwa, yuko chini ya Kamisheni, pia hata katika sheria hii ametamkwa atamsaidia Jaji Mkuu. Kwa hiyo, kiongozi wake Mkuu kwa kweli ni Jaji Mkuu kama vile sisi tulivyo kwamba katika muhimili huu, Kiongozi Mkuu ni Spika na hawa, Jaji Mkuu bado atakuwa na mamlaka ya kiutawala kutoa maelekezo, kwa hiyo, ule wasiwasi hautakuwepo. Tunachosema amsaidie Jaji Mkuu, asaidie Mahakama kupanga mipango mizuri, kupanga vipaumbele muhimu ambavyo tuna uhakika hizi kero zilizopo sasa zitatatuliwa, upungufu uliopo sasa utaangaliwa kwa undani. Mimi nina uhakika kama tulivyofanikiwa kwa upande mhimili wa Bunge, nina uhakika kwa utaratibu wa sheria, mhimili unaoitwa Mahakama utafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia nzuri ya Serikali ni kubwa sana, nimshukuru sana Waziri na tumtakie kila kheri Serikali yetu kwa usikivu. Tuisikie maneno, hii ni Serikali yenye usikivu, hakuna jambo ambalo linatamkwa katika shida Serikali haitasikiliza. Mimi nawashukuru sana Mawaziri kwa jinsi mnavyotusikiliza na jinsi ambavyo mnashirikiana nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwa ufupi katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa nia njema ya kutaka kuleta maboresho katika Mahakama zetu. Toka jana, juzi tumekuwa tukishughulika na mambo muhimu sana kwa ajili ya Taifa letu ambalo sisi wote kama Wabunge tunapaswa tuyachangie na kuyajadili kwa kina na kwa faida ya Taifa letu maana kazi tuliyonayo *is not permanent job* kesho tutakuwa mitaani na hata zile *privilege* zingine ambazo tunadhani tunazo zitakuwa hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa Mahakama ni chombo muhimu sana na mhimili muhimu katika Taifa. Taifa lolote ambalo linacheza na chombo muhimu kama hiki, linahatarisha amani ya nchi. Napenda kushauri Wabunge wenzangu na Waziri na Wizara inayohusika, Watanzania wengi wamekuwa na hoja, Watanzania wengi wamekuwa na mashaka, ni kwa sababu mahali pekee ambapo wanategemea haki inaweza kupatikana, imekuwa haipatikani. Kama Taifa, mahali pekee ambapo mwananchi

anaweza kukimbilia, tukipachezea, tusipopaimarisha, hapo ni mahali ambapo panaweza pakasabisha machafuko ya nchi. Mahakama inapokuwa inafanya kazi yake kama inavyopaswa, ni mahali ambapo demokrasia ya kweli inaweza ikawa *practiced*. Nchi zozote duniani ambazo zinashughulika au zinadamisha demokrasia ya kweli, Mahakama ni mahali ambapo watu wake wanakimbilia, wana uhakika ya kwamba haki itakwenda kutendeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania ambayo tunaamini kwamba demokrasia yetu ndio inakuwa, inashangaza unamwona hata Mbunge anashangaa mtu akiandamana, haamini maandamano ni sehemu ya demokrasia. Hii inadhihirisha kwamba katika Taifa letu demokrasia bado ni changa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaposhughulikia suala la Mahakama, Mahakama ikiimarishwa, Mahakama ikiwa inatoa haki, Mahakama ikiwa hamnyanyasi mtu, hapo ndipo demokrasia ya kweli inaweza ikatendeka na watu wakakimbilia kwa sababu kuna kimbilio la maana. Ndugu zangu, Mahakama zetu kama wenzetu walivyosema zimekuwa na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa kidogo Mheshimiwa Waziri pamoja na sababu ambazo zimetolewa hapa za kuleta Muswada huu lakini sijapata sababu kubwa katika hotuba yake kwa nini tunabadilisha mfumo huu wa sasa kutoka ule mfumo wa zamani. Katika ule mfumo wa zamani *what was the problem, what was the route cause* na kwa nini tuhamie sasa katika mfumo mpya, tungeweza tukajibu hayo matatizo. Kwa hiyo, tunapohama katika ule mfumo wa zamani tunaweza tukawa tunabadilisha rangi ya daladala lakini injini bado ni ileile. Kwa hiyo, haiwezi kutusaidia kama hatujajua chanzo cha matatizo ilikuwa ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu, nilikuwa nadhani pamoja na mambo mazuri ambayo Serikali inaweza ikawa inayaleta lakini vilevile kama Taifa tuna matatizo ya *ethics, morals* na *mindset*. Tunaweza tukawa na Miswada mizuri na taratibu nzuri lakini kama *mindset* za watu hazijabadilika bado tatizo litazidi kuendelea. Nilitegemea katika Muswada huu kuwe *at least* na jambo fulani ambalo linawalazimisha hawa watumishi wa Mahakama kwa namna moja au nyingine kwamba wajikite kuhakikisha kuna maadili fulani ambayo tunayategemea kwa mtumishi wa Mahakama na mtazamo mkubwa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Lakini kikubwa zaidi ambacho binafsi ninadhani ni chanzo kikubwa cha matatizo katika Mahakama zetu ambazo wenzangu nao wametangulia kuzungumza ni tatizo la fedha. Mahakama zetu zimekuwa hazina fedha za kutosha ambayo inaweza ikasaidia zifanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza mwanzo, nchi za *Scandinavia* kwa mfano mahali ambapo demokrasia inafanyika vizuri, mtu anapopata ushindi wa asilimia themanini na kitu, asilimia tisini, anaonekana ni *dictator* kwa sababu kuna mawazo tofauti huwezi kupata ushindi wa namna hiyo au mtu anapopita bila kupingwa ni u-*dictator* kwa sababu hamwezi kuwa na mawazo yanayofanana. Kwa hiyo, tunapokuwa na Mahakama zinazotoa haki, kutakuwa na ushindani wa nguvu, watu watahindana kirahisi bila woga, wata-*exercise* uhuru wao katika Taifa lao bila woga, hapo tutasema

Mahakama inafanya kazi kwa sababu wanajua kama mtu akimwonea atakwenda katika chombo ambacho kitampa haki, kimuonyeshe njia, atapata usalama katika Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika watu wengi hapa wako Chama Tawala si kwa sababu wanapenda, wanasukumwasukumwa kwa sababu wanaogopa. Sasa tukiwa na Mahakama zenye nguvu, zenye uhuru, watakuwa na uhuru kujiunga na Vyama vyovyote ili mradi wa-*exercise* uhuru wao. Wengi wana *suppress mind* zao, hawana uhuru, *they don't speak their mind* kwa sababu wanaona haki haiwezi kupatikana, kwa hiyo, wanajificha. Leo hii hata akifanya biashara yake anajificha, unasikia CCM wataniona, kwa nini wakuone katika nchi yako kama kweli wewe unafanya mambo yako ya haki, uko katika Mahakama inayotoa haki? Haya ndiyo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mahakama zetu tuziboreshe, tutoe fungu zuri, walipwe vizuri, tuwatunze vizuri ili wananchi wa Tanzania wawe na uhuru kama Katiba yetu inavyosema nchi ni ya kidemokrasia ili *to practice* demokrasia kwa kiwango cha juu sana. Watu wanaogopa kufanya demokrasia kwa sababu haki haipo na watu wengi wanakaa humu ndani wana-*suppress mind* zao. Sasa tukianza katika Bunge mtu hawezi ku-*speak his mind* ana-*suppress mind* huko nje wananchi watakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningepomba wananchi wote bila kujali itikadi za Chama...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, hebu naomba ukae kidogo. Ziko Kanuni zetu ambazo zinatuuongoza Waheshimiwa Wabunge, kwanza, unapoongea unamwa-*address* Mwenyekiti, sasa unachangia mawazo yako mazuri halafu unatoa viashiria vya kuwafanya Wabunge hawa humu ndani mawazo yao ni finyu, wote huo ni uvunjaji wa Kanuni inavyosema unatumia maneno ya kuudhi watu wengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa naomba uendelee kuchangia mchango wako vizuri lakini umwa-*address* Mwenyekiti na kutumia kigezo cha Wabunge walioko ndani kama ndio kigezo chako wewe cha kujenga hoja, naomba uendelee. (*Makofi*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba nikuangalie wewe. Nilichokuwa nasema kwa sababu haki haipatikani kama inavyopaswa, kwa hiyo, tunajikuta kama Watanzania wakati mwingine tuna-*suppress mind* zetu, tunashindwa kuongea kwa sababu inabidi uwe mnafiki, inabidi ujipendekeze wakati ni Taifa huru, tuna uhuru wa miaka 50, tunatakiwa tutembe kifuu mbele kama Watanzania bila kujipendekeza kwa mtu, bila kujinafikisha ili mawazo ya kila Mtanzania yalete faida kwa Taifa letu, hicho ndio nilichokuwa nakisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, hebu kwa pamoja kama Watanzania, kama Wabunge tunaolipenda Taifa letu, tuhakikishe Mahakama zetu zinaboreshwa, fedha ya kutosha ipatikane ili Majaji wetu wapate heshima ya kutosha kama mwenzangu alivyochangia, wapate ulinzi wa kutosha tuwe na Taifa zuri mahali ambapo tunaweza tukakimbilia, tukapata haki. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na nashukuru kwa kuzingatia utaratibu.

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Kwanza, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba kwa kuleta Muswada huu, ameuleta muda muafaka na umenifumbua macho kwamba kama chombo muhimu hiki cha Mahakama kinaanzisha Mfuko wa Mahakama kwa ajili ya kuboresha shughuli za kiutendaji nadhani ni wakati muafaka na sisi Bunge, maana ni mambo mazuri haya, tuwe na Mfuko wa Bunge kwa ajili ya kuboresha shughuli za Bunge Kikatiba. Kwa hiyo, ni Muswada mzuri sana umetufumbua macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tunaposema kwamba Muswada huu umeletwa kwa dharura na tunajaribu kupinga, mimi sikubaliani na mawazo haya kwa sababu matatizo mengi sana yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na yamesisitizwa sana na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ya fedha mpaka amejaribu kuangalia na Mabunge ya Jumuiya ya Madola, tunakubali Mahakama zetu zina matatizo. Kwa hiyo, matatizo yote haya ndiyo yanayo-*necessitate* Muswada huu uje kwa haraka ili kwenda kuyaondoa. Muswada huu unaonesha jinsi ambavyo Mahakama sasa inajipanga vizuri na kuja na mambo mapya ya Tume ya Mfuko na kuboresha Kamati za Maadili, suala la bajeti linategemeana pia na suala ya jinsi Mahakama ilivyojipanga kwa mujibu wa Sheria. Sasa wanajipanga vizuri, wanakuja hapa watuonesha walivyojipanga vizuri kwa njia ya Sheria halafu tunawazuia wasijipange vizuri, watakwenda kutatua matatizo hayo vipi kwa wananchi? Tuunge mkono Muswada huu, wajipange vizuri ili waondoe matatizo haya yanayowakabili wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo hili la Kamati za Maadili. Wasiwasi wangu ni juu ya elimu ambayo wananchi wetu kule Majimboni wanayo. Pale Jimboni Mwibara, kuna Mahakama mbili za Mwanzo, Kikombia na Nansimo, ni kwa kiasi gani wana Mwibara hawa walivyo na elimu ya kwamba kumbe wanayo fursa ya kisheria ya kwenda kumlalamikia Hakimumu na ni malalamiko yapi ambayo ndiyo yanapaswa kumlalamikia Hakimumu na ni mambo gani ambayo yanapaswa kupelekwa kwenye rufaa kama kesi yake hakutendewa haki? Naomba huu mfuko ambao sasa utanzishwa kuwe na elimu ya kutosha, lisiwe ni suala la siri, wananchi waelewe kwamba wanayo fursa ya kwenda kuwalalamikia Mahakimu na hasa kule kwenye Mahakama za Mwanzo, Mahakimu hawa wamekuwa kama Miungu. Unakuta Hakimumu wa Mahakama ya Mwanzo anaanza kazi saa nne, saa tano, wengine mpaka wanafuatwa majumbani mwao. Sasa ni mambo yapi ambayo wananchi wanapaswa kuyapeleka kama malalamiko na ni yapi ambayo wanapaswa kuyapeleka kwa njia ya rufaa kwenye kesi zao. Kwa hiyo, hilo ni kwenye eneo la hizi Kamati za Maadili, vinginevyo tutakuwa na Kamati za Maadili lakini wananchi hawana uelewa wa namna gani wanaweza wakalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo. Zamani nilikuwa naona hata magari yameandikwa Ukaguzi wa Mahakama za Mwanzo. Ukaguzi huu wa Mahakama za Mwanzo mara nyingi ulikuwa na lengo la kuwafanya Mahakimu kwenye Mahakama za Mwanzo wawe na ufanisi, wanajua wakati wowote watakaguliwa, wanajua wakati wowote watakutwa kwenye vituo vya kazi lakini eneo hili la ukaguzi siku hizi limekuwa ni la kusuasua. Nashauri kwa sababu leo tutapitisha Sheria hii yenye mfuko ndani yake, Mfuko huu uteremke mpaka kule chini kwa njia ya ukaguzi wa Mahakama zetu za Mwanzo ili kuweka ufanisi na wananchi walio wengi kule vijijini waweze kuboreshewa huduma zao kwenye Mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo hili la Washauri wa Mahakama kwa jina maarufu Wazee wa Baraza. Wazee hawa wamekuwa wakifanya kazi kwenye Mahakama zetu za Mwanzo katika mazingira magumu, wengine wanatembea kwa mguu, wanatoka maeneo mbalimbali kwenda kutoa huduma lakini wanaambiwa kwamba watalipwa kwa zile kesi ambazo zimesikilizwa na kutolewa maamuzi. Pamoja na kwamba ziko kesi ambazo zimesikilizwa na kutolewa maamuzi lakini bado Wazee hawa hawalipwi fedha zao kulingana na jinsi ambavyo wameambiwa wakimaliza kesi moja wanalipwa fedha zao. Kitendo hiki kinaashiria nini? Kinaashiria pia kwamba Wazee hawa hawatakuwa makini katika kumshauri Hakimku ili afikie maamuzi ambayo ni ya haki katika kesi hizi. Naomba pamoja na Muswada huu haujaonyesha vizuri nini madhumuni na matumizi ya Mfuko huu, tunashauri kwamba pia Mfuko huu utakapoanza mara moja basi madeni yote ya Washauri hawa wa Mahakama ambayo yamelimbikizwa yalipwe mara moja. Kutokana na hali hiyo, naomba madhumuni na nia hasa ya Mfuko huu yaonyeshwe katika Sheria hii. Si vema kusema tu kwamba kutakuwa na Mfuko wa Mahakama halafu tukaendelea kuonyesha vyanzo vyake, tukaendelea kuonyesha utakavyokaguliwa na taarifa zake zitakavyotolewa, naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika tuambiwe madhumuni ya Mfuko huu na yaonekane katika Sheria hii ambayo leo tutaipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama za Mwanzo kwa mujibu wa takwimu ambazo zimetolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kama kweli Hakimku mmoja anahudumia Mahakama 300 na kitu wakati kwangu pale Mwibara nina Mahakama mbili tu ambazo zinahudumiwa na Hakimku mmoja basi kwa takwimu hizi tutakuwa na Mahakama nyingi sana ambazo zina matatizo.

TAARIFA

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba kuna Mahakimu 759 tu wanaohudumia Mahakama 1105 wakati mahitaji halisi ni Mahakimu 2210 na nikasema kwamba Mahakimu hawa 759 maana yake wanahudumia Mahakama moja moja, kuna Mahakama 346 hazina Hakimku hata mmoja, sikusema kwamba Hakimku mmoja anahudumia Mahakama 346. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sawa ni taarifa ya idadi kamili ya upungufu na idadi kamili ya namba za Mahakama zetu.

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Lakini Wabunge labda kama ni mimi tu hatuna hata hotuba ambayo Msemaji Mkuu wa Upinzani alikuwa anaitoa kwa hiyo, sielewi kama ilikuwa na lengo la kukumbatia hizi takwimu ndio sababu nilikuwa nazungumzia hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola, hebu kidogo tafadhali. Waheshimiwa Wabunge hii taarifa huko kwenye meza zenu hamna?

WABUNGE: Hatuna!

MWENYEKITI: Katibu wa Bunge, taarifa zinapaswa kusambazwa. Kwa hiyo, kuna tatizo kabisa, naomba ufanywe utaratibu wa haraka sana Waheshimiwa Wabunge wapate nakala hizo sasa hivi wakati tunaendelea na mjadala huu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe kama kunatokea tatizo la namna hii, tafadhali muwasiliane na Kiti haraka kwa sababu mjadala hii itaendeshwa kufuatana na takwimu na taarifa kamili ambazo ziko ndani. Kwa hiyo, kama hazijagawiwa, naomba sana Ofisi ya Katibu wa Bunge, hebu tusaidieni Waheshimiwa Wabunge wapate hizo taarifa ili kusudi waweze kuchangia vizuri. (*Makofi*)

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Maelezo uliyoyotoa mwishoni hapa ni mazuri na yamejikita kwenye sehemu ya mchango wangu kwa hiyo, naomba niishie hapo ili wengine na wenyewe waweze kupata nafasi ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lugola na kwa kweli nakushukuru sana kwa kutoa hiyo taarifa ya kutokuwepo kwa taarifa hiyo ya Kambi ya Upinzani.

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na napenda kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Maswa nitaendelea kuwatumikia kwa upendo na mshikamano pamoja na Wabunge, Serikali na mihimili yote kwa ujumla. Naomba niseme ya kwamba fikra chanya zilizotolewa na Muswada huu zimebeba deni kubwa ambalo washiriki wa mhimili wa Mahakama siku zote walikuwa na kiu ya kupata chombo kitakachowasaidia kujiendesha na kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 63(2) ya Katiba inasema:-

“Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikari ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mhimili huu unahitaji changamoto zetu. Matakwa ya Sheria hii yanazaa deni moja kubwa sana la kuwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake. Katiba inasema tuisimamie na kuishauri Serikali. Napongeza kwamba Mheshimiwa Waziri na Kamati wamejitahidi kuchangia kwa kadri ya uwezo wao, maono yao na tumeletewa hapa tutekeleze jukumu la Kikatiba la kuboresha pale penye upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutambue vilevile kwamba Muswada huu umekuja na pendekezo tupu katika matakwa ya Ibara ya 52 kuhusu masuala ya upatikanaji pesa kwa ajili ya Muswada huu. Serikali Kuu wakati umefika baada ya miaka 50 ya uhuru tuwe na maamuzi magumu ya kuthubutu kwa kuweka msingi mzuri kwa miaka 100 ijayo ambapo Mwenyezi Mungu atakuwa sisi ametutanguliza mbele ya haki lakini watoto hawa watauliza, hivi Bunge walikuwa hawawezi kuwa na uthubutu na ikaona maono endelevu yenye mang’amuzi kwa maslahi ya ustawi wa maendeleo ya nchi na Serikali ikakubali. Naamini Serikali watakuwa watiifu, Serikali ni wasikivu, kwa hiyo, kwa mazuri tutakayoyazungumza katika kuboresha Muswada huu, nina uhakika watakubali. Kusudio langu ni kupendekeza asilimia katika Kifungu cha 52, tupendekeze asilimia inayotokana na ujumla wa bajeti inayokuja. Mhimili huu tuenzi, kama tunataka haki itendeke, kama tunataka utawala bora utekelezeke, kama tunataka Majaji, Mahakimu watekeleze majukumu yao basi tujenge uthubutu wa kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba uwongo humeza ukweli wa kufikiri lakini vilevile napenda kusema kwamba akili za kufikiri tunapokuwa hapa tunazalisha umoja wa fikra. Naomba sana ndugu zangu, kila rika lina haki zake, lakini vilevile kila aliye na subira yuko na Mwenyezi Mungu, itasikitisha sana ukimwona mwenzio ana upungufu ukifikiria jinsi ya kwenda kumnong’oneza na kumtia ujazo, umzomee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tusijaribu kwenda kinyume na matarajio ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu gani nimeyasema haya? Mababu wametuasa kuwa kasuku wa neema na vilevile tuwe radhi na mabaya. Sasa leo tukijiuliza, Mwenyezi Mungu akitujalia kesho, je, tumekuwa nzige wa kuharibu mazao ya umoja na mshikamano? Kwa sababu gani nayasema hayo? Mwongo huzika hamasa ya kupendana, nawaomba sana tuendeleze umoja wa subira ili tuweze kuwatumikia wananchi. Muswada huu unahimiza masuala ya haki na kuwa mbegu ya haki, tunaamini kabisa ni pale tu Bunge hili leo litakapoamua na kuridhia Kifungu cha 52 kiboreshe kwa kusema kwamba watakuwa wanapata si chini ya asilimia mbili ya *total budget* ya nchi hii na bajeti ya nchi hii kwa mujibu wa takwimu nilizopewa, *GDP* imekuwa ikipanda na kama imekuwa ikipanda *we can accommodate these things*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya naona karatasi yangu ya takwimu haipo hapa lakini napenda kukuambia kwamba kama tunataka kweli Sheria zetu zisiwe tamu kwa maneno zije kutafsirika kwa vitendo, *we must be bold enough to decide and be seem to be making decisions*. Naomba mkubali Kifungu cha 52 kiborehwe na kesomeke:-

“Subject to the provision of the Constitution, the sums of money required for the purpose of the Judiciary shall not be less than the two percent of the total Government Budget and shall be paid by the Treasury into the Judiciary Fund”. (Applause)

That is the only mechanism that can resolve all the problems of the judicial system. The integrity of the judicial system depends on financial capacity. If you want really not to see descent in the judicial system, we must make sure that the judicial system is empowered financially. If we are going to fail to empower the judicial system, these are going to be cosmetic arrangements which are not going to be, basi nirudi kwenye Kiswahili. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, , ni vema sana tukatambua kwamba malighafi ya kustawisha na kushamirisha na kunawirisha Sheria hii, ni uwezeshaji wa kipato cha pesa na Bunge hili tuhakikishe Kifungu cha 52 kinabadilishwa. Ikumbukwe kwamba kama takwimu zilivyotolewa, ni aibu sana bajeti ya Mahakama inakuwa shilingi bilioni 52 wanapewa shilingi bilioni moja, bajeti ya Mahakama Kuu wanapewa *ceiling*, sasa ukiweka *ceiling* maana yake na *justice in Tanzania* umeiwekea *ceiling*. (Makofi)

Ndugu zangu, kazi ya Mahakama hii, sisi sote ni wateja wa kutendewa haki, ni wateja tunaongelea kutendewa haki na wananchi wetu wanatutegemea sisi tusimamie ili Mahakama iweze kutenda majukumu yake vizuri. Unapokuwa na *shortfall* ya 49 bilioni halafu Wizara ya Fedha wanangojea bado mwezi mmoja wanapeleka labda bilioni tisa, watatekelezaje *Procurement Act*? Naomba sana na naomba niwaambie ndugu zangu wana CCM na Serikali ya CCM, adui mkubwa ni Wizara ya Fedha, atawang’oa madarakani, kwa sababu maamuzi yote yanayohitaji *funding*, tunapitisha kwa nia njema kule wanatokea wanyampara. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zangu, malengo na shabaha ya Katiba ya CCM yanashabihiana na malengo ya katiba ya nchi, hebu myalinde, sisi kazi yetu ni kuwakumbusha na kuwahimiza. Dhamira yetu ni umoja na upendo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kusema kwamba katika Vifungu vingine, nashangaa sana zile Bodi za Mikoani zisimamiwe na Mkuu wa Mkoa. Hebu tuwape Mahakama uhuru wa kutengeneza Kamati zao. Wilayani *DC* anafanya nini kwenye Mahakama? *This is interference of independency*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waondolewe kabisa hawa watu, hakuna faida hata kidogo. Kama Bunge tuna uhuru wetu hatuingiliwi na Mkuu wa Mkoa na Mahakama tuipe uhuru wake wa kufanya shughuli zake. Katiba ya CCM na malengo ya CCM kayasomeni ndivyo yanavyohimiza. Mpango kazi ndivyo unavyohimiza. Sasa Sheria

mnazozitunga, zikienda kinyume CHADEMA watafanya maandamano msiwalaumu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapenda, tunapendana lakini wakati umefikia tusimamie misimamo itakayolinda ustawi na maendeleo na misimamo ya kumuenzi Baba wa Taifa. Tuenzi wosia wa Baba wa Taifa. Itikadi tunazijua, misimamo tunajua, siasa na uongozi bora tunajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona haya niyahimize kwa machungu makubwa sana kwa sababu kikulacho ki nguoni mwako. Sisi wenyewe tutatafunana lakini umma unahitaji huduma. Kila siku asubuhi mnatusalisha ibada nzuri sana lakini baada ya sala matendo yetu yanakuwa Mswalie Mtume. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa dakika zilizobaki, nafikiri naweza kuruhusu mchangiaji mmoja na nilimwita Mheshimiwa Missanga. Naomba Mheshimiwa Missanga nikupe nafasi sasa ya kuchangia.

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Subhanah Wataala, kwa kunipa nafasi ya kuzungumza kwenye Bunge lako hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hii ni mara yangu ya kwanza katika awamu hii, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba uniruhusu niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Singida Magharibi kwa kunirejesha kwa kishindo kwa awamu hii ya tatu na mimi napenda kuwahakikishia kwamba nitawatumikia kikamilifu. Niombe ushirikiano wao na mimi nitaendeleza ushirikiano kama ambavyo nimekuwa nikifanya siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri, maandishi yaliyoandikwa ni mazuri na yameeleweka. Yeye, Mwanasheria Mkuu na wote nawapongeza kwa hayo ambayo wametuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu kidogo nimpongeze Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Taifa, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi kubwa aliyofanya ya kuvua gamba. Nadhani na wengine watatufuata. Naomba niwapongeze wote wale ambao wameteuliwa kuchukua nafasi za uongozi katika Sekretarieti na Kamati Kuu mpya. Niwapongeze pia na Wajumbe wa Halmashauri Kuu tuliowachagua jana. Matumaini yangu ni kwamba wote kwa pamoja watatufanyia kazi nzuri na kukipeleka mbele Chama chetu Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Nyerere alisema, bila CCM imara na nchi yetu ndiyo hivyo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nimpongeze Mheshimiwa Jaji Mkuu, Majaji, Mahakimu na watumishi wote wa mhimili huu kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. Ni ukweli usiofichika kwamba wenzetu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu

sana. Kulaumu ni rahisi, lakini kutenda ni vigumu. Hata mimi na Mwenyekiti wangu wa Simba hapa ni rahisi sana kulaumu mchezaji akikosa goli, kama yule aliyekosa penalti ya Simba siku ile ya mwisho ile, ni rahisi sana kumlaumu lakini ukiingizwa mle ndani, Missanga haya funga, nitashindwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wenzetu hawa tunawalaumu, wanachelewesha kesi, wanafanya mambo ya ajabu ajabu lakini kazi hii ni ngumu na ni nyeti na ina-*attract* kila mtu. Kwa hiyo, mimi niwape pole lakini niwape pongezi kwa kazi ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa upungufu ambao umesababisha mpaka pengine wakafanya kazi bila kukamilisha majukumu ambayo wanategemewa kuyafanya, ni mengi lakini mojawapo ni hili ambalo linatatuliwa katika kuanzisha Mfuko wa unaoletwa na Muswada huu wa Sheria. Niipongeze Serikali sana kwa kuuleta Muswada huu katika wakati muafaka, nakumbuka ulikuwa uje mwaka jana, kwa bahati mbaya haikuwezekana lakini Serikali kwa nia safi wakaona kwamba ili wajipange vizuri na katika bajeti hii inayokuja tuweze kuingiza haya ambayo yanakusudiwa kutekelezwa katika Muswada huu ndiyo maana nadhani Muswada huu umeletwa katika *Certificate of Urgency*. Kwa hiyo, nawapongeza na ningeomba sisi Waheshimiwa Wabunge tulielewe hilo na tuisaidie Serikali kwa kupitisha Mfuko huu ili tuwasaidie Majaji na Mahakimu wetu waweze kufanya kazi vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mfuko huu kuanzishwa, ni matumaini yangu kwamba upungufu ule ambao ulikuwa umejitokeza kama siyo wote lakini mwingi utakuwa umetatuliwa. Mfano, mambo ya kuchelewesha kesi, wenyewe wataalam wa Sheria hawa siku zote wanasema, *just delayed just denied*, ndivyo wanavyotuongia siku zote. Sasa inawezekana wanachelewesha kwa sababu mbalimbali lakini nasema mojawapo ni ule uwezo wa kuwawezesha kufanya kazi sawasawa. Sasa wa kupitisha Muswada huu, matumaini yangu ni kwamba wataifanya kazi kwa kasi inayostahili, watatoa haki kwa muda unaotakiwa ili wananchi waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya upungufu, mada hii ni ndefu sana inahitaji mtu upewe nusu saa au saa moja, nianze na Mahakama zetu za Mwanzo maana huko ndiko tunakoanzia. Wenzangu wameeleza hapa Mahakama za Mwanzo ni chache ukilinganisha na mahitaji, Hakimu mmoja inabidi apangiwe Mahakama moja au mbili lakini tatizo sasa ni kwamba huyu Hakimu aliyepangiwa Mahakama moja, mbili ama tatu hata kile kipando cha kwenda kule ambako anatakiwa kwenda kufanya kazi hiyo hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nimesimamishwa kwa sababu Hakimu ananifahamu ananiomba nimpe *lift* baada ya kuwahukumu watu kwenye Mahakama sehemu za Ikungi, sehemu ambayo anatoka Mheshimiwa Tundu Lissu, wakati huo kabla Jimbo halijagawanywa, nimemkuta pale anapigwa na mvua, ametoka kuamua kesi, anakwenda mjini, mama wa watu yule Hakimu, kwa kweli nikaona huruma sana. Sasa ndiyo najjuliza, hivi kweli huyu kamhukumu mtu miezi sita, mwaka mmoja, halafu leo anapanda daladala na hao ambao ndugu yao amefungwa, hivi kweli huu si unyanyasaji na udhalilishaji wa mhimili huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, matazamio yangu, hili inawezekana lilikuwa halionekani vizuri zaidi kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Maadamu sasa Mahakama wenyewe wanapata Mfuko wao wa kuangalia vipaumbele vyao, nadhani yale makubwa ambayo walikuwa wanayasema sana kama ndiyo tatizo, nina hakika sasa yatatatuliwa kwa sababu watapata fungu ambapo wenyewe watasema sasa fungu hili ambalo tumelipata tutaliwekeza kama ni kwenye nyumba za watumishi, kama ni maslahi ya watumishi, kama ni usafiri, kama ni kitu gani na kadhalika. Kwa hiyo, matazamio yangu sasa walau malalamiko sasa yataweza kupungua katika eneo hilo. Lakini kwa kweli sitarajii tena kuona Hakimku ameamua kesi halafu unampandisha daladala anarudi mvua inanyesha, hana mwamvuli hana chochote, huko ni kumnyanyasa Hakimku huyo, tena bahati mbaya Hakimku mwenyewe ni mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba niishukuru sana Serikali kwa kutujengea Mahakama ya Mwanzo pale Utemini, Mahakama nzuri, nadhani iko kwenye asilimia 95 nukta fulani kukamilika, ilikuwa ni moja ya tatizo la siku nyingi. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana, karibu sana, naomba siku ya kuja kufungua Mahakama hiyo utuarifu vizuri ili tukupokee na tusherehekee katika kufungua Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi zamani nilikuwa naogopa sana kuzungumzia habari ya Mahakama, habari ya Mahakimu, nilikuwa naona kama vile nashawishi watu wangu, wananchi wangu, wapigakura wangu wafungwe, nilikuwa nachelewa sana, hata wakiniuliza mbona Mahakama yetu mbovu? Nawaambia jamani mimi naogopa, nisije nikaenda Bungeni kule nikasema jamani tunaomba tujengewe Mahakama fulani, watasema badala ya kutuombea kitu kingine, unakwenda kutuombea Mahakama? Lakini ukweli ni ukweli, maadamu tunazungumzia Muswada hapa, ndiyo maana angalau nimepata nafasi ya kulizungumza hili bila ya kuwa na uficho wowote. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili ni nyumba, inakuwaje Hakimku akakae nyumba Uswahilini tu na nyumba yenyewe ukiiangalia maskini ya Mungu ni nyumba ambayo ina matatizo. Huyu huyu ndio unamtegemea kabisa ndiyo akatoe *judgement* Mahakamani za mtu kua, ingawa katika Mahakama za Mwanzo hizi kesi za kua hazipo, lakini hata hizo za wizi na kadhalika, nadhani hili nalo kwa sababu sasa wamepata Mfuko suala la nyumba litatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, matarajio yangu, kama alivyosema rafiki yangu mmoja hapa sijui Msukuma au Mzanzibara au Mzanzibari, ni kwamba katika siku zijazo, jinsi uchumi wa nchi utakavyokuwa unaendelea, nina hakika Serikali yetu itatenga asilimia kamili inayojulikana kwa ajili ya Mifuko yote hii, huu wa Mahakama lakini hata ule Mfuko wetu wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kumwambia mwenzangu pale, alikuwa anauliza, je, sisi Bunge tunao Mfuko kama huu? Bahati mbaya labda alikuwa ameghafilika lakini sisi tayari tulishapata nafasi hii ya kuwa na Mfuko wa Bunge, ambao

ndiyo umefanya kazi nzuri na nina hakika kwa Tume mpya tuliyoichagua, utaendelea kufanya kazi kwa Wabunge pamoja na Watumishi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la usafiri ni moja ya tatizo ambalo limekuwa ni kubwa sana, naamini sasa watajipanga wenyewe, jamani, usafiri utolewe. Lakini vilevile suala la maslahi yanatofautiana sana kati ya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Ya ngapi Mheshimiwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Missanga, ni kengele ya pili hiyo!

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Aaaaah! Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za leo, naomba kwanza niwapongeze wachangiaji wetu wote katika Muswada huu, wametusaidia kuishauri Serikali kwa namna moja ama nyingine ili kuweza kuuboresha Muswada huu kwa miajili ya kuweza kusaidia chombo chetu cha mhimili wa Mahakama kuweza kufanya kazi yake vizuri.

Nimepokea tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, ameniomba niwatangazie Wabunge wote wa CHADEMA kwamba kutakuwepo na kikao muhimu cha Kamati ya Wabunge hao wa CHADEMA, siku ya Jumapili tarehe 17/4/2011 katika ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4.00 asubuhi. Tafadhali mfike wote bila kukosa.

Halafu nimepokea tangazo lingine la kazi kutoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Anasema kwamba tafadhali naomba uwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuwa kutakuwa na kikao kifupi cha Kamati, Jumamosi tarehe 16/4/2011, kitakachofanyika mara baada ya kikao cha uchaguzi wa CPA katika ukumbi wa Pius Msekwa C, wajumbe wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yaliyokuja hapa Mezani na baada ya matangazo haya shughuli yetu ya leo tunaahirisha na naomba niahirishe shughuli hii mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumamosi, Tarehe 16 Aprili, 2011, Saa Tatu Asubuhi)

